**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 14 Juni, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge itakumbukwa kuwa, katika Mkutano wa Bunge wa Saba, Bunge hili pamoja na shughuli nyingine lilipitisha Miswada ya Sheria ya Serikali Tisa. Kati ya Miswada hiyo, Miswada Saba tayari imepata kibali cha Mheshimiwa Rais na sasa ni Sheria ya Nchi kama ifuatavyo:-

1. *The Land Use Planning Act*, 2007 ni Sheria sasa Namba 6 ya Mwaka 2007

2. *The Town Planners (Registration) Act* 2007 sasa ni Sheria Namba 7 ya 2007

3. *The Suplementary Appropriation (for Financial Year* 2003, 2004) *Act*, 2007 ni Sheria Namba 9 ya Mwaka 2007

4. *The National Bank of Commerce (Re-Organization and Vesting Assets and Liabilities) Act, 2007* ni Sheria Namba 10 ya Mwaka 2007

5. *Prevention and Combating of Corruption Act, 2007* ni Sheria sasa Namba 11 ya Mwaka 2007

6. *Optometry* A*ct* ni Sheria Na.mba 12 ya 2007

7. *The Fire and Rescue Act, 2007* ambayo ni Sheria Namba 14 ya Mwaka 2007.

Kwa taarifa yenu Waheshimiwa Wabunge Miswada miwili iliyobaki yaani: "*The Urban and Planning Bill 2007"* na "*The Roads Bill, 2007*" haijapelekwa kwa Mheshimiwa Rais kwa sababu bado ipo kwa Mpigachapa Mkuu wa Serikali ikiwa katika hatua zake za mwisho za uchapishwaji.

Mtakumbuka kwa mfano ule Mswada wa "*Roads Bills*" ni mrefu sana una majina ya barabara zote nchini na kadhalika. Siyo rahisi kuuchapa kwa haraka na ukaupatia kwa usahihi. Ikishakamilika nayo itapelekwa kwa Mheshimiwa Rais ili ipate kibali chake. Naomba niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge Miswada hiyo itakapopata kibali cha Mheshimiwa Rais nitakuja kuwafahamisha hapa Bungeni. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:**

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2006 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2007/2008.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULLO)**

Taarifa ya Sera za Fedha kwa kipindi cha Mwaka 2006/2007 na Mwelekeo wa Sera za Fedha kwa Mwaka 2007/2008.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 21

### Ofisi za Wabunge Majimboni

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Masharti ya Kazi ya Mbunge kifungu cha 13 kinaeleza kuwa, Mbunge wa Jimbo atapewa Ofisi na vifaa vya ofisi na Serikali; na kwamba, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa itahakikisha upatikanaji wa vitu hivyo. Lakini nilipotoa hoja katika Mkutano wa Bajeti 2006/2007 kuhusu suala zima la Ofisi za Wabunge, Serikali ilinijibu kuwa, itaiwezesha Ofisi ya Bunge ili iweze kuwapatia Wabunge Ofisi zinazofanana na majukumu waliyo nayo:-

(a) Je, ni lipi jibu sahihi kati ya majibu hayo mawili. Je, ni lile lililo kwenye Masharti ya Kazi ya Mbunge au ni lile la Ofisi ya Bunge kuwezeshwa kuwapatia Wabunge Ofisi hizo?

(b) Katika Bajeti ya Mwaka 2006/2007. Je, kila Mbunge wa Jimbo alitengewa fedha kiasi gani na ni kiasi gani cha fedha kimeshatolewa?

(c) Je, katika Jimbo la Kibaha Mjini ni kiasi gani cha fedha kilitolewa na kulifanya kazi gani?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mhe. Dr. Zainab Amir Gama, Mbunge wa Kibaha Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Masharti ya Kazi ya Mbunge katika kifungu Na. 13 kinaeleza kuwa, nanukuu: "Mbunge wa Jimbo atapewa Ofisi na vifaa vya Ofisi na Serikali. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa itahakikisha upatikanaji wa Ofisi na vifaa muhimu vinavyohitajika". Aidha, ni kweli kuwa Ofisi yangu imekuwa ikitoa majibu hapa Bungeni kuwa Ofisi ya Bunge itawezeshwa ili iweze kuwapatia Wabunge Ofisi zinazofanana na majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, ama kwa Masharti ya Kazi ya Mbunge au kauli ya Ofisi yangu kuhusu Ofisi ya Bunge kuwezeshwa, bado linabaki kuwa ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba Wabunge wanapatiwa Ofisi zinazofanana na majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, suala la Ofisi za Wabunge ni miongoni mwa agenda za Serikali kwa muda mrefu na sasa Serikali imekwishafanya uamuzi wa dhati wa kutekeleza azma yake ya kuwatengea Wabunge Ofisi zinazostahili. Ili kutekeleza azma hiyo katika mwaka wa fedha 2007/2008 Serikali imetenga shilingi bilioni (1) kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Wabunge na Makadirio ya awali yatakuwa ni Ofisi arobaini (40). Pamoja na fedha za ujenzi wa Ofisi, Mikoa imetenga shilingi milioni 398,641,000/= kwa ajili ya uendeshaji wa Ofisi za Wabunge.

Mheshimiwa Spika, ili kuwapa nafasi Waheshimiwa Wabunge waweze kushiriki katika mipango ya ujenzi wa Ofisi hizo, Serikali imeona pia ni vema fedha hizo zipelekwe katika Halmashauri. Zoezi la kuainisha Ofisi hizo arobaini za awali linaendelea kukamilishwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika kipengele (a) ni jukumu la Serikali kuhakikisha kuwa Ofisi za Wabunge na vifaa vya Ofisi vinapatikana. Kwa sasa jukumu hilo limekabidhiwa kwa Wakuu wa Mikoa. Kutokana na msingi huo, kwa mwaka 2006/2007 Mikoa ilitenga jumla ya shilingi 166,299,500 kwenye Bajeti za matumizi mengineyo kwa ajili ya ukarabati wa Ofisi za Wabunge, ununuzi wa samani, malipo ya gharama za maji, umeme, ulinzi na simu kwa wale waliofungiwa simu za mezani katika Mikoa mbalimbali.

(c) Mheshimiwa Spika, Mbunge wa Jimbo la Kibaha Mjini amepatiwa Ofisi katika jengo la Mkuu wa Wilaya ya Kibaha. Kwa mwaka 2006/2007 Mkoa wote wa Pwani pamoja na Mikoa mingine ya Kagera, Kilimanjaro, Morogoro, Mtwara, Ruvuma na Singida haikutenga fedha yoyote kwa ajili ya ukarabati na ununuzi wa vifaa vya Ofisi ya

Wabunge. Sababu kubwa ilikuwa ni ufinyu wa Bajeti. Hata hivyo, kwa kutumia fedha za Mfuko wa Kuboresha Utendaji Kazi (*Performance Improvement Fund (PIF)* ambao unaratibiwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani imewezeshwa kununua samani za Ofisi yake ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Mbunge wa Jimbo, Kibaha Mjini. Vifaa vitakavyofungwa katika Ofisi ya Mbunge ni pamoja na:-

- *Executive table* 1
- *Executive chair* 1
- *Visitors chairs* 4
- *Conference table* 1
- Zulia na mapazia

Thamani ya vifaa hivyo ni shilingi milioni 1,356,916/= na wanatarajiwa kuvifungwa katika Ofisi hiyo kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2007. *(Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Waziri, naishukuru Serikali baada ya swali langu sasa ofisi yangu naona watu wanazungukazunguka, lakini nilipewa majibu mabaya na *RAS* wake. Baada ya kusema hivyo nina swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa kuna mihimili mitatu Bunge, Serikali na Mahakama. Kila mhimili utapata uchungu kushughulikia masuala yake. Je, haoni sasa ni wakati muafaka badala ya kugombana na akina RAS, hela hawana wanatujibu vibaya na wao wamechoka tunagombana nao kwa nini hela hizi siziende Ofisi ya Bunge? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Lakini nimshukuru Mama Gama kwa ku-*appreciate* kwamba maelezo yale yamemridhisha.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ipo mihimili mitatu kwa maana ya Bunge, *Judiciary* pamoja na Utawala yaani *(The Executive).* Mihimili hii mitatu ndiyo itakayounda kitu kinaitwa Serikali. Ndiyo maana katika majibu yetu tumesema pengine ni vizuri tukakubaliana kwamba Serikali ndiyo imepewa jukumu hili. Hoja wala si kwamba fedha ziende Ofisi ya Spika au ziende kwa nani kubwa ni kwamba Serikali kwa ujumla wake tunao wajibu wa kufanya jambo hili ambalo ni la muhimu sana.

Sasa Serikali baada ya kutafakari kwa kina na kwa kweli jambo hili limezungumzwa sana ikaonekana basi angalau kwa kuanzia wacha tuanze na kupeleka fedha hizi moja kwa moja kwenye Halmashauri zetu, Halmashauri hizi ambazo Wabunge mna kauli kubwa na kwa hiyo mnaweza mkashiriki kikamilifu katika kujaribu kutengeneza hizi ofisi katika kiwango ambacho mnaridhika. Sasa Ofisi ya Spika

ingekuwa na uwezo au mtandao wa kutosheleza kuweza kufika huko pengine Serikali ingeweza ikafikiria jambo hilo kwa nia nzuri tu kwamba tunachotaka ni ofisi na wala si suala la malumbano kati ya mihimili hiyo mitatu.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wamesema fedha watazipeleka Halmashauri na kwa kuwa Halmashauri si suala la Muungano. Je, Wabunge wa Zanzibar fedha zao zitapelekwa kwenye nini? Wakati utaratibu wa kihasibu Serikali ya Zanzibar haiku *accountable* kwa *Auditor General* wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, jambo hilo tuliliona na tunafanya mazungumzo na Ofisi ya Waziri Kiongozi ili kuweza kuona ni utaratibu gani kwa upande wa Zanzibar utakaoweza kusaidia kutatua tatizo hilo moja kwa moja.

Na. 22

**Maendeleo ya Mfuko wa TASAF**

**MHE. JACOB D. SHIBILITI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mfuko wa Jamii wa Taifa *(TASAF)* umeleta Maendeleo makubwa hapa nchini na hasa kwa zile Wilaya za kwanza kupewa miradi na mfuko huo:-

(a) Je, hadi sasa Wilaya ya Misungwi imepewa kiasi gani cha fedha?

(b) Je, ni vijiji vingapi vimepata fedha kutokana na mfuko huo awamu hii na aina gani ya miradi waliyoibua;(c)Je, miradi hiyo iko katika hali gani?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* ulianza rasmi 9 Novemba, 2000 kwa Wilaya 40 za Tanzania Bara na Unguja na Pemba kule Zanzibar na sasa mradi huu umeenea Wilaya zote za Tanzania Bara na Zanzibar. Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza imetengewa kiasi cha Dola za Kimarekani 802,052.00 sawa na Tshs. 962,462,400.00 (kwa wastani wa fedha ya kubadilisha Dola ya Tshs. 1,200.00) zitakazotumika kutekeleza miradi itakayoibuliwa na jamii kwa kipindi cha mradi kinachoishia Desemba 2009. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2006 hadi Aprili, 2007 Wilaya ya Misungwi iliidhinishiwa kiasi cha Tshs. 362,496,413.22 kwa utekelezaji wa miradi 11 na imeishapewa kiasi cha Tshs. 175,907,349.11 kwa awamu ya kwanza. Fedha hizo hutumwa moja kwa moja kwa jamii na hutolewa kwa awamu mbili yaani baada ya

kutumia asilimia 70 ya pesa ya awamu ya kwanza na kutoa mrejesho wa matumizi ndipo awamu nyingine hutolewa.

(b) Mheshimiwa Spika, mpaka sasa vijiji ambavyo vimepata fedha katika mradi wa *TASAF* ni kumi na moja ambavyo vimepata jumla ya shilingi 362,496,413. Fedha hizo zilikuwa kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa zahanati, vyumba vya madarasa, soko, barabara na ufugaji wa ng'ombe.

(c) Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Miradi ya Jamii inayochangiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii, yaani *(TASAF)* hutegemea sana mwamko na juhudi za jamii husika, kwani wao ndio wasimamizi wakuu wa utekelezaji. Viongozi katika ngazi ya kijiji ndio wanaosimamia uchangishaji wa asilimia 20% au asilimia 5% inayolazimu jamii kuchangia. Michango hii inaweza ikiwa nguvu kazi, vifaa, kwa mfano kokoto, mchanga, mawe, matofali ya kuchoma na kadhalika au fedha taslimu. Hali ya miradi iliyotajwa hapo juu ni kama ifuatavyo:-

· Mradi wa ujenzi wa wadi wa Wagonjwa – Busongo na Miradi ya madarasa mawili ya Bugomba, Gambajingi na Misungwi ipo katika hatua ya kuwekwa jamvi la msingi.

· Miradi ya ujenzi wa Zahanati za Mwamazengo na Mwambuko ipo katika ujenzi wa jamvi la msingi.

· Miradi ya ujenzi wa barabara kilomita 6 Igongwa – Matale kazi iliyofanyika hadi kufikia mwezi wa nne ni kusafisha kilomita 3, na barabara ya kilomita 5 Mwisubi – Buguba imesafishwa kilomita 3 kazi ilisimama kutokana na mvua zilizokuwa zikinyesha.

· Miradi ya ujenzi wa madarasa 2 Shule za Sekondari Masawe na Mabuki na Mradi wa ufugaji wa ng'ombe kazi bado haijaanza kutokana na jamii kutotekeleza wajibu wao wa uchangiaji kwa maana ya ukusanyaji wa mchanga na kokoto/mawe kama mchango wao. Kama ilivyoelezwa awali utekelezaji wa Miradi hii hutegemea sana wananchi, Viongozi wa Wilaya, Kata na Vijiji katika kuihamasisha jamii. Hivyo basi wito unatolewa kwa Waheshimiwa Wabunge na Madiwani kusaidia ufuatiliaji na uhamasishaji ili miradi katika sehemu zetu ikamilike kwa muda uliopangwa na kwa ubora unaotakiwa. Hii itasaidia kupunguza gharama inayoweza kujitokeza muda ukiwa mrefu unaweza kutokea kutokana na kupanda kwa bei na hata jamii kuvunjika moyo kwa kushughulikia kitu kimoja kwa muda mrefu.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri pia pamoja na utendaji mzuri wa viongozi wote wa *TASAF* niulize swali moja tu.

Kwa kuwa wananchi wamekuwa wakiibua miradi yao mbalimbali ikiwemo afya, elimu, maji na barabara. Lakini miradi ya elimu inapata fedha kwa urahisi zaidi kuliko miradi mingine kama alivyonijibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwa vijiji vya Mwamboko

na Mwamazengo ambavyo viliomba zahanati fedha zilichelewa sana. Hali kadhalika na Mwasubi waliomba barabara fedha zilichelewa. Je, ni tatizo gani hasa linalofanya sekta hizo nyingine zicheleweshe fedha zake?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, lakini kabla ya kutoa majibu kwanza kwa niaba ya Serikali naomba nipokee pongezi zake kwa Serikali na viongozi wa Mashirika kama *TASAF*. Lakini la pili, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Shibiliti kwa juhudi za kufuatilia na amefika ofisini kwangu mara kadhaa kufuatilia maslahi ya wananchi wa Misungwi. Sababu kubwa inayofanya miradi mingine iwahi kabla ya nyingine kwanza inatokana na jinsi wananchi katika vijiji vinavyohusika wanavyochangamkia hiyo miradi. Katika vijiji vingine kuna malumbano makubwa baina ya vijiji vyenyewe na viongozi wao, hivyo vinacheleweshwa, lakini katika vijiji vingine wanawahi.

La pili ni utaratibu kwamba hii miradi inavizinduliwa vijijini inategemea inapelekwa kwenye sekta ipi. Kwa hiyo kama ni mradi wa elimu utapelekwa pale katika Halmashauri katika Idara ya Elimu. Kama ni Mradi wa Barabara utapelekwa katika Idara ya Ujenzi na inategemea hizo Idara zina kazi kiasi gani pengine unaweza kukawepo na ucheleweshο kidogo katika mtindo wa namna hiyo, lakini kwa kawaida miradi yote hii inatarajiwa iende sambamba na ichukue karibu wiki tatu na majibu yao kupatikana.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Nashukuru sana. Mimi nina swali dogo moja la nyongeza. Kwa kuwa programu hii ya *TASAF* ambayo ni mikopo kutoka Benki ya Dunia inatarajiwa kuisha mwaka 2009 na kwa kuwa kwa mujibu wa maelezo ya Wabunge na Waziri imeonyesha mafanikio makubwa na kwa kuwa vile vile zimetumika raslimali nyingi sana katika kuwajengea uwezo viongozi kuanzia ngazi ya Taifa hadi ya vijiji. Je, Serikali imejiandaaje kimkakati baada ya mwaka 2009?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu kwanza nipokee pongezi zake kwa kazi nzuri inayofanya kazi na *TASAF* na Serikali ya awamu ya nne ya Chama cha Mapinduzi. Serikali kama ilivyofanya katika *TASAF I* ilitathmini na ikajenga hoja ikaendelea na *TASAF II* na Serikali itafanya hivyo hivyo katika *TASAF II* itatathmini na kuona kama iko haja ya kuendelea na *TASAF III*. (*Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa *TASAF* imepokelewa vizuri sana na wananchi wetu vijijini. Na kwa kuwa wananchi wanategemea sana kupata fedha za miradi kupitia *TASAF* na kwa kuwa wananchi sasa hivi wameibua miradi mingi sana na iko Makao Makuu ya *TASAF* lakini inayorudi ni michache. Sasa Serikali itasaidia ili miradi ile iwe inarudi mapema ili wananchi waendelee kujiletea maendeleo yao kwa njia ya haraka?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Msindai, kama ambavyo nilivyomshukuru Mheshimiwa Halima Mdee kukubaliana kwamba kazi hii inatekelezwa

vizuri sana na matokeo ya kazi hiyo imeongeza sasa *demand* ya kutaka msaada zaidi katika kuhudumia jamii ya Watanzania ili kutekeleza ile azma ya Chama cha Mapinduzi na maisha bora kwa kila Mtanzania. (*Makofi)*

Serikali kwa sasa inaendelea kutathmini kama nilivyojibu hapo awali jinsi utaratibu huu wa *TASAF II* unavyoendelea na tutasaidiana na Halmashauri kujaribu kuangalia wapi panakwamisha hii miradi. Tukumbuke kwamba miradi hii maidhinisho kamili yanafanyika katika ngazi ya Wilaya kinachofanyika kule *TASAF* ni kuangalia tu kwamba zile taratibu zote zimefuatwa. Kwa hiyo, pengine ni vizuri tukashirikiana na Waheshimiwa Wabunge kuangalia katika Halmashauri yetu kama zile taratibu zinakwenda kwa haraka inavyotakiwa. Lakini kwa upande wake Serikali inatimiza wajibu kuona kwamba fedha hizi zinafika haraka.

Na. 23

**Huduma za Mawasiliano ya Simu za CELTEL**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Kampuni ya Simu ya *CELTEL* imejitahidi kujenga minara miwili katika Jimbo la Bumbuli katika Vijiji vya Bumbuli (Kata ya Bumbuli) na Mahezangulu (Kata ya Tamota) imekamilika na imeanza kutumika tangu mwezi Machi, 2007:-

(a) Je, ni lini wananchi wa Tarafa ya Mgwashi wapatao 188 wenye simu za mkononi na wengine 93 ambao wamejiorodhesha kutaka kununua simu za mkononi watafikiwa na mtandao wa *CELTEL?*

(b) Je, Serikali haioni kwamba, Tarafa hiyo itakuwa na biashara kubwa ya simu za mkononi kwa wakazi 50,000?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Hezekia Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya Kampuni ya *CELTEL* kujenga minara katika jimbo la Bumbuli na Mahezangulu ambayo imekwishaanza kutumika, Kampuni hiyo katika kuhakikisha kwamba inadumisha shughuli zake katika maeneo mbalimbali nchini, ina mpango wa kufikisha huduma zake katika Tarafa ya Mgwashi ifikapo mwezi Juni, 2008 ili wananchi wa Tarafa hiyo waweze kufaidika na huduma za *CELTEL.*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda Wizara hiyo ipokee shukrani nyingi za wananchi wa Jimbo la Bumbuli kwa kazi

nzuri iliyofanyika kwa upande wa Wizara pamoja na Kampuni ya *CELTEL* ambayo iko makini sana katika kuhudumia wananchi. Kwa kuwa Tarafa ya Mgwashwi itashughulikiwa nadhani kabla ya mwisho wa mwaka unaokuja wa fedha nitaomba wanaofanya hiyo kazi waangalie kusahihisha matatizo madogo madogo katika Kata za Tamota, Ponde na Mamba ikizingatiwa kwamba eneo la Lushoto lina mabonde bonde sana. Kwa hiyo, unatakiwa umakini katika kufunga vyombo vya masafa. Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Naona hakuna swali ila ni shukrani tu.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Mgwashi inapakana na Tarafa ya Mlola. Tarafa ya Mlola yenye Kata 4 haina mawasiliano kabisa ya simu. Tarafa hii ina utajiri mkubwa sana wa zao la maharage na mazao mengine ina Sekondari 7, Shule za msingi 30, kituo cha afya, zahanati 5 na kituo cha Polisi lakini hakuna mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri alifahamishe Bunge hili na wananchi wa Mlola. Je, Tarafa hii itapatiwa lini mitandao ya simu? Ahsante Mheshimiwa Spika.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mshangama kwamba Mlola inapatikana na Mgwashi na katika maeneo yake mawasiliano ya simu hayajafika.

Lakini napenda nimhakikishie kwamba kampuni ya *Vodacom* inayo mpango mwaka huu kufikia sehemu ya Mkuzi, Lukozi, Malindi, Mlalo, Soni na Bumbuli; na katika maeneo hayo ambapo *Vodacom* watafika na *Zantel* nao watafika kwa sababu wao wanafanya kazi kwa pamoja na kutegemeana.

Mheshimiwa Spika, lakini si hivyo tu Kampuni ya *TTCL* inayo mpango wa kwenda maeneo ya Rwai, Ubiri, *Gale Mission*, Mnazi, Vuga Rwangi na tunategemea maeneo ya Mheshimiwa Mbunge yatafikiwa nimwombe Mheshimiwa Mbunge avute subira. Lakini naomba nichukue nafasi hii kwa Niaba ya Waheshimiwa Wabunge nizishukuru Kampuni za simu zote kwa juhudi kubwa wanazofanya kufikisha huduma za simu vijijini.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kazi ya uwekaji Mtandao wa simu za mkononi unaofanywa na *Celtel* Bumbuli kwa sasa unafanana na ujenzi huo Jimbo la Namtumbo. Nazipongeza kampuni hizo za simu zinazofanya kazi hiyo Namtumbo. Lakini kwa kuwa ujenzi huo unafanyika katika eneo moja tu la Barabara Kuu.

Je, Serikali inaweza kutumia busara yake kuwaomba kampuni hizo za simu waongeze huduma hizo katika Tarafa ya Sasawala yenye Kata ya Lusewa, Magazini, Ligela na Kata ya Kitanda?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba mawasiliano yamefika Namtumbo kwenye Barabara Kuu na tutawaomba Kampuni ya simu waone kama kuna uwezekano wa kufika huko baada ya wao kujiridhisha na utafiti watakaoufanya wa soko na hali ya kibiashara.

Na. 24

**Uanzishwaji wa Chuo cha Ufundi-Kishapu**

**MHE. FRED MPENDAZOE TUNGU** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ya Awamu ya Nne inatilia mkazo suala la kuanzisha Vyuo vya Ufundi kwa kila Wilaya na inazingatia pia suala la kuwa na Shule za Sekondari katika kila Kata na kwa kuwa, Kampuni ya Almasi ya Mwadui iko tayari kuyatoa baadhi ya majengo yake kwa Serikali ili yatumike baadhi ya majengo yake kwa Serikali ili yatumike kuanzisha Chuo au Sekondari:-

Je, Serikali imefikia hatua gani ya kuyachukua majengo hayo ili yaweze kutumika kwa ajili ya kuanzisha Chuo cha Ufundi, *VETA* – Wilaya ya Kishapu, na majengo mengine yaweze kutumika kuanzisha Shule ya Sekondari Kidato cha Kwanza hadi cha Sita, hasa ikizingatiwa kuwa, Wilaya ya Kishapu ina upungufu wa Shule za Sekondari na haina Chuo cha Ufundi ambacho ni muhimu sana kwa sasa.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fred Mpendazoe Tungu, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuipongeza Kampuni ya Almasi ya Mwadui kwa kuwa tayari kuyatoa baadhi ya majengo yake kwa Serikali ili yatumike kuanzisha Chuo cha Ufundi Stadi au Sekondari.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa ya ukaguzi wa majengo na miundombinu uliofanyika tarehe 10 Mei, 2007, Wilaya ya Kishapu inashauriwa kutafuta eneo jingine kwa ajili ya kuanzisha Chuo cha *VETA* cha Wilaya, ili iweze kupatiwa chuo chini ya Mpango wa Serikali unaoandaliwa wa uanzishwaji wa Vyuo vya Ufundi vya Wilaya. Aidha, kuanzisha Shule ya Sekondari Kidato cha 1- 4 inawezekana baada ya kufanya ukarabati mkubwa wa majengo kama ilivyo ahidiwa na Mmiliki wa sasa. Hata hivyo inabidi Uongozi wa Wilaya ushughulikie suala la umiliki wa shule na kuweka utaratibu unaofaa kwa wanafunzi waliokuwepo toka awali, waliopo sasa na watumishi. Kuhusu

uanzishwaji wa Kidato cha 5 – 6 Wilaya inashauriwa kutafuta eneo lingine lenye nafasi ya kutosha kujenga madarasa, mabweni, maabara na nyumba za walimu.

Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa iliyokuwa Shule ya Sekondari ya Mchepuo wa Biashara (*Shycom*) sasa inakuwa Chuo cha Ualimu wa Masomo ya Biashara na kitaanza kuchukua walimu wa Stashahada kuanzia mwaka huu wa fedha 2007/2008.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nilitaka kujua Serikali ina mpango gani wa jumla wa kimkakati wa kuboresha hizi shule za sekondari za Kata ambazo sasa zipo hasa kwa kuzingatia kwamba shule hizi zimejengwa katika muundo au mtindo wa kidharura hazina huduma nyingi hasa mabweni na Mkakati gani pia wa kuandaa kuwepo kwa shule zenye *A level* kwenye maeneo mbalimbali nchini?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Mheshimiwa Maige ningependa kusema kama ifuatavyo: Kwanza kuhusu jinsi ya kuimarisha shule za Sekondari zilizojengwa katika Kata. Kwa niaba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi naomba kuwapongeza viongozi na wananchi wote waliojenga shule mpya hadi kufikia tarehe hii ni shule 1084 tunashukuru sana. *(Makofi)*

Katika vipaumbele vya Bajeti ya Wizara katika mwaka huu fedha 2007/2008 ni maeneo matatu ambayo yatatiliwa sana mkazo. La kwanza ni ujenzi wa nyumba za Walimu ili waweze kukaa huko ambako shule za Kata zimejengwa ambako hakuna nyumba za Walimu. Sasa ukishapata Walimu ndiyo njia mojawapo ya kuimarisha elimu katika maeneo hayo. Ya pili ni upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Kwa hiyo, hiyo ni njia ya pili ya kuimarisha shule hiyo na ya tatu ni kupata *servicing training* au mafunzo kazini ya Walimu ambao wamepata mafunzo mafupi ili waweze kufundisha vizuri zaidi. Naamini kabisa hizo njia tatu tukizikamilisha vizuri shule zitaimarishwa.

Kuhusu ujenzi wa *hostel* mimi ningependa kuchukua nafasi hii kuwaomba bado uongozi na wananchi kushirikiana kujenga *hostel* kwa sababu mnajua uwezo wa Serikali yetu si rahisi kwa mwaka huu kujenga *hostel* kwa kutumia fedha za Serikali kwa asilimia 100. Kwa hiyo, bado tunaomba msaada wa wananchi na viongozi tuweze kujenga *hostel* na kuziimarisha ili watu wetu wakae. Mengine yatafuata kadri uwezo wa fedha utakavyopatikana. (*Makofi*)

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri. Lakini tarehe 10/8/2006 niliuliza swali hapa likihusiana na majengo yaliyokuwa yanatumiwa na *COJIFA*, yaliyoko katika Wilaya ya Bukombe, Kijiji cha Buntubili ili yakabidhiwe Wilaya ya Bukombe tuyatumie kwa kujenga Chuo cha Ufundi *VETA.* Na kwa kuwa wakati wa kuuliza swali hilo Waziri wa

Miundombinu alisimama akatoa rai kwamba inawezekana kabisa akakabidhiwa kuliko kuendelea kuchakaa.

Na kwa kuwa Serikali Wilaya ya Bukombe iliandika barua kwenda *TANROAD* Mkoani na *TANROAD* Mkoa wakaandika kwenda *TANROAD* Makao Makuu na *TANROAD* Makao Mkuu toka mwaka jana wakaandika barua kwenda kwa Katibu Mkuu wa Miundombinu lakini mpaka leo hakuna jibu lolote linaloendelea, hatujalipata na majengo haya yako wazi. Je, Serikali inaweza kuniambia kuna umbali kiasi gani wa kutoa majibu ya kukubali kwamba tuyaendeleze kama Chuo cha Ufundi au kukataa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli majengo ambayo yanaachwa na taasisi mbalimbali wananchi wengi hupenda yaimarishwe ili yaweze kutumika kwa ajili ya shughuli kama za vyuo au shule za sekondari au shule za Msingi. Lakini kwa vyuo vya ufundi vinahitaji majengo maalum ambayo yamejengwa kwa misingi mizuri ili yasiweze kuleta matatizo wakati yakitumika. Sasa majengo ambayo Mheshimiwa Mbunge anasema yaliachwa na *COJIFA*, ambayo alikuwa anataka yatumike kama Chuo cha Ufundi kimsingi hayafai kwasababu yanahitaji msingi imara ili zile mashine za ufundi zitakazowekwa pale zitakapoanza kutumika jengo lisije likapasuka halafu likaleta madhara. Ndiyo maana *TANROAD* waliamua wao waweze kuyatumia wao kwa shughuli mbalimbali za ujenzi wa taifa katika eneo hilo.

Hivyo bado tunasisitiza wananchi pamoja na Mheshimiwa Mbunge waendelee kuwasiliana na watu wa *TANROAD* na Wizara ya Miundombinu waone ni jinsi gani watakavyoweza kuyatumia majengo yale vizuri. Lakini kwa chuo cha ufundi tungependa wananchi watenge eneo la kutosha ambalo Wizara yangu pamoja na *VETA* watakwenda kukagua ili waweze kuona ni jinsi gani wanaweza kujenga chuo ambacho kitakuwa imara kwa manufaa ya wananchi katika Wilaya hiyo.

Na. 25

**Kutoweka kwa Baadhi ya Wanyama – Tanzania**

**MHE. AME PANDU AME** aliuliza:-

Kwa kuwa Zanzibar ni sehemu ya Tanzania na kwa kuwa hivi sasa Visiwani humo wanyama kama vile Paa-Nunga, Swala, Pundamilia na Mbuni wametoweka:-

Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kupeleka wanyama hao wasiohatarisha maisha ya watu visiwani humo ili nako waweze kuonekana?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi kujibu swali la Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mbunge wa Nungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Naomba nilifahamishe Bunge lako tukufu kwamba swala, Pundamilia na Mbuni si wanyama wa asili wa Zanzibar wanyama hawa walipelekwa Zanzibar katika miaka ya 1980 kwa ajili ya maonyesho. Baada ya maonyesho kumalizika, waliwekwa kwenye Zoo katika msitu wa Dole Masingini.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na usimamizi hafifu na kukosekana kwa utaalamu wanyama hao walikuwa wanavunja zizi mara kwa mara na kukimbilia katika mashamba ya watu, kuharibu mazao na hivyo kuuawa.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa haina mpango wa kuwapeleka wanyamapori hao kwenye mazingira ya asili huko Tanzania Visiwani kwa kuwa kabla ya kufanya hivyo utafiti wa kina unahitajika kuhusu bionuai za Zanzibar ili kuainisha masuala muhimu ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa chakula, maji, makazi, maficho, kinga ya maadui na mahusiano ya wanyama hao na jamii ya watu waliokaribu na maeneo yaliyofikiriwa kuwa makazi ya wanyama hao.

Mheshimiwa Spika, katika orodha ya wanyama waliotajwa na Mheshimiwa Mbunge, mnyama mwenye asili ya Zanzibar ni Paa-Nunga *(Cephalophus aders)*. Mnyama huyu hajatoweka ila yuko hatarini kutoweka kutokana na shughuli za binadamu za kilimo cha kuhamahama, ukataji miti usio endelevu na uwindaji haramu.

Kwa sasa mnyama huyu anapatikana katika Hifadhi ya Taifa ya Jozani, Msitu wa Hifadhi wa Kiwengwa- Pongwe na Misitu ya Mtende na Muyuni. Hivi leo idadi ya wanyama hawa inakadiriwa kuwa 600. Juhudi za kuwahifadhi zinaendelezwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya uhifadhi kwa wananchi na kupiga marufuku uwindaji wa wanyama hao.

Mheshimiwa Spika, mnyama anayesaidikiwa kutoweka katika Misitu ya Zanzibar ni chui wa Zanzibar *(Panthera Pardus adders).* Hakuna taarifa za aina nyingine za wanyama au ndege wanaosaidikiwa kutoweka.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa mazingira wanaoishi Paa-nunga yanalingana na swala anaonaje Waziri akaleta swala japo 1000 wakaletwa Zanzibar? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nilieleza kwamba utafiti unahitajika ili kubaini kama kuna chakula cha kutosha, kuna maficho, maji na hakutakuwa na athari kati ya wanyama watakaopelekwa huko na wenyeji wanaokaa karibu na eneo litakalopangwa kwa ajili ya wanyama hao. Kwa sasa Serikali haina mpango mpaka utafiti huo uwe umekamilika kupeleka wanyama hao huko Zanzibar. *(Makofi)*

Na. 26

**Mapato ya Uwindaji kwa Halmashauri za Wilaya**

**MHE. FELIX N. KIJIKO** aliuliza:-

Kwa kuwa muda mrefu Halmashauri za Wilaya za Mkoa wa Kigoma zimekuwa zikipata asilimia 25 (25%) ya mapato yatokanayo na uwindaji wa wanyamapori na kwa kuwa, kiasi hicho kimekuwa kikishuka mwaka hadi mwaka bila Serikali kueleza sababu za msingi za kushuka kwa kipato hicho ambacho kimekuwa kikiwasaidia ki-maendeleo wananchi walio katika vijiji vinavyopakana na hifadhi hizo:-

(a) Je, Serikali inawaeleza nini wananchi hao kuhusu hali hiyo?

(b) Je, kwa nini Serikali inakubali kupokea mchango huo wa asilimia 25 bila kujua kiasi cha asilimia inayochukuliwa?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mbunge wa Muhambwe, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Serikali huzipatia Halmashauri zinazozunguka maeneo ya uwindaji asilimia 25 ya mapato yatokanayo na uwindaji wanyamapori kutoka katika vitalu vilivyoko katika Wilaya zao. Katika kila kipindi cha mwaka wa fedha, Wizara yangu huandaa Bajeti ya mwaka husika ikiwa ni pamoja na makisio ya mapato yatokanayo na uwindaji wa wanyamapori katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Aidha, mapato yote yatokanayo na uwindaji wa wanyamapori huwasilishwa Hazina kwa mujibu wa kanuni za fedha zilizopo. Hatimaye, Hazina huipatia Wizara asilimia 25 ya mapato ya uwindaji wa wanyamapori iliyokusanya na kuzigawa kwa Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felix Kijiko lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kuwa Halmashauri za Wilaya za Mkoa wa Kigoma tangu mwaka wa fedha 2002/2003 hadi 2006/2007 zimekuwa zikipata asilimia 25 inayopungua mwaka hadi mwaka kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali ambalo Mheshimiwa Kijiko atapatiwa.

Mheshimiwa Spika, kupungua huku kumetokana na kushuka kwa idadi ya watalii na wanyama waliowindwa mwaka hadi mwaka. Kushuka huku kumetokana na matatizo mbalimbali mbalimbali ikiwa ni pamoja na matatizo ya wakimbizi. Asilimia 25 iliyotolewa na Hazina ilizingatia upungufu huo na kushuka kwa mapato ya uwindaji na watalii kupungua mwaka hadi mwaka hali ambayo ilisababisha kupungua kwa asilimia 25 ya mapato kwa Halmashauri zote husika.

Aidha mapato kutokana na uwindaji yataongezeka kutokana na katika mwaka wa fedha 2007/2008 hivyo mapato ya Halmashauri hizo yanategemewa kuongezeka sawia.

(b) Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba Serikali huwa inakubali kupokea mchango wa asilimia 25 bila kujua kiasi cha asilimia inayochukuliwa. Fedha zinazokusanywa katika kila kitalu cha uwindaji zinatokana na ada ya kitalu, bei ya kila aina ya mnyama, idadi ya wanyama waliowindwa tozo ya siku ya wawindaji walizokaa porini au siku za safari, tozo za wawidaji bingwa, nyara za Serikali na kadharika. Baada ya kukusanywa fedha hizo na kuwasilishwa Hazina, asilimia 25 yake hupelekwa katika Wilaya husika kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ameyatoa nia ya swali hili ni kusaidia Wizara hiyo. Katika pori lililoko Mkoa wa Kigoma na hasa pori la Mweovozi ambalo lina *plots* nyingi za Wawindaji taarifa zenye uhakika na limefanyiwa kazi ni kwamba wameweka viwanja vya ndege ambavyo vimetayarishwa na ndege zinakwenda kule na kuchukua nyara zilizopo bila taarifa yoyote ama bila Wizara kudhibiti.

Sasa Mheshimiwa Waziri anaweza akahakikisha kwamba kuna udhibiti gani ambao Wizara yake imefanya ama inafanya ama kuwa na takwimu sahihi kwamba kuna nyara kiasi gani zinachukuliwa ambazo nadhani ndiyo changamoto inasababisha kipato kishuke kuja mpaka kupata asilimia 25 ambayo Wizara haijui? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, biashara ya uwindaji inafanyika katika maeneo ambayo yako mbali sana na miji na makazi ya watu na kila kitalu cha uwindaji kinatakiwa kifanye maendeleo ya eneo lake ili kuruhusu uwindaji wa kitalii. Maendeleo hayo ni pamoja na kujenga barabara, kujenga maeneo ambayo ndege ndogo zinaweza kutua ili kuleta watalii hao ambao ni watu matajiri sana wanakuja kwa ajili ya *sports hunting*.

Aidha watalii hao wanapokwenda katika kitalu chochote wanafuatana na Afisa Maliasili aliyepangwa mahususi kuangalia kwamba mwindaji anawinda wanyama wale tu ambao wameorodheshwa katika maombi yake na anaruhusiwa kuwinda na yeye baada uwindaji huo analeta ripoti ya wanyama waliowindwa na nyara ambazo zimechukuliwa.

Hivyo hakuna nafasi kwamba Serikali haijui ni nyara kiasi gani au ndege gani ambazo zimeingia na kutoka katika maeneo mbalimbali ya uwindaji nchini. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa wananchi hao wanasumbuliwa sana na wanyama hao na hasa wanyama siku hizi huwa wakali, wanaua watu pamoja na kuharibu mashamba. Je, Serikali haiwezi ikaongeza asilimia hii kutoka asilimia 25 mpaka asilimia 40 ili wananchi wafaidike kutokana na uharibifu huo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 Serikali imeangalia upya gharama na malipo yanayofanywa katika Sekta ya uwindaji na malipo hayo yamerekebishwa na hivyo tunategemea kwamba kila

Wilaya ambayo ina vitalu vya uwindaji zitapata fedha zaidi kutokana na marekebisho hayo.

Na. 27

**Uchimbaji wa Madini ya Vito**

**MHE. DORA H. MUSHI** aliuliza:-

Je, Kampuni za Uchimbaji Madini ya Vito zinaishirikisha vipi Serikali ili kuhakikisha kwamba, asilimia inayotolewa na kampuni hizo za uwekezaji ni sahihi kulingana na uzalishaji wenyewe?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dora Heriel Mushi, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uhakiki na usahihi wa madini yanayozalishwa na wawekezaji hapa nchini hufanyika katika hatua mbili. Hatua ya kwanza hufanyika wakati wa uzalishaji na hatua ya pili hufanyika kabla ya kusafirisha madini kwenda kuyauza nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, uhakiki wakati wa uzalishaji hufanyika kwa kufanya kaguzi mbalimbali migodini ambazo hujumuisha kaguzi za taratibu za uchimbaji na uchenjuaji na pia uhakiki wa takwimu za uzalishaji. Kaguzi hizi hufuatia taarifa za robo mwaka zinazotolewa na makampuni hayo kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Madini.

Mheshimiwa Spika, uhakiki wa pili ambao hufanyika kabla ya kwenda kuuza madini yaliyozalishwa hufanyika katika hatua ya mwisho kabla ya kusafirishwa kwenda nje ya nchi. Katika hatua hii wataalam wa Wizara yangu kwa kushirikiana na *TRA* hufanya ukaguzi ili kujua thamani ya madini yanayotegemewa kusafirishwa. Baada ya kujua thamani ya madini hayo mwekezaji hutakiwa kulipa mrahaba wa asilimia 5 kwa madini ya vito, iwapo madini hayo ya vito yatakuwa hayajasanifiwa na asilimia sifuri kwa madini ya vito ambayo yamesanifiwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, taratibu mbili zilizotajwa hapo ju ni kwa madini yote yanayozalishwa yakiwemo madini ya vito. Hata hivyo, kwa kutambua thamani na unyeti wa madini ya vito, Serikali imeweka sharti la wawekezaji wa Kigeni kuwa na ubia na Watanzania kwenye kampuni zao zinazowekeza kwenye madini ya vito.

Sharti hilo ni la Watanzania kuwa na angalau asilimia 25 ya hisa za kampuni za kigeni. Sharti hili huwapa nafasi Watanzania kushiriki moja kwa moja katika kuwekeza kwenye rasilimali ya madini na kujiongezea kipato na kupunguza umaskini.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa asilimia 30 za madini ya *Tanzanite* yameweza kuonekana kwenye soko la dunia na hayo madini yanapelekwa na wawekezaji wakubwa na kwa kuwa tunajua kabisa kwamba wao ndiyo wana uwezo mkubwa wa kutoa madini kwa wingi wao ndio wana vyombo vya kisasa vya kuchimba madini na kuyatoa kwa uwezo mkubwa.

Je, hii asilimia 70 ya madini ya *Tanzanite* yanayoonekana kwenye soko kwenye soko la dunia yanatoka wapi na wakati tunajua kabisa kwamba wachimbaji wadogo wadogo kwa muda mrefu miaka minne sasa imepita bila uzalishaji wa *Tanzanite?*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kumpongeza kwa kufanya utafiti na kuwa na takwimu lakini swali lililoulizwa linahusu takwimu ambazo kwa hakika zinahitaji kuthibitisha na kumbukumbu zetu zilizoko katika Ofisi zetu.

Kwa hiyo, kimsingi pamoja na kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kufanya utafiti lakini namwomba atembelee Ofisini kwetu ili tuweze kwanza kujiridhisha kwa takwimu tulizonazo kwanza kama ni sahihi.

Lakini hili la pili kwamba wachimbaji wadogo kwa takribani miaka minne hawajaweza kuzalisha kwa heshima kubwa naomba nitofautiane naye kwamba si kweli. Kumbukumbu zetu zinaonyesha kwamba kuna uzalishaji unaofanywa na wachimbaji wadogo japokuwa pengine uzalishaji wake si kwa kiwango cha wachimbaji wakubwa.

Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge nimkaribishe kwamba tu-*reconcile* hili la takwimu lakini pia tutampa ufafanuzi wa kina kuhusu takwimu za madini yanayokwenda nje.

Na. 28

**Mahitaji ya Umeme Bukoba Vijijini**

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU** aliuliza:-

Kwa kuwa, umeme ni nyenzo muhimu katika kuleta maendeleo; na kwa kuwa, wakazi wa Mkoa wa Kagera wanapata umeme kutoka Uganda; na wale wa Bukoba Vijijini na Misenyi waliahidiwa kupatiwa umeme kutoka Uganda na wakakubali migomba na mazao mengine yang'olewe ili kupitisha nyaya za umeme mkuu (*HT*) kutoka Uganda:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa, inachangia katika kuchelewesha maendeleo katika Kata hizo na inavunja moyo wananchi hao ambao tangu mwaka 1996 umeme umepita Katani Vijijini/ mashambani mwao bila wao kupatiwa umeme huo?

(b) Je, ni lini Serikali itatoa umeme katika sehemu hizo yaani Kata ya Katoma Vijiji vya Lukindo, Kyambeo, Kagera, Ivogero, Kata ya Bugorora, katika vijiji vya Kabigo, Bugorora, Buchurago na Kata ya Nsungu katika vijiji vya Ngando, Ilogero?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bernadeta Kasabago Mushahu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Serikali inafahamu umuhimu wa umeme kuwa ni chachu ya maendeleo. Kutokana na ukweli huo Serikali imefanya jitihada kuhakikisha wananchi walioko katika njia ya umeme utokao Uganda wanapatiwa umeme. Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la Misaada la *SIDA* imeonyesha nia ya kufadhili utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme katika vijiji vya Mkoa wa Kagera. Upembuzi yakinifu ulishafanyika na *Project Document* kwa ajili ya kuombea fedha imewasilishwa kwa wafadhili *(SIDA).*

Mradi huu ni mkubwa utakaogharimu jumla ya dola za Kimarekani milioni 10.4 mradi utahusisha baadhi ya Vijiji vya Wilaya za Bukoba Vijijini na Misenyi, Vijiji vya Wilaya ya Karagwe na Vijiji vya Wilaya ya Muleba. Hivyo, kama mradi huu utapata ufadhili, baadhi ya maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge yatapatiwa umeme. Maeneo mengine ambayo hayatafikiwa, Serikali itaendelea kutafuta pesa kupitia utaratibu wa *Rural Energy Agency (REA).*

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wakazi wa Kata hizi ambako umeme mkuu umekuwa ukipita, wamekuwa wakisubiri kupatiwa umeme kwa zaidi ya miaka 10, lakini hawajapata. Na kwa kuwa upembuzi yakinifu sasa umekamilika, *Project Document* imeishawasilishwa kule kunakohusika. Je, ninaweza nikaelezwa ni lini hasa Mradi huu utaanza? Pili, Je, Katika Bajeti hii ijayo, Serikali itakuwa imetenga kiasi Fulani kutoka kwenye makusanyo ya ndani kwenye *Rural Electrification Agency* ambao ni Mradi wa kupeleka Umeme Vijijini kwenye Mradi huu kusudi wakazi wa Bukoba Vijijini, Misenyi, Muleba na Karagwe waweze kupatiwa huduma ya umeme?

**SPIKA:** Waheshimiwa mtaona kuwa muda wa maswali umeisha. Lakini nafidia matangazo yangu marefu sana ya Miswada. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri atoe majibu na tutaona muda utakaokuwa umebaki.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha kusema, kwa miradi niliyoitaja, *Project Document* tumeishapeleka kwa Mfadhili na tumeishawasilisha. Kwa hiyo, tunachosubiria sasa hivi kwa kweli ni majibu ya lini fedha zitatoka. Na kama nilivyokwisha kusema kwenye jibu la msingi, mara fedha zitakapotoka, tutaanza kutekeleza Mradi huo kwa maeneo ambayo nimeyataja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kama tumetenga fedha kwenye Bajeti ya mwaka huu, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni nia ya Serikali kuhakikisha kwamba miradi yote ambayo imeainishwa na uchambuzi yakinifu umeishafanyika, kwa jitihada za Serikali pamoja na wafadhili tutatekeleza kwa kadri ambavyo Serikali itakuwa inapata fedha. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira, tuko pamoja. Lakini pia nimpongeze sana kwa jinsi ambavyo amekuwa akiwasiliana na sisi kufuatilia utekelezaji wa miradi hii. *(Makofi)*

Na. 29

**Ujenzi wa Vyanzo vya Maji Arumeru**

**MHE. ELISA D. MOLLEL** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Arumeru walitoa maji ya Mto Nduruma kwa wakazi wa Jiji la Arusha kwa ahadi ya Serikali kuwa watapewa shilingi 100,000,000 kwa ajili ya kuwasaidia kujenga vyanzo vya maji pamoja na miundombinu ya kusambaza maji katika kata sita; na kwa kuwa, ahadi hiyo ilikuwa ya mwaka 2003/2004 lakini bado haijatekelezwa.

Je, Serikali inatoa majibu gani kwa wananchi wa Arumeru kuhusu ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Elisa Mollel, Mbunge wa Arumeru Magharibi, ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mwaka 2003/2004 Serikali ilitoa ahadi ya shilingi milioni 100 kwa ajili ya kusaidia miradi ya maji kwenye baadhi ya vijiji katika Wilaya ya Arumeru. Vijiji hivyo vipo katika Kata za Nkwaurua, Moshono Mlangarini, Nduruma, Kikwe na Mbuguni. Katika kutekeleza ahadi yake Serikali ilitoa kiasi cha shilingi milioni 20 katika mwaka wa fedha 2005/2006.

Fedha hizo zilitumika katika ujenzi wa chanzo cha maji *intake structure* kwa ajili ya kijiji cha Kipande, Nkwavele katika Kata ya Nkwaurua, kujenga sehemu ya uzio kwenye chanzo cha maji cha mradi wa maji ya bomba wa Baraa- Mashono unaohudumia Kata za Moshono na Baraa kununua na kufunga mabomba ya plastiki yenye urefu wa kilomita 1.05 katika kijiji cha Nduruma kilichopo Kata ya Nduruma na ujenzi wa tanki lenye meta za ujazo 45 katika eneo la Sangota kwa ajili ya kijiji cha Oldadai katika Kata ya Sokoni II.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006, Serikali iliandaa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Katika Maandalizi ya utekelezaji wa programu hiyo, Wizara ilitekeleza

kila Halmashauri iwasilishe orodha ya miradi midogo midogo ambayo inaweza kutekelezwa na kuondoa kero za wananchi katika muda usiozidi miezi sita. Katika orodha hiyo Wizara yangu ilishauri Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru kuvipa kipaumbele vijiji ambavyo nimevitaja hapo juu.

Mheshimiwa Spika, Miradi iliyopendekezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru ni katika vijiji vya Nkwaurua Kata ya Mashono, Mlangarini Kata ya Mlangarini, Nduruma Kata ya Nduruma, Kikwe Kata ya Kikwe, Mbuguni Kata ya Mbuguni, King'ori Kata ya King'ori Ngyani Kata ya Nkoaranga, Sura Kata ya Songoro na vijiji vya Ekinywa na Ilkiushin katika Kata ya Olturmet. Fedha za utekelezaji wa miradi ya maji katika vijiji hivi zitatumwa Wilayani mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2007/2008 na hivyo kutekeleza ahadi ya Serikali.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge swali moja lililobaki litapangiwa siku nyingine kwa kuwa muda sasa umetosha. Matangazo nitaanza na wageni: Wageni walioko kwenye *gallery* ambao nimepewa taarifa mapema ni Viongozi Wakuu wa Muungano wa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu Tanzania *(TAHLISO)* ambao nitawataja na nikiwataja itabidi wasimame ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuwaona. Kwanza ni Ndugu Paul Magesa – Mwenyekiti wa Kikao cha Marais wa Vyuo Vikuu, Ndugu Komba Noel – Katibu Mkuu wa *TAHLISO*, Ndugu Bruno Ngingo – Mwenyekiti wa Muungano wa Serikali za Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu, Ndugu Paul Selelii Chobo – Rais wa Serikali ya Wanafunzi wa *CBE*, Dar es salaam, Ndugu Renatus Mathius – Kamishina wa *TAHLISO*, Bi. Salama Abdallah Juma – Kamishina wa *TAHLISO*, Zanzibar na Ndugu Walter Ngonyani – Rais wa *IMTU*. Karibuni sana. Natumaini mazungumzo yenu na Serikali yataleta ufumbuzi katika matatizo yaliyoko katika Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Balozi Seif Idd, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ameniomba niwatambulishe wageni wake ambao ni Wenyeviti wa Wadi zilizomo ndani ya Jimbo la Kitope, Unguja Zanzibar. Wenyeviti wote wa Wadi kutoka Jimbo la Kitope, Zanzibar, Tafadhalini! Karibuni sana sana. Pia Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini B, Unguja. Karibuni sana Waheshimiwa!

Mikutano ya Kamati: Mheshimiwa Anna Abdallah, Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, ameniomba nitangaze kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati leo mara baada ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji katika Ukumbi Na. 231.

Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati za Huduma za Jamii, ameniomba nitangaze kuwa kutakuwa na Mkutano wa Kamati hiyo kesho, siyo leo, kesho tarehe 15 Juni, 2007 saa 5.00 asubuhi, Ukumbi Na. 428 Ghorofa ya 4 Jengo la Utawala.

Tangazo kuhusu shughuli za Tarehe 16 Mei, 2007. Naomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, atalihutubia Taifa siku ya Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa

Afrika. Maadhimisho hayo yatafanyika Kitaifa hapa Dodoma katika Uwanja wa Jamhuri na shughuli zenyewe zinaanza saa 3.00 asubuhi.

Jumamosi Tarehe 16 Juni, 2007, hapa Dodoma, Mheshimiwa Rais akishiriki kama Mgeni Rasmi wa Siku ya Mtoto wa Afrika. Waheshimiwa Wabunge wote tunaombwa tuweze kujumuika katika siku hii muhimu ya Watoto wetu. Wabunge wote mnaalikwa.

Sasa, nizungumzie kidogo kuhusu pipi. Kumetokea tatizo kidogo. Leo pipi ziliwekwa pale kwenye sebule kabla ya kuingia hapa na zikaisha. Haikuwezekana kuwa na za ziada. Lakini, kiutawala pia tulikuwa tumepata tabu kidogo, wenzetu upande wa Mpambe *(Seargent At Arms)* walituambia isingefaa kuleta vibakuli vya udongo Ulaya ndani ya Bunge, kwa sababu ikitokea katika mjadala mtu amepandwa jazba, asije akakitupa na kikamzuru Mbunge mwenzie.

Kwa hiyo, tumeagiza sasa kutoka kwa Kikundi cha Wajasiriamali wadogo vibakuli vidogo vya utamaduni, vitakuwa vimetengenezwa kwa aina fulani ya kiutamaduni. Sijui tuite nyasi au kama kikapu vile kitasukwa vizuri. Hivyo ndivyo vitakavyotumika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ndio kuna Mjasiriamali amepata tenda ya Bunge kuweza kuwa na vikapu hivyo. Kwa hiyo tunatumaini kuanzia Jumatatu pipi zitakuwepo za kutosha na zitakuwa hapa ndani. Kama nilivyosema zinasaidia sana katika kuwaweka Wabunge katika hali ya kutokutafakari sana. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2006 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2007/2008

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likae kama Kamati ili liweze kupokea na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2006 na Mwelekeo katika Muda wa Kati Kwa kipindi cha mwaka 2007/2008 – 2009/2010. Pamoja na hotuba hii, nawasilisha Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2006 na Kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha salama katika kipindi kingine cha kutoa Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa letu inayotokana na utekelezaji wa sera na uongozi mzuri wa Serikali ya Awamu ya Nne inayoongozwa na Rais wetu Mpendwa, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Hatuna shaka kuwa mafanikio yaliyopatikana yataendelea kukipatia Chama cha Mapinduzi ushindi ili kiendeleze mazuri yote yaliyoanzishwa kwa lengo la kukuza uchumi na kuondoa umaskini nchini mwetu.

Taarifa hii ni matokeo ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi ikiongozwa na Mwenyekiti. wake Mhe. Dr. Abdallah O. Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa kujadili na kutupa ushauri pamoja na changamoto zilizochangia katika kuboresha na kufanikisha kukamilisha taarifa hii. *(Mkaofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia nichukue nafasi hii kuwashukuru Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mhe. Gaudence C. Kayombo (MB), Katibu Mkuu, Balozi Charles K. Mutalemwa, Naibu Katibu Mkuu, Bibi Joyce K.G. Mapunjo, Wakurugenzi, viongozi wa asasi na wafanyakazi wote wa Wizara yangu, ambao wamefanya kazi kwa bidii na ufanisi mkubwa katika kufanikisha ukamilishaji wa taarifa hii.

Napenda pia kuwashukuru viongozi na wafanyakazi wenzetu wa wizara, idara mbalimbali za Serikali, Mashirika ya umma na asasi kwa ushirikiano wao mkubwa wakati wa kuandaa taarifa hii. *(Mkaofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka mmoja aliyekuwa Mbunge mwenzetu Hayati Juma Jamaldin Akukweti, ambaye pia alikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Bunge, aliiaga dunia kutokana na ajali ya ndege wakati akitekeleza majukumu ya kitaifa. Hivyo, kwa masikitiko makubwa naomba kutoa salamu za pole kwa ndugu, jamaa na familia ya marehemu. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa Mapitio na Malengo ya jumla ya Uchumi wetu, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Burian (MB), aliyekuwa Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Bunge, Mheshimiwa Bernard K. Membe (MB), aliyekuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo (MB), kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa William Ngeleja, kuteuliwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, na Mheshimiwa, Mtutura Abdallah Mtutura kwa kushinda uchaguzi mdogo na kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Tunduru kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Mapitio ya Mwenendo wa Uchumi Jumla Katika Kipindi cha Mwaka 2006/2007. Shabaha na Malengo ya Uchumi ya jumla katika mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, shabaha kuu za kisera katika mwaka 2006/2007 zilikuwa kama ifuatavyo:-

§ Kuendelea kutengemaza uchumi jumla;

§ Kuendelea kutekeleza MKUKUTA;

- § Kuimarisha na kusaidia sekta isiyo rasmi ili ipanuke na kutengemaa kwa lengo la kuingizwa kwenye mfumo rasmi wa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ili kuzifikia shabaha hizo kuu, malengo ya uchumi jumla yaliyowekwa katika kipindi cha mwaka 2006/2007-2008/2009 yalikuwa kama ifuatavyo:-

- § Pato halisi la Taifa kukua kwa asilimia 5.9 mwaka 2006, asilimia 7.3 mwaka 2007, asilimia 7.7 mwaka 2008, na asilimia 7.9 mwaka 2009;

- § Kiwango cha kasi ya upandaji bei kisichozidi asilimia 4.0 kufikiwa ifikapo mwezi Juni 2007;

- § Mapato ya ndani kuongezeka kufikia asilimia 14.5 ya Pato la Taifa mwaka 2006/2007, asilimia 14.7 mwaka 2007/2008 na kuongezeka hadi asilimia 14.8 mwaka 2008/2009;

- § Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana *(M2)* kudhibitiwa kwa viwango vinavyowiana na malengo ya ukuaji wa uchumi na kasi ya upandaji bei; na

- § Akiba ya fedha za kigeni itakayokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi saba. Mwenendo wa Uchumi Jumla katika mwaka 2006/2007

Mheshimiwa Spika, Kuhusu mwenendo wa uchumi jumla - Pato la Taifa: Katika mwaka 2006, Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 6.2 ikilinganishwa na Makadirio ya awali ya asilimia 5.9 kwa kipindi hicho, na ukuaji wa asilimia 6.7 mwaka 2005.

Kushuka kwa kiwango cha ukuaji wa Pato la Taifa (ikilinganishwa na mwaka 2005) kulisababishwa na ukame uliotokea katika maeneo mengi nchini katika msimu wa mvua wa mwaka 2005/2006, ukosefu wa umeme na kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia. Sekta zilizoathirika zaidi na hali hiyo ni kilimo, bidhaa za viwandani, umeme na maji.

Viwango vya ukuaji viliongezeka kwa sekta za uuzaji wa jumla, rejareja na mahoteli na utalii; uchukuzi na mawasiliano, madini na fedha, bima na huduma za kibiashara. Aidha, kiwango cha ukuaji kwa sekta ya uendeshaji Serikali na huduma nyingine hakikubadilika na kubakia katika kiwango cha mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupungua kwa kiwango cha ukuaji, sekta ya kilimo iliendelea kutoa mchango mkubwa katika Pato la Taifa, ikilinganishwa na sekta zingine, ambapo mwaka 2006 mchango wa sekta hiyo ulikuwa asilimia 44.7. Mchango wa sekta nyingine, hususan bidhaa za viwandani; uuzaji wa jumla, rejareja na mahoteli na utalii, madini na ujenzi uliendelea kuongezeka, ikiashiria kubadilika kwa mfumo wa uchumi unaoelekea kwenye nchi isiyotegemea kilimo pekee kwa maendeleo yake.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kukua kwa Pato la taifa kutoka sh. 13,063,317 milioni hadi sh. 14,995,247 milioni, Pato la Wastani la Mtanzania liliongezeka hadi sh. 399,873 ikilinganishwa na sh. 360,865 mwaka 2005, sawa na ongezeko la asilimia 10.8 kwa bei za mwaka husika.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Kasi ya Upandaji Mfumuko wa Bei: Wastani wa kasi ya upandaji mfumuko wa bei katika mwaka 2006 ulikuwa asilimia 7.3, ikilinganishwa na asilimia 5.0 mwaka 2005. Kuongezeka kwa kasi ya upandaji mfumuko wa bei mwaka 2006 kulitokana na kupanda kwa bei za bidhaa, hususan chakula na mafuta ya petroli ambayo pia yalichangia kuongezeka kwa gharama za usafirishaji na uzalishaji umeme unaotumia mafuta.

Hadi Aprili 2007, kasi ya upandaji mfumuko wa bei ilikuwa asilimia 6.1, baada ya kushuka kutoka asilimia 7.2 mwezi wa Machi. Kiwango hicho kinatarajiwa kuendelea kushuka, kutokana na ongezeko la upatikanaji wa chakula baada ya kipindi cha mavuno kuanza sehemu nyingi za nchi.

Mheshimiwa Spika, Ukuzaji rasilimali: Katika mwaka 2006, ukuzaji rasilimali uliongezeka na kufikia sh. 878,649 milioni mwaka 2006, kutoka sh. 735,180 milioni mwaka 2005, kwa bei za mwaka 1992, sawa na ongezeko la asilimia 19.5. Uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa ulikuwa asilimia 37.0 kwa bei za mwaka 1992 ikilinganishwa na asilimia 32.9 mwaka 2005. Ukuzaji rasilimali kwa bei za miaka husika uliongezeka kutoka sh. 3,149,402 milioni mwaka 2005 hadi sh. 3,802,413 milioni mwaka 2006 sawa na ongezeko la asilimia 20.7.

Kuongezeka kwa ukuzaji rasilimali kulitokana hasa na ongezeko katika ujenzi wa majengo, uagizaji wa vifaa na kuongezeka kwa shughuli nyinginezo za ukuzaji rasilimali zikiwemo uendelezaji ardhi, barabara na madaraja.

Mheshimiwa Spika, ukuzaji rasilimali katika sekta binafsi uliongezeka na kufikia sh. 2,582,664 milioni kutoka sh. 2,050,093 milioni mwaka 2005, kwa bei za miaka husika, sawa na ongezeko la asilimia 26.0. Mchango wa sekta binafsi katika ukuzaji rasilimali ulikuwa asilimia 67.9 ikilinganishwa na asilimia 65.1 mwaka 2005.

Kwa upande wa sekta ya umma ukuzaji rasilimali uliongezeka na kufikia sh. 1,183,832 milioni, mwaka 2006 kutoka sh. 1,068,172 milioni mwaka 2005 kwa bei za miaka husika, sawa na ongezeko la asilimia 10.8.

Mheshimiwa Spika, Mchango wa sekta ya umma katika ukuzaji rasilimali ulikuwa asilimia 31.1 ikilinganishwa na asilimia 33.9 mwaka 2005. Kupungua kwa mchango wa sekta ya umma katika ukuzaji rasilimali kunatokana na mchango wa mashirika ya umma kupungua katika ukuzaji mitaji, pamoja na kuendelea kuongezeka kwa mchango wa sekta binafsi katika uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, Ujazi wa Fedha na Karadha: Katika mwaka ulioishia Desemba 2006, ujazi wa fedha kwa tafsri *pana* ($M_2$) ulikua kwa asilimia 13.5 ikilinganishwa na asilimia 36.9, kipindi kama hicho mwaka 2005. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi ($M_3$) uliongezeka kwa asilimia 22.2 Desemba 2006 ikilinganishwa na asilimia 38.2 Desemba 2005.

Kushuka kwa viwango vya $M_2$ na $M_3$ mwaka 2006 ikilinganishwa na mwaka 2005 kulitokana na ongezeko la mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya uagizaji wa bidhaa za kukuzia mitaji *(capital goods)* na zile za kati *(intermediate goods)* pamoja uuzaji wa hawala za Serikali kupitia Benki Kuu ili kudhibiti kasi ya upandaji bei. Viwango vya $M_2$ na $M_3$ katika mwaka 2006/2007 viliendana na malengo yaliyowekwa ya asilimia 23.4 na asilimia 24.2 kwa $M_2$ na $M_3$ kwa mtiririko huo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/06, benki za biashara ziliendelea kutoa mikopo kwa sekta binafsi. Mikopo iliyotolewa na benki za biashara katika mwaka 2005/06 ilikuwa sh. 1,656,837.8, sawa na ongezeko la asilia 35.9 ikilinganishwa na sh. 1,219,305.6 zilizotolewa mwaka 2004/05. Hadi Desemba 2006 mikopo kwa sekta binafsi ilifikia sh. 2,027,196.3 ikilinganishwa na sh. 1,425,062.3 Desemba 2005, sawa na ongezeko la asilimia 42.3. Sekta zilizopata viwango vikubwa vya mikopo ni ujenzi na majengo, uzalishaji, kilimo, usafirishaji, madini, viwanda na biashara nyingine.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/06, wastani wa riba zilizotolewa na benki za biashara kwa amana za akiba ulishuka kutoka asilimia 2.61 Juni, 2005 hadi asilimia 2.54 Juni, 2006, na ilipofika Desemba 2006, wastani wa riba hizo uliongezeka na kufikia asilimia 2.59. Aidha, wastani wa riba iliyotozwa na benki za kibiashara kwa mikopo ulishuka kutoka asilimia 15.51 Juni, 2005 hadi asilimia 15.44 Juni 2006 na kuongezeka hadi asilimia 16.43 Desemba, 2006. Ingawa ushindani baina ya benki za biashara umeongezeka, mwenendo wa riba katika benki hizo unaonyesha kuwa bado kuna tofauti kubwa kati ya riba za amana na za mikopo.

Tofauti hiyo ilikuwa asilimia 9.6 Juni, 2006 ikilinganishwa na asilimia 10.7 Juni, 2005, na kufikia asilimia 10.3 ilipofika Desemba 2006. Aidha, tofauti hiyo ya riba kuendelea kuwa kubwa kiasi hicho, ni kiashiria kuwa bado gharama ya kukopa katika benki za biashara ni kubwa. Serikali, kwa kupitia Awamu ya Pili ya Maboresho na Mageuzi katika Sekta ya Fedha, inashughulikia tatizo hilo ili kupunguza totauti hiyo, hivyo kuwawezesha wananchi wengi zaidi waweze kukopa kwa gharama nafuu zaidi kwa ajili ya kujiendeleza na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, Mapato na Matumizi ya Serikali, katika nusu ya kwanza ya mwaka 2006/07, mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 1,311.7, sawa na asilimia 8.0 juu ya makisio ya shilingi bilioni 1,211.5 kwa kipindi hicho. Kati ya mapato hayo, shilingi bilioni 1,201.7 zilitokana na kodi ambapo mapato yasiyo ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 110.0. Kuongezeka kwa mapato kulitokana hasa na kuimarika kwa usimamizi na ukusanyaji wa kodi, hususan, kodi ya mapato, kodi ya ongezeko la thamani kwa bidhaa za ndani na nje, na ushuru wa forodha. Katika robo ya tatu ya

mwaka 2006/07, mapato ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 2,002.4, sawa na asilimia 9.7 juu ya makisio ya shilingi bilioni 1,824.7 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, katika nusu ya kwanza ya mwaka 2006/07, matumizi yalifikia shilingi bilioni 2,104.5, sawa na asilimia 81.0 ya matumizi yaliyopangwa kwa kipindi hicho. Kati ya matumizi hayo, sh. 1,342.3 bilioni zilitumika kwa matumizi ya kawaida na sh.761.1 bilioni kwa miradi ya maendeleo. Hadi Machi 2007, matumizi ya Serikali yalifikia sh. 3,394.3 bilioni, sawa na asilimia 94.5 ya matumizi yaliyopangwa kwa kipindi hicho. Katika hotuba itakayotolewa mchana wa leo, Waziri wa Fedha, atabainisha kwa kina, mwenendo wa mapato na matumizi ya Serikali katika mwaka 2006/07 na makadirio kwa mwaka 2007/08.

Mheshimiwa Spika, deni la Taifa, lilipungua kutoka dola za Marekani 9,383.9 milioni Desemba, 2005, hadi dola za Marekani 7,188.4 milioni Desemba, 2006, sawa na punguzo la asilimia 23.3. Kati ya deni hilo, dola za Marekani 5,749.0 milioni ni deni la nje, sawa na asilimia 80.0 ya deni lote, na dola za Marekani 1,439.4 milioni ni deni la ndani. Deni la nje lilipungua kwa asilimia 29.3, kutoka dola za Marekani 8,153.7 milioni mwaka 2005.

Kupungua kwa deni la Taifa kulitokana na msamaha wa madeni uliotolewa na mashirika ya fedha ya kimataifa, nchi wanachama wa *Paris Club*, na baadhi ya nchi zisizokuwa wanachama wa *Paris Club*, pamoja na juhudi za Serikali katika kulipa madeni ya ndani. Baada ya misamaha hii, nchi yetu imejinasua na mzigo mkubwa wa deni la nje kwa kiasi ambacho viwango vya upimaji wa uhimili wa madeni *(debt sustainability indicators)* vimeshuka kufikia viwango vinavyokubalika (*thresholds*) kwa nchi maskini za *HIPC*, ikiwamo Tanzania. Ili kuhakikisha kuwa nchi yetu haitumbukii tena katika lindi la madeni ya nje yasiyohimilika, Serikali inaendelea kuzingatia mwongozo wa Mkakati wa Kudhibiti Madeni ya Nje kwa kukopa mikopo nafuu *(concessional loans)* tu na stahimilivu, ili kujenga uwezo wa uchumi na kuongeza uwekezaji, ajira, mauzo nje, mapato ya Serikali, miundombinu na kuendeleza rasilimali watu, hususan katika fani za sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, Biashara ya Nje, thamani ya mauzo nje (ikijumuisha bidhaa na huduma), iliongezeka kutoka dola za Marekani 2,945.5 milioni mwaka 2005 na kufikia dola za Marekani 3,135.6 milioni mwaka 2006, sawa na ongezeko la asilimia 6.4. Ongezeko hilo lilichangiwa hasa na mapato ya huduma (ikijumuisha mapato ya utalii na ya matumizi ya bandari) yaliyoongezeka kwa asilimia 15.4. Thamani ya mauzo ya bidhaa iliongezeka kwa asilimia 2.75, kufikia dola za Marekani 1,723.0 milioni, ikilinganishwa na dola za Marekani 1,675.8 milioni zilizopatikana mwaka 2005. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na mauzo ya bidhaa zisizo asilia, hususan dhahabu na bidhaa za viwanda.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuongezeka kwa bei katika soko la dunia kwa bidhaa nyingi za asilia mwaka 2006, thamani ya mauzo nje ya bidhaa hizo ilipungua kwa asilimia 24.6, kutoka dola za Marekani 354.4 milioni mwaka 2005 hadi dola za Marekani 267.1 milioni mwaka 2006. Kupungua huko kulitokana hasa na kupungua kwa kiasi cha

bidhaa zilizouzwa nje. Thamani ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia iliongezeka na kufikia dola za Marekani 1,419.5 milioni mwaka 2006 kutoka dola za Marekani 1,321.0 milioni mwaka 2005, sawa na ongezeko la asilimia 7.4. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na mauzo ya dhahabu na bidhaa za viwandani. Changamoto iliyopo ni kuongeza mauzo nje na kuhamasisha uzalishaji kwa viwango vinavyokidhi matakwa ya soko la dunia. Bidhaa zilizouzwa nje zinaonyeshwa katika Jedwali Na. 2 na katika Kielelezo Na. 1 kwenye vitabu vyenu.

Mheshimiwa Spika, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje (f.o.b[2]) mwaka 2006 iliongezeka kwa asilimia 28.9 kufikia dola za Marekani 3,864.1 milioni, ikilinganishwa na bidhaa za thamani ya dola za Marekani 2,997.6 milioni mwaka 2005. Ongezeko hili lilichangiwa kwa kiasi kikubwa na kupanda kwa bei za mafuta ya petroli, ongezeko la thamani ya uagizaji wa mashine na mitambo, malighafi ya bidhaa za viwandani na bidhaa za matumizi ya kawaida.

Aidha, kwa takwimu hizi, thamani ya bidhaa zilizouzwa nje zilikuwa na uwezo wa kugharamia asilimia 44.6 tu ya uagizaji nje. Hivyo, Serikali itaongeza msukumo katika kutekeleza Mkakati wa Kuongeza Mauzo ya Bidhaa Nje *(Export Development Strategy)* ili kuongeza wingi na ubora wa bidhaa tunazouza nje, kuongeza thamani *(value addition)* ya bidhaa zetu kwa kuzisindika, kuwekeza katika uzalishaji wa bidhaa mpya za kuuza nje, kutumia kikamilifu fursa mbalimbali tunazopata za kuuza nje, kama vile mpango wa *AGOA*[3], *EBA*[4] na fursa nyingine zinazotolewa Canada, Japan, China na Korea, ikiwa ni pamoja na kutafuta masoko mapya kwa bidhaa zetu. Tanzania imeanza kufanya vizuri katika biashara ya huduma, hususan biashara ya utalii ambayo imeliingizia Taifa mapato makubwa ya fedha za kigeni. Mwaka 2006, Mapato yaliyotokana na biashara ya huduma yaliongezeka na kufikia dola za Marekani 1,412.6 milioni kutoka dola za Marekani 1,269.2 milioni mwaka 2005, sawa na ongezeko la asilimia 11.3. Ongezeko hilo lilichangiwa na mapato ya utalii, usafirishaji wa mizigo na huduma nyingine. Mapato yatokanayo na utalii yaliongezeka kwa asilimia 4.7 kufikia dola za Marekani 862.0 milioni, na kuchangia asilimia 61.0 ya mapato ya huduma, ikilinganishwa na dola za Marekani 823.0 milioni zilizopatikana mwaka 2005.

Ongezeko hili la mapato ya utalii, lilitokana na juhudi zilizofanywa na Serikali na wadau wengine za kutangaza vivutio mbalimbali vya utalii vilivyoko nchini pamoja na kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta ya utalii, ukijumuisha mahoteli, usafirishaji watalii na uwindaji wa kitalii. Aidha, malipo ya huduma yaliongezeka kwa asilimia 3.3 hadi dola za Marekani 1,247.3 milioni, ikilinganishwa na dola za Marekani 1,207.3 milioni mwaka 2005. Kuongezeka kwa malipo ya huduma kulitokana na ongezeko la malipo ya huduma za usafirishaji mizigo, kusafiri nje, huduma za fedha, na huduma nyinginezo zikiwemo mawasiliano, bima, TEKNOHAMA[5] (ICT)[6], na huduma nyingine za kibiashara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio kiasi yaliyopatikana katika kuongeza mapato ya biashara ya huduma, ikijumuisha utalii, changamoto iliyopo ni kuboresha huduma zetu kwa kuongeza vivutio vya utalii na miundombinu kama bandari, barabara na reli, ili kuweza kutumia kwa kikamilifu fursa za kusafirisha mizigo kwenda na kutoka

katika nchi za jirani kama vile Rwanda, Burundi, Zambia, Malawi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006, nakisi ya urari wa malipo ya kawaida unaojumuisha urari wa biashara ya bidhaa, huduma, malipo mbalimbali, na uhamisho mali wa kawaida iliongezeka kufikia dola za Marekani 1,458.7 milioni, ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani 881.6 milioni mwaka 2005. Kupanuka huko kwa nakisi kulichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa nakisi katika urari wa biashara ya bidhaa, kulikotokana na ongezeko kubwa katika uagizaji wa bidhaa nje (ikilinganishwa na mauzo nje) na ongezeko la malipo nje kwa huduma zinazotolewa na mashirika/makampuni ya nje.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006, akiba ya fedha za kigeni iliongezeka kwa asilimia 6.4, kufikia dola za Marekani 2,260.1 milioni, ikilinganishwa na dola za Marekani 2,048.4 milioni mwaka 2005. Kiasi hicho cha akiba ya fedha za kigeni mwaka 2006, ni sawa na thamani ya uagizaji bidhaa na huduma toka nje kwa miezi 5.3, ikilinganishwa na miezi 5.8 mwaka 2005. Kiasi hiki kilikuwa chini ya lengo lilikusudiwa la uwezo wa kuagiza bidhaa na kulipia huduma kwa zaidi ya miezi 7. Upungufu huu wa akiba ya fedha za kigeni ulitokana na kuongezeka kwa matumizi ya fedha za kigeni katika uagizaji wa mafuta kwa ajili ya mitambo ya kuzalishia umeme, baada ya ukame kusababisha kina cha maji katika mabwawa ya kuzalishia umeme kupungua, pamoja na ongezeko katika uagizaji wa bidhaa za kukuza mitaji na chakula.

Mheshimiwa Spika, thamani ya shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na dola ya Marekani kwa mwaka 2006, ilikuwa na wastani wa sh. 1,251.9 kwa dola moja, ikilinganishwa na wastani wa shilingi 1,128.8 kwa dola moja mwaka 2005. Mwenendo huo ni sawa na kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania kwa asilimia 10.9. Aidha, thamani ya shilingi kwa dola moja ilikuwa sh.1,261.6 mwishoni mwa Desemba 2006 ikilinganishwa na sh. 1,165.5 mwishoni mwa Desemba 2005. Kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na dola ya Marekani kulitokana hasa na kutokuwepo kwa akiba ya fedha za kigeni za kutosha zitokanazo na mauzo nje, wakati kukiwa na mahitaji makubwa ya fedha za kigeni ili kugharamia uagizaji wa bidhaa toka nje, hususan mafuta kwa ajili ya kuzalishia umeme, kuagiza bidha za kukuza mitaji na chakula kukabili upungufu uliosababishwa na ukame.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Uchumi Duniani na Ushirikiano wa Kimataifa, pato la dunia lilikua kwa wastani wa asilimia 5.4 mwaka 2006, ikilinganishwa na asilimia 4.9 mwaka 2005. Ongezeko la pato la dunia lilichangiwa kwa kiasi kikubwa na ukuaji mkubwa wa pato katika nchi za Asia na Ulaya. Aidha, pato la nchi zinazoendelea lilikua kwa wastani wa asilimia 7.9 mwaka 2006, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 7.5 mwaka 2005. Ongezeko hilo la wastani wa ukuaji wa pato katika nchi zinazoendelea lilichangiwa kwa kiasi kikubwa na ukuaji mkubwa wa pato katika nchi za China na India, ambao ulikua kwa wastani wa zaidi ya asilimia 9.5. Juhudi zaidi zinahitajika kwa nchi yetu kufikia viwango vya wastani vilivyofikiwa na nchi nyingine zinazoendelea.

Mheshimiwa Spika, Mwenendo wa Biashara Duniani katika mwaka 2006, biashara ilikua kwa asilimia 8.0 ikilinganishwa na asilimia 6.5 mwaka 2005. Sehemu kubwa ya ongezeko hilo ilitokana na ukuaji wa mauzo ya nje na uagizaji wa bidhaa kutoka nje katika nchi za Ulaya. Katika nchi maskini zinazoendelea, mauzo ya nje yaliongezeka kwa asilimia 30.0 mwaka 2006, ikilinganishwa na asilimia 36.0 mwaka 2005. Sehemu kubwa ya thamani ya mauzo nje ilichangiwa na ongezeko kubwa la bei ya mafuta, bidhaa asilia pamoja na bidhaa za viwandani. Aidha, wastani wa bei za chuma ulipanda kwa kiwango kikubwa na hivyo nao kuchangia katika ukuaji wa mauzo nje kwa mataifa yaliyouza bidhaa hizo mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, Nchi ya China iliendelea kufanya vizuri kibiashara kwa kuwa na ongezeko la asilimia 27.0 ya mauzo ya bidhaa nje, ikilinganishwa na nchi nyingine kubwa kibiashara duniani kama Ujerumani (asilimia 15.0) na Marekani (asilimia 14.0). Bidhaa zilizochangia kuongezeka kwa viwango vya mauzo ya nje kwa kiasi kikubwa ni pamoja na vifaa vya ofisini, mawasiliano, nguo na chuma.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Uchumi wa Bara la Afrika katika mwaka 2006, pato la Bara la Afrika lilikua kwa asilimia 5.5, ikilinganishwa na asilimia 5.6 mwaka 2005. Kupungua kwa pato la Bara la Afrika kulitokana na migogoro ya kisiasa na hali mbaya ya hewa katika baadhi ya nchi barani Afrika. Sehemu kubwa ya pato katika Bara la Afrika ilitokana na kuimarika kwa uchumi, kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa za Afrika kwenda nchi nyingine duniani, pamoja na bei kubwa za mafuta, chuma na madini.

Mheshimiwa Spika, viwango vya ukuaji wa pato Barani Afrika vilikuwa tofauti katika nchi mbalimbali. Kwa nchi zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara wastani wa pato ulipungua kutoka asilimia 6.0 mwaka 2005 na kufikia asilimia 5.7 mwaka 2006. Katika nchi za Eneo la Maziwa Makuu wastani wa pato ulipungua kutoka asilimia 6.2 hadi kufikia asilimia 5.5.

Kupungua kwa wastani wa pato katika eneo hili kulitokana na hali ya hewa yaani ukame, ongezeko la bei ya mafuta, vita pamoja na hali mbaya ya kisiasa. Aidha, kwa nchi za Kusini mwa Afrika, wastani wa ongezeko la pato ulipungua kutoka asilimia 7 hadi asilimia 6.6. Kupungua kwa pato hilo kulitokana hasa na kushuka kwa kiwango cha ukuaji wa pato la nchi ya Angola, kilishuka kutoka asilimia 20.6 mwaka 2005 hadi kufikia asilimia 15.3 mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa, Ushirikiano wa kiuchumi kati ya nchi yetu na mataifa mengine duniani umeendelea kuimarika kwa kiwango kikubwa na hivyo kuendelea kulijengea Taifa letu mazingira mazuri ya shughuli za kiuchumi na kijamii. Naomba nitaje baadhi ya maeneo muhimu ambayo nchi yetu inashirikiana na mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*) katika Mkutano wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*) uliofanyika Novemba 2006 Arusha, Tanzania, Wakuu wa Nchi waliamua kuziruhusu nchi za Rwanda na Burundi kuwa wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuanzia Julai, 2007.

Mkutano huo pia uliidhinisha mapendekezo ya kuanzishwa kwa utafiti unaolenga kuifanya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa na utaratibu wa pamoja wa kodi kwa bidhaa zinazozalishwa kutoka nchi wanachama wa Soko la Pamoja la Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika (*COMESA*) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) ifikapo mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EADS*[7]) ulizinduliwa Novemba, 2006. Mkakati huu ndio utakaokuwa dira ya ushirikiano katika miradi na programu za Jumuiya hii kwa kipindi cha miaka mitano (2006-2010). Sheria ya Ushindani inayohusisha sekta za fedha, biashara na uwekezaji ilizinduliwa mwaka 2006. Vilevile maandalizi ya mkataba utakaosaidia nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuepuka utozaji ushuru mara mbili pamoja na ukwepaji kodi yaliendelea katika mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushirikiano katika masuala ya mawasiliano, maandalizi ya ujenzi wa barabara za Mombasa - Katuna na Dar es salaam – Mutukula yalikamilika, na ujenzi wa barabara hizi unatazamiwa kukamilika katika kipindi cha miaka miwili ijayo.

Mheshimiwa Spika, Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria *(Lake Victoria Basin Commission)* ilizinduliwa rasmi mwaka 2006 na shughuli kubwa ya Kamisheni hii ni kuainisha mipango ya maendeleo katika Ukanda wa Ziwa Victoria, ikiwa ni pamoja na usalama wa usafirishaji na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Kimataifa kuhusu Eneo la Maziwa Makuu (*ICGLR*[8]), katika mwaka 2006 Wakuu wa Nchi za Eneo la Maziwa Makuu walitia saini maafikiano ya pamoja ya Mpango wa Kuongeza Usalama na Kukuza Maendeleo katika Eneo la Maziwa Makuu pamoja na itifaki ya uanzishwaji wa Mfuko wa Fedha wa Maendeleo na Programu zinazolenga katika masuala ya amani na usalama, demokrasia, utawala bora na maendeleo ya kiuchumi, na kijamii. Vilevile, Seretarieti ya Eneo la Maziwa Makuu ilianzishwa, makao makuu yake yakiwa Bujumbura, Burundi, ikiongozwa na mwanadiplomasia mwanamke wa Kitanzania, Balozi Liberata Mulamula, akiwa Katibu Mkuu wake wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*), katika mkutano wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika uliofanyika Maseru, Lesotho, mwaka 2006, Wakuu hao wa Nchi waliamua kulifanya eneo hili kuwa eneo huru la biashara ifikapo mwaka 2008, na kuwa na ushuru wa forodha wa pamoja ifikapo mwaka 2010. Vilevile, ilikubaliwa kuundwa kwa kamati itakayohusisha Mawaziri wa Fedha, Uwekezaji, Maendeleo ya Uchumi, Biashara na Viwanda kushirikiana na Sekretarieti kuandaa mwongozo wa kuharakisha utekelezaji wa maamuzi na kuimarisha ushirikiano katika nchi wanachama. Aidha, Wakuu wa Nchi hizi za *SADC* pia walisaini itifaki ya masuala yanayohusu fedha na uwekezaji ili kuvutia zaidi wawekezaji katika kanda hii ya Afrika.

Mheshimiwa Spika, Mpango Mpya wa Ushirikiano kuleta Maendeleo ya Afrika *(NEPAD*[9]*)* mwezi wa Juni 2006, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisaini makubaliano *(Memorandum of Understanding (MoU)* na Jopo la Watu Mashuhuri *(Panel of Eminent Persons)* kuashiria Tanzania kuanza rasmi mchakato wa kutathminiwa na kujipima yenyewe *(African Peer Review Mechanism - APRM)* kwenye masuala ya utawala bora na uwajibikaji. Ili kuanza mchakato huo, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) iliunda Baraza la Kitaifa kuratibu zoezi la nchi kujitathmini na kujipima yenyewe ili kudumisha utawala bora chini ya Mpango wa *NEPAD*. Baraza hilo linajumuisha wadau mbalimbali nchini, hususan asasi za kidini, jumuiya za kiraia, Bunge, Vyuo Vikuu, vyama vya wafanyakazi, sekta binafsi, Serikali, vijana na walemavu.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Makubaliano wa Kuimarisha Ushirikiano kati ya *NEPAD* na Kamati ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Maamuzi kati ya China na Afrika ulisainiwa mwaka 2006, ambapo pamoja na mambo mengine, ilikubaliwa kuanzishwa na kuendeleza programu za muda mrefu katika sekta mbalimbali, kama vile rasilimali watu pamoja na utekelezaji wa miradi maalumu itakayokubaliwa kwa pamoja kati ya China na Afrika. Baadhi ya miradi ambayo imepitishwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) kwa ajili ya kufadhiliwa ni pamoja na utafiti wa nishati jadilifu *(renewable energy)* unaohusisha nchi za Uganda, Tanzania na Gambia.

Mheshimiwa Spika, uzinduzi wa Itifaki inayohusu Ujenzi wa Miundombinu ya Habari na Mawasiliano *(NEPAD ICT Broadband Protocol)* unaoshirikisha nchi 23 za Mashariki na Kusini mwa Afrika ulifanyika mwezi Agosti 2006 mjini Kigali, Rwanda na kusainiwa na nchi saba za awali, ambazo ni Lesotho, Madagascar, Malawi, Rwanda, Afrika Kusini, Tanzania na Uganda. Kusainiwa kwa itifaki kutaharakisha utekelezaji wa ujenzi wa mtandao wa mawasiliano *(East African Submarine Cable System - EASSy)* utakaokuwa na urefu wa kilomita 9,900, kwa lengo la kuongeza ubora na kupunguza gharama za mawasiliano kati ya nchi na nchi, badala ya kutegemea mawasiliano kwa njia ya *satellite*. Ujenzi wa mtandao huo utakapokamilika, unatazamiwa kugharimu dola za Marekani 300 milioni.

Mheshimiwa Spika, dhamira kubwa ya ushirikiano wa kiuchumi na kiufundi baina ya nchi zinazoendelea ni kutafuta ufumbuzi wa matatizo yanayozikabili, badala ya kutegemea nchi zilizoendelea. Katika juhudi za kuimarisha ushirikiano baina ya Nchi Zinazoendelea, mkutano wa kamati maalumu ya ushirikiano baina ya Afrika na mataifa yanayoibukia kiuchumi ya China, India na Brazili ulifanyika Ethiopia, Septemba, 2006. Katika mkutano huo, ilikubaliwa kuwa na mpango wa matumizi mazuri ya rasilimali ili kuchangia maendeleo ya viwanda Barani Afrika. Vilevile iliafikiwa, pamoja na mambo mengine, kuendeleza na kuimarisha juhudi zilizopo ili kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi, biashara, na upatikanaji wa masoko kwa bidhaa zinazozalishwa barani Afrika pamoja na uendelezaji wa sekta za kilimo na miundombinu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006, Tanzania iliendelea kufaidika na fursa mbalimbali zilizotolewa na Serikali ya China, chini ya Mpango wa Ushirikiano wa kiufundi kwa nchi zinazoendelea *(TCDC),* kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la

Umoja wa Mataifa *(UNDP)*. Wataalamu wa Kitanzania kutoka wizara na taasisi mbalimbali walihudhuria mafunzo nchini China kwenye maeneo ya teknolojia ya mianzi, uzalishaji umeme kwa njia ya maji, matumizi ya nguvu za jua, elimu ya usindikaji vyakula pamoja na uzalishaji wa samaki.

Mheshimiwa Spika**,** pamoja na Tanzania kuwa miongoni mwa nchi za Afrika chini ya Jangwa la Sahara zilizoidhinishwa na Serikali ya Marekani kunufaika na mpango wa AGOA, bado haijaweza kunufaika ipasavyo na fursa hii, ikilinganishwa na nchi zingine kama Lesotho, Kenya, Mauritius na Swaziland. Mwaka 2006 mapato yaliyotokana na mauzo chini ya mpango huu yalifikia dola za Marekani 4.2 milioni, ikilinganishwa na dola za Marekani 3.8 milioni zilizopatikana mwaka 2005, sawa na ongezeko la asilimia 11. Hata hivyo, Tanzania inayo nafasi kubwa ya kunufaika zaidi na mpango huu kwa kutumia rasilimali zetu kama madini, mazao ya misitu na mazao ya kilimo, ambazo ni nyingi na zinahitajika mahali pengi duniani. Changamoto iliyopo ni kupanua wigo wa bidhaa zinazouzwa chini ya mpango wa AGOA, kwani kuna aina 1,835 ya bidhaa zinazoweza kuuzwa chini ya mpango huu. Ni muhimu kuunganisha nguvu za wazalishaji wa bidhaa mbalimbali ili kuweza kuzalisha bidhaa bora na za kutosha kukidhi mahitaji ya soko la Marekani ambalo ni kubwa; kuongeza ubadilishanaji wa taarifa za kibiashara kati ya wafanyabiashara wa Tanzania na wa Marekani; kujenga uwezo wa wajasiriamali wetu ili waweze kuzalisha bidhaa zenye ubora na zinazoendana na mahitaji ya soko la Marekani.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wa sekta husika wataeleza kwa kina maendeleo katika sekta zao; hivyo katika hotuba hii, nitatoa vidokezo vichache tu juu ya maendeleo ya kisekta, hususan yale yanayogusa uchumi wa nchi, moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006 sekta ya kilimo ilikua kwa asilimia 4.1, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.1 mwaka 2005. Upungufu huu wa ukuaji unatokana na hali ya ukame katika maeneo mengi nchini mwetu katika msimu wa mvua wa mwaka 2005/06. Kama nilivyoeleza hapo awali, pamoja na kupungua kwa kiwango cha ukuaji wa sekta hii, iliendelea kutoa mchango mkubwa katika Pato la Taifa ikilinganishwa na sekta zingine, ambapo mwaka 2006 mchango wa sekta hii ulikuwa asilimia 44.7, ikilinganishwa mchango wa asilimia 45.6 mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza Sekta ya Kilimo na kuondokana na kilimo tegemezi cha mvua, kilimo cha umwagiliaji kiliongezeka kutoka hekta 264,388 mwaka 2005 mpaka hekta 278,388 mwaka 2006. Ongezeko hilo lilitokana na ujenzi wa mabanio ya skimu 4 kwenye ukanda wa kijani wa Ziwa Nyasa; matumizi ya teknolojia za umwagiliaji kwenye Ukanda wa Ziwa Victoria na mafunzo ya matumizi ya vifaa mbalimbali vya umwagiliaji kwa wakulima katika wilaya za Ilemela, Nyamagana, Magu, Maswa, Tarime na Bukoba. Juhudi hizi lazima ziendelee kwa kasi zaidi katika mwaka wa fedha 2007/08.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa mwaka 2007/08 malengo ya kukuza sekta ya kilimo yatakuwa kama yafuatayo:-

(i) kuimarisha mikakati ya kuongeza idadi ya wawekezaji binafsi katika sekta ya kilimo;

(ii) kuongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara; (iii) kuwafundisha wakulima matumizi ya vifaa mbalimbali vya umwagiliaji katika sehemu mbalimbali ambako kilimo cha umwagiliaji kinafanyika; na (iv) kuviwezesha vyama vya wazalishaji kuzalisha mazao ambayo yanakidhi matakwa ya soko la ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006 uzalishaji wa nyama uliongezeka na kufikia tani 388,294 ikilinganishwa na tani 378,509 mwaka 2005, sawa na ongezeko la asilimia 2.6. Aidha, uzalishaji wa maziwa nao uliongezeka na kufikia lita 1,412,786 ikilinganishwa na lita 1,386,400 mwaka 2005. Hata hivyo, uzalishaji wa ngozi ulipungua na kufika vipande 3,442,231 ikilinganishwa na vipande 3,700,000 viliyopatikana mwaka 2005. Upungufu huu wa ngozi ulisababishwa na ukame ambao ulisababisha upungufu mkubwa wa malisho na vyakula vya mifugo, na hivyo kupelekea kupungua kwa idadi ya wanyama waliochinjwa wanaotoa ngozi.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza mchango wa sekta ndogo ya mifugo katika Pato la Taifa, mpango wa mwaka 2007/08, unalenga yafuatayo:-

- kuendeleza na kuimarisha ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya mifugo, kama vile majosho,malambo n.k.;
- kuimarisha uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine wanaotoa huduma za mifugo;
- kuboresha mifumo ya malisho, tija, usindikaji na masoko ya bidhaa za mifugo;
- kuboresha upatikanaji wa pembejeo za mifugo, mazao ya mifugo na huduma za ukaguzi; na
- Kuandaa na kutekeleza mpango wa kudhibiti na kutokomeza magonjwa ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006 sekta ya viwanda ilikua kwa asilimia 8.6 ikilinganishwa na asilimia 9 mwaka 2005. Kupungua huku kwa ukuaji wa sekta hiyo, kulitokana na kupanda kwa gharama za umeme na mafuta ya kuendeshea mitambo na usafirishaji ambavyo vilichangia pia kuongezeka kwa gharama za uzalishaji katika sekta ya Viwanda kutoka shilingi 1,957,757 milioni mwaka 2005 mpaka shilingi 2,177,611 milioni mwaka 2006. Aidha, miundombinu hafifu, hususan reli na barabara, iliendelea kuchangia kupanda kwa gharama za uzalishaji viwandani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupungua kwa kiwango cha ukuaji wa sekta ya viwanda, mchango wake katika Pato la Taifa uliongezeka hadi asilimia 9.2, ikilinganishwa na asilimia 9 mwaka 2005. Kuongezeka huku kwa mchango wa sekta

katika Pato la Taifa kulichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa kama vile saruji, vinywaji, mabati, nondo, vyombo/vifaa vya plastiki na nguo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006, Serikali iliendelea kutekeleza sera za kuimarisha na kuendeleza viwanda vidogo vidogo na biashara, hii ikiwa ni pamoja na kuwawezesha wajasiriamali wadogo wadogo. Serikali kwa kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo Vidogo, ilitoa mafunzo kwa wajasiriamali 5,478 na wakufunzi 184. Shirika lilitoa pia mikopo yenye thamani ya shilingi 2.5 bilioni kwa vikundi vya wajasiriamali mbalimbali.

Mheshimiwa Spika**,** katika mwaka 2006, Mamlaka ya Kusimamia Programu ya Ukanda wa Kuzalisha Bidhaa za Kuuza nje (EPZA[11]) iliundwa. Aidha, maeneo yaliyopendekezwa kwa utekelezaji wa programu hiyo yapo katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Mwanza, Arusha, Kilimanjaro, Morogoro, Lindi, Ruvuma, Kigoma, Tanga, Mtwara, Mara na Kagera.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa mwaka 2007/08 unalenga kuweka mkazo kwenye mambo yafuatayo:-

- kuimarisha maendeleo ya Viwanda Vidogo na vya Kati (SMEs) na kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa kwa kusindika bidhaa za kilimo;

- kuvutia uwekezaji katika sekta za uzalishaji, kuongeza upatikanaji wa soko na kuboresha teknolojia za ”*biogas*” na mionzi ya jua;

- kuimarisha taasisi za maendeleo zinazojihusisha na utafiti;

- kutoa mafunzo ya ujasiriamali; na

- Kuendelea kutekeleza programu ya MKUMBITA[12] na Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006, Sekta ya Madini ilikua kwa asilimia 16.4 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 15.7 mwaka 2005. Aidha, mchango wa sekta hiyo katika Pato la Taifa uliongezeka hadi asilimia 3.8, ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika**,** mwaka 2006, thamani ya mauzo ya madini nje ilikuwa dola za Marekani 823.9 milioni, ikilinganishwa na dola za Marekani 711.3 milioni mwaka 2005. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 15.8. Mojawapo ya sababu za ongezeko hili inatokana hasa na ongezeko la bei ya dhahabu katika soko ya dunia.

Mheshimiwa Spika, katika Mpango wa Mwaka 2007/08, tutalenga kufanya yafuatayo:-

- kuendelea kuhamasisha maendeleo ya uwekezaji katika sekta ya madini;

- kuongeza thamani ya madini hapa nchini ili kuongeza mchango wa sekta ya madini katika Pato la Taifa;

- kuweka mikakati itakayoboresha na kuendeleza wachimbaji wadogo na wa kati; na

- kujenga maghala ya kuhifadhi udongo wa madini *(cores from exploration)* kwa ajili ya makampuni ya madini.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006 Sekta ya Nishati iliathirika sana na hali ya ukame uliyoikumba nchi yetu na kupanda kwa bei ya mafuta kwenye soko la dunia, ambavyo kwa pamoja vilisababisha upungufu mkubwa wa uzalishaji umeme unaotokana na nguvu za maji na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji wa umeme unaotumia mafuta.

Mheshimiwa Spika, pamoja na matatizo haya katika sekta hii, Serikali iliendelea kutekeleza miradi ya dharura ya nishati ya umeme kwa lengo la kuondoa uhaba na upungufu wa nishati nchini; ilifanya kazi ya upembuzi yakinifu juu ya taarifa za sesimiki *(Seismic data)* za upatikanaji gesi na mafuta ya petroli kwa maeneo ya Wilaya ya Kilwa; ilifanikiwa kwa kushirikiana na Kampuni ya Artumas kuchimba visima viwili vya majaribio huko Mnazi Bay (Mnazi Bay 2 na Mnazi Bay 3) Wilaya ya Mtwara Vijijini.

Mheshimwa Spika**,** Serikali pia iliunda kikosi-kazi *(task force)* kinachojumuisha taasisi za Serikali, sekta binafsi na taasisi zisizo za Serikali, kwa lengo la kutathmini maendeleo ya uzalishaji na matumizi ya **"***biofuel"* nchini, katika harakati za kuendeleza matumizi ya nishati mbadala na kundokana na tatizo la utegemezi wa umeme unaotokana na nguvu za maji na unaotumia mafuta.

Mheshimiwa Spika, katika Mpango wa Mwaka 2007/08, Serikali kwenye Sekta ya Nishati inalenga kufanya yafuatayo:-

- kuendeleza utekezaji wa Mradi wa Dharura wa Umeme (EPP);

- kuimarisha njia kubwa za umeme na kuboresha usambazaji katika vituo vidogo;

- kuwekeza zaidi katika Mnazi Bay na Mradi wa Maendeleo ya Songo Songo;

- kuanzishwa kwa mkakati maalumu wa hifadhi ya bidhaa za petroli na biashara ya petroli; na

- kuendelea kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala, pamoja na sera na sheria juu ya **"***biofuels*" nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika**,** katika mwaka 2006/07, kulikuwa na mafanikio yafuatayo katika sekta ya barabara: kilometa 9,934.33 za Barabara Kuu zinazounganisha mikoa na nchi jirani na kilometa 18,957.39 za Barabara za Mikoa zinazounganisha Wilaya na miji

mikuu ya mikoa nchini zilikarabatiwa; barabara kuu na barabara za mikoa zenye urefu wa kilometa 26,719.2 na madaraja 2,177 vilifanyiwa matengenezo ya kawaida na kingo za madaraja 179 zilitengenezwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006, kozi za kuwajengea uwezo wa kiutendaji makandarasi wazalendo katika mikoa ya Tanzania Bara ziliendelea kutolewa ambapo jumla ya makandarasi 1,615 walihudhuria kozi hizo na kufanya idadi ya makandarasi kufikia 2,989 tangu mpango huu wa mafunzo uanzishwe mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2007/08 mkazo mkubwa utaendelea kuelekezwa kwenye kutekeleza Programu Maalumu ya Maendeleo na Ukarabati wa Miundombinu katika mikoa sita ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Kigoma, Rukwa na Tabora inayojumuisha barabara za mikoa na barabara muhimu vijijini zinazokwenda kwenye maeneo ya uzalishaji ili viunganishwe na masoko na kurahisisha ugavi wa pembejeo za kilimo katika maeneo ya vijijini, na hivyo kuchochea ukuaji uchumi na kupunguza umaskini wa maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mawasiliano na Uchukuzi, katika mwaka 2006, Sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi ilikua kwa kiwango cha asilimia 7.5 ikilinganishwa na asilimia 6.4 mwaka 2005. Ongezeko hili la ukuaji limetokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika huduma za mawasiliano, hususan ongezeko kubwa la wateja wa simu za mkononi; na kuimarika kwa barabara nyingi ambako kumerahisisha uchukuzi wa shehena za mizigo hasa mazao ya kilimo na viwanda, malighafi na kuimarika kwa huduma za posta. Aidha, mwaka 2006, mchango wa sekta ya mawasiliano na uchukuzi katika Pato la Taifa umeendelea kuwa asilimia 5.4, kiwango ambacho ni sawa na cha mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika**,** katika mwaka 2006 baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya mawasiliano ni pamoja na ujenzi wa uzio katika viwanja vya ndege vya *Lake* Manyara, Musoma, Arusha, Bukoba, Mwanza, na Kigoma. Aidha, ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege cha Songwe uliendelea kwa ujenzi wa jengo la kuongozea ndege, jengo la zimamoto, na jengo la mapokezi/kuondokea abiria. Pia, Serikali ilifanikiwa kununua hisa zilizokuwa za Shirika la Ndege la Afrika Kusini la *SAA* ndani ya *ATCL* na hivyo kuweza kuimiliki kampuni ya *ATCL* kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ya sekta hii ni pamoja na Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)*, kufanya upembuzi yakinifu uliobainisha kuwa njia ya mkongo unaotumia vigae vya glasi *(optic fibre).* Gharama za matumizi yake ni nafuu na kuanzishwa kwa huduma ya simu isiyotumia waya *(fixed + wireless voice)* kwa kutumia teknolojia ya CDMA[13] pamoja na huduma mpya ya *"broadband —ADSL*[14]*"* kwa ajili ya huduma za *"data" na "internet"*. Aidha, maeneo ya bandari za mwambao yaliongezwa kina na kukarabatiwa; pamoja na ukarabati wa kituo cha mafuta cha Kurasini (KOJ[15]) Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika**,** katika mwaka 2007/08 kwenye Sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi, Serikali imelenga kufanya yafuatayo:-

- kutekeleza programu ya maendeleo na ukarabati wa miundombinu; na

- kuratibu na kuhakikisha usalama na utunzaji wa mazingira katika utekelezaji wa miradi ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwahamasisha wadau mbalimbali wa sekta ya elimu katika kuendeleza elimu ya awali, msingi na ile ya sekondari, hivyo kupelekea kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wa madarasa ya elimu ya awali, msingi na sekondari. Katika elimu ya awali idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka 47,867 mwaka 1997, hadi 669,137 mwaka 2006. Elimu ya msingi kiwango cha jumla cha uandikishaji (GER[16]) kimezidi kuongezeka kutoka asilimia 109.9 mwaka 2005 hadi 112.7 mwaka 2006. Kiwango halisi cha uandikishaji (NER[17]) nacho kilizidi kuongezeka kutoka asilimia 94.8 mwaka 2005 hadi 96.1 mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, pamekuwepo na ongezeko la kuridhisha la idadi ya wanafunzi wanaojiunga na elimu ya sekondari. Mwaka 2006 wanafunzi (kidato cha 1 - 6) walifikia 675,672 ikilinganishwa na wanafunzi 524, 325 mwaka 2005, sawa na ongezeko la asilimia 28.9. Kati ya wanafunzi hao wa mwaka 2006, wasichana walikuwa 317,544, sawa na asilimia 47 na wavulana walikuwa 358,128, sawa na asilimia 53 ikilinganishwa na wasichana 244,571, sawa na asilimia 46.6, na wavulana walikuwa 279,754, sawa na asilimia 53.4 mwaka 2005. Aidha, kutokana na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES) idadi ya wanafunzi waliojiunga kidato cha kwanza mwaka 2006 iliongezeka kufikia wanafunzi wapya 243,399, ikilinganishwa na wanafunzi 180,239 waliojiunga kidato cha kwanza mwaka 2005, sawa na ongezeko la asilimia 25.9. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imepata mafanikio makubwa katika maeneo mbalimbali ya elimu ya juu, ikiwemo ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kutoa elimu ya juu, kuboresha mazingira ya ufundishaji, pamoja na urekebishaji wa mitaala ili iendane na mahitaji ya soko la ajira. Idadi ya wanafunzi waliojiunga na vyuo vya ufundi vya umma imeongezeka hadi kufikia 2,466 mwaka 2005/06, ikilinganishwa na wanafunzi 2,242 mwaka 2004/05. Idadi ya waliojiunga na vyuo vya umma vya elimu ya juu mwaka 2005/06 nayo iliongezeka kufikia 35,606 ikilinganishwa na wanafunzi 34,113 mwaka 2004/05. Hata hivyo, idadi ya wanafunzi wa kike ilipungua kutoka 11,329 mwaka 2004/05, hadi 11,110 mwaka 2005/06. Idadi ya wanafunzi katika vyuo vikuu vya binafsi pia iliongezeka kutoka 3,554 mwaka 2004/05 hadi wanafunzi 5,275 mwaka 2005/06.

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM) umekamilika mwezi Desemba mwaka 2006. Hivi sasa utekelezaji wa awamu ya pili ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM II – 2007-2011) umeanza kutekelezwa. Mpango huu una lengo la kuendeleza pale awamu ya kwanza ya MMEM ilipoishia na kuboresha zaidi yale yaliyoachwa na MMEM I.

Pamoja na MMEM II, katika mwaka 2007/08, Serikali itaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) kwa lengo la kupanua na kuiboresha ili kukabiliana na ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaohitimu elimu ya msingi. Vilevile, Serikali itaendelea kuboresha zaidi mazingira ya kutoa elimu, uwiano

wa kijinsia, kuimarisha mfumo wa habari, elimu, mawasiliano, pamoja na mfumo wa uongozi katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika sekta ya elimu, bado sekta hii inakabiliwa na changamoto kadhaa, zikiwemo upungufu wa walimu, upungufu wa nyumba za walimu, upungufu mkubwa wa vifaa vya kufundishia, uwezo mdogo wa mamlaka zetu za Serikali za Mitaa kuhudumia sekta ya elimu, pamoja na jinsi ya kuongeza wigo wa kimapato ili kufidia gharama za utekelezaji wa mipango mbalimbali ya sekta hii.

Hata hivyo, Serikali imejizatiti kuongeza walimu na vifaa vya kufundishia, pamoja na kuongeza kasi ya uandikishaji wa wanafunzi na uboreshaji wa mazingira ya ufundishaji kwa walimu wa ngazi zote.

Katika mwaka 2006, Serikali yetu iliendelea kuhakikisha kuwa huduma bora ya maji safi na salama inatolewa kwa wananchi wa mijini na vijijini kwa kuwashirikisha wananchi kama sera inavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majanga mbalimbali yakiwemo ya ukame na ukosefu wa umeme yaliyoikumba nchi yetu mwaka 2006, bado huduma hii iliendelea kutolewa kwa kiwango cha kuridhisha kwa wananchi walio wengi japokuwa uzalishaji wa maji safi na salama ulipungua kiasi kutoka mita za ujazo 101,337,870 mwaka 2005 hadi mita 93,306,183.06 mwaka 2006.

Hata hivyo, usambazaji wa maji katika maeneo ya mijini uliongezeka kutoka asilimia 74.0 mwaka 2005 hadi asilimia 76 mwaka 2006.

Pia katika kuhakikisha kuwa vyanzo vya maji havichafuliwi, mitambo kadhaa ya kusafishia maji taka yanayotiririka katika mabonde ya Wami/Ruvu, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Mto Pangani ilikaguliwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2007/08, Serikali itaendeleza juhudi za kuongeza na kuboresha huduma za usambazaji maji safi na utunzaji wa vyanzo vya maji na mazingira kwa ujumla. Kwa kufanya hayo, idadi ya watu wanaopata huduma ya maji mijini na vijijini itaongezeka, vyanzo vya maji vitalindwa, na pia upatikanaji wa maji kwa kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua itaendelea kusambazwa na kudumishwa. Aidha, Serikali itaendelea kuhamasisha uanzishwaji wa kamati na mifuko ya maji na vyombo vingine kwa lengo la kuboresha huduma za maji nchini.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Afya ina malengo mengi likiwepo la kupunguza vifo vya uzazi na watoto walio na umri chini ya miaka mitano. Juhudi zaidi za kupunguza vifo vya watoto hawa kwa kiasi kikubwa zinakwamishwa na kuendelea kuongezeka kwa watoto wanaozaliwa wakiwa wameathirika na virusi vya UKIMWI, kuongezeka kwa idadi ya watoto yatima, na kuongezeka kwa kasi ya ugonjwa wa malaria. Katika mwaka 2006, vituo vya kutolea huduma za afya vikijumuishwa vya Serikali, sekta binafsi na

mashirika ya dini na ya kujitolea viliongezeka kutoka 5,284 mwaka 2005 hadi 5,379 sawa na ongezeko la asilimia 1.8.

Aidha, huduma maalumu kwa wanawake wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano, ziliendelea kutolewa nchi nzima bila malipo katika vituo vyote vya Serikali vya kutolea huduma hiyo ili kupunguza athari ya vifo hivi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/08, Serikali itaendelea kuboresha huduma za afya kwa kulenga katika maeneo yafuatayo:-

- Kuhakikisha kwamba madawa muhimu yakiwemo ya kurefusha maisha kwa walioathirika na UKIMWI yanapatikana;

- Kutekeleza kwa ufanisi mipango na mikakati mbalimbali ya afya ya jamii na ya msingi ukiwemo Mkakati wa Kutibu Magonjwa ya Watoto kwa Uwiano;

- Kuimarisha utafiti katika Sekta ya Afya.;
- Kukarabati Hospitali za Mikoa; na

- Kuimarisha kinga na tiba dhidi ya malaria

Mheshimiwa Spika**,** kuhusu masuala mtambuka, makadirio ya idadi ya watu Tanzania kwa kutumia takwimu za sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002 yanaonyesha kwamba mwaka 2006, idadi ya watu ilikuwa 38,669,744. Kati ya hao wanawake ni asilimia 51.0. Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na watu 37,526,206, ambapo Tanzania Zanzibar ilikadiriwa kuwa na watu 1,143,538. Kiwango cha ukuaji wa idadi ya watu nchini ni asilimia 2.9. Idadi ya watu Tanzania inakadiriwa kufikia watu 63,516,735 ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika**,** kuhusu ajira, matokeo ya Utafiti wa Nguvu Kazi uliofanyika mwaka 2005/06 yanaonyesha kuwa watu wenye uwezo wa kufanya kazi katika Tanzania Bara wameongezeka kutoka milioni 17.8 mwaka 2000/01 na kufikia milioni 20.6 mwaka 2005/06, sawa na wastani wa ongezeko la watu 760,000 katika soko la ajira kila mwaka. Kati ya hao, waliokuwa na kazi kwa tafsiri ya kitaifa walikuwa milioni 18.3, wanaume milioni 9.0 na wanawake milioni 9.3. Tafsiri ya kitaifa inazingatia mazingira ya ajira katika Tanzania ambapo sehemu kubwa ya watu wanafanya kazi za kujiajiri badala ya kuajiriwa. Aidha, kazi nyingi ni za msimu katika sekta ya kilimo na sekta isiyokuwa rasmi.

Mheshimiwa Spika**,** watu wasio na kazi walikuwa milioni 2.3 mwaka 2005/06, sawa na asilimia 11.0 kwa tafsiri ya kitaifa, ikilinganishwa na asilimia 12.9 mwaka 2000/01. Wanaume walikuwa milioni 1.0 na wanawake milioni 1.3. Katika Jiji la Dar es Salaam, asilimia 31.4 ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi walikuwa hawana kazi ikilinganishwa na asilimia 46 ya mwaka 2000/01.

Miji mingine asilimia 16.3 ikilinganishwa na asilimia 26.0 mwaka 2000/01; na vijijini asilimia 7.1 ikilinganishwa na asilimia 8.0 mwaka 2000/01. Ukosefu wa ajira uliwaathiri zaidi wanawake wa mijini na vijana kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika**,** Uchambuzi wa matokeo unabainisha kuwa mchango wa sekta rasmi ya umma yaani Serikali na mashirika umepungua sana katika kutoa nafasi za ajira. Badala yake, sekta ya kilimo, sekta isiyo rasmi na sekta nyingine binafsi ndizo zinazoajiri watu wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika**,** mapambano dhidi ya UKIMWI, takwimu za mwaka 2006 zinaonyesha kuwa kiwango cha maambukizi ya UKIMWI kilikuwa asilimia 8.2. Aidha, inakisiwa kuwa watu 1,816,326 walikuwa wanaishi na virusi vya UKIMWI nchini katika mwaka 2006, ambapo kati ya idadi hiyo, 672,778 wanaishi mijini na 1,143,548 wanaishi vijijini.

Kwa takwimu hizi, ni dhahiri kuwa kasi ya maambukizi ya UKIMWI nchini bado ipo juu na Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inakusudia kuhakikisha kuwa kasi hii inapungua kwa kiwango kikubwa. Katika kuhakikisha hili linafanikiwa, Serikali itahakikisha kuwa elimu sahihi juu ya njia bora za kujikinga na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) inawafikia watu wote kwa kushirikisha viongozi wa siasa, dini, taasisi za umma na watu binafsi katika kufanikisha suala hili. Pia Serikali itaendelea kuwahimiza wananchi kuendelea kupima afya zao kwa hiari ili kujiandaa kuishi kwa matumaini wakibainika kuwa wana virusi vya UKIMWI na hivyo kupunguza maambukuzi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006 Kamati ya Taifa ya Utandawazi iliboresha mpango-kazi wa kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Kimataifa ya Kijamii katika Utandawazi. Katika uboreshaji huo, Kamati ilizingatia matokeo ya tafiti zilizofanywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na Taasisi ya Tafiti za Kijamii na Kiuchumi (*ESRF*). Maeneo ya mpango-kazi huo yaliainishwa kwa kuzingatia matokeo ya utafiti wa utambuzi wa kazi zilizokwishafanyika katika eneo hili la utandawazi, changamoto mpya za utandawazi zinazotukabili, pamoja na utafiti kuhusu ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006 programu ya kitaifa iliendelea kutoa elimu ya jinsia katika sekta zote na jamii kwa ujumla. Wawakilishi wa masuala ya kijinsia kutoka katika Wizara mbalimbali walipata mafunzo. Aidha, mifumo mbalimbali ya kuhusisha masuala ya jinsia kwenye sera mbalimbali za maendeleo ya kiuchumi na kijamii iliandaliwa. Nakala 2000 za Mpango wa Taifa wa Kupambana na Ukatili dhidi ya Wanawake zilisambazwa kwa wadau wote.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006, Serikali iliendelea na shughuli za uhifadhi wa mazingira kwa kuandaa kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na kuandaa programu za kujenga uwezo wa utekelezaji wa sheria hiyo**.** Ili kuhifadhi na kuboresha mazingira, Serikali itaendelea kuelekeza rasilimali za kutosha pamoja na kuwashirikisha wananchi katika utunzaji na usimamizi endelevu wa mabonde na maeneo yenye vyanzo vya maji, kupanda na kuitunza miti, kudhibiti uchafuzi wa mazingira ya ardhi utokanao na taka za plastiki, na mpango wa matumizi bora ya ardhi

(*land-use planning*). Aidha, masuala ya mazingira yataendelea kuingizwa katika sera na mikakati ya sekta zote za uchumi nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mipango Maalumu, Serikali imeendelea kutekeleza malengo ya MKUKUTA kupitia programu na mipango ya kisekta kwa kushirikisha wadau mbalimbali. Serikali imechukua hatua kadhaa katika kuratibu utekelezaji wa MKUKUTA kama vile kuoanisha bajeti ya Serikali na malengo ya MKUKUTA; kuandaa mwongozo wa uandaaji mipango kwa kuzingatia vipaumbele vya kisekta vya maeneo ya MKUKUTA (*Medium Term Strategic Planning and Budget Manual*); na kuandaa Mkakati wa Pamoja wa Misaada kwa Tanzania (*Joint Assistance Strategy for Tanzania* - JAST).

Aidha, Mpango wa Kufuatilia Hali ya Umaskini (MKUKUTA *Monitoring Master Plan*) uliandaliwa na utekelezaji wake unaendelea. Mpango huu, umeainisha viashiria 84 vinavyotumika kupima utekelezaji wa MKUKUTA. Taarifa mbalimbali chini ya mpango huu hutolewa katika Ripoti ya Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu (*Poverty and Human Development Report* – PHDR), Ripoti ya Utekelezaji ya Mwaka ya MKUKUTA (RIMKU), na Ripoti ya Hali ya Utekelezaji wa MKUKUTA (MKUKUTA *Status Report*).

Ripoti ya kwanza ya Utekelezaji wa MKUKUTA (MKUKUTA *Status Report* 2006), inaonyesha kuwa kumekuwa na maendeleo ya kuridhisha katika juhudi za kukuza uchumi na kupunguza umaskini nchini katika maeneo ya umaskini wa kipato, huduma za jamii (elimu, afya, maji, n.k.) na utawala bora.

Aidha, Serikali iliendelea kuelekeza rasilimali zake nyingi katika maeneo ambayo yanachochea ukuaji wa uchumi, na hivyo kuongeza uwezo wa kupunguza umaskini. Maeneo hayo ni pamoja na kilimo, miundombinu ya barabara na nishati, na katika utoaji wa huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika**,** pamoja na athari za ukame ulioikumba nchi yetu, bado uchumi wetu uliweza kuhimili dhoruba hiyo na kukua kwa asilimia 6.2, kama nilivyoeleza hapo awali. Kilimo ambacho ndiyo mhimili mkubwa wa uchumi wetu kilikua kwa asilimia 4.1 chini ya kiwango cha ukuaji wa mwaka 2005. Ningependa kusisitiza hapa kuwa kilichopungua siyo kiasi cha uzalishaji katika sekta ya kilimo, bali ni kiwango cha ongezeko la uzalishaji au ukuaji, ndicho kilichopungua. Nimeyasema haya ili takwimu hizo zieleweke vyema na kupata tafsiri sahihi. Kwa hiyo, sekta hii iliendelea kuzalisha chakula na kutoa kipato cha kupunguza umaskini kwa wananchi walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006, kumekuwepo na mafanikio katika huduma za jamii, kama vile sekta ya elimu, afya na maji. Katika sekta ya elimu kiwango cha kufaulu mitihani, idadi ya shule zilizojengwa, vifaa na mazingira ya kufundishia, idadi ya wanafunzi wanaoanza darasa la kwanza, idadi ya wanaomaliza darasa la saba na wanaoingia kidato cha I na V imeendelea kuongezeka na mitaala ya elimu ya sekondari iliboreshwa.

Mheshimiwa Spika**,** Serikali imeendelea kuboresha afya ya mtoto na uzazi, kutoa chanjo na kuhudumia waathirika wa UKIMWI. Matokeo ya utafiti wa afya na idadi ya watu (TDHS[18]) wa mwaka 2004/05, yalionyesha kupungua kwa viwango vya vifo vya watoto wachanga kutoka watoto 99 mwaka 1999 hadi 68 mwaka 2005, kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai. Viwango vya vifo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano vilipungua kutoka 147 hadi 112 kwa kila watoto hai 1,000. Katika mwaka 2006 takriban watu 48,000 kati ya 100,000 walioathirika na ugonjwa wa UKIMWI walipatiwa dawa za kupunguza makali.

Mheshimiwa Spika, katika kudumisha utawala bora na uwajibikaji, Serikali iliendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na:- (i) kuimarisha jeshi la polisi; (ii) kuongeza idadi ya majaji wa Mahakama Kuu; (iii),kutunga upya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa; (iv) kuimarisha mfumo wa sheria na haki za binadamu; (v), kuhamasisha umma kuhusu haki za binadamu na wajibu wa jamii; na (vi) kuanza rasmi mchakato wa Mfumo wa Afrika wa Nchi kutathminiwa na kujipima zenyewe (APRM) katika masuala ya utawala bora na uwajibikaji.

Aidha, Serikali imeendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha za umma, kwa kuimarisha ofisi za ukaguzi katika Wizara, Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/07, Serikali iliendelea kutekeleza Awamu ya Pili ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii – TASAF II. Lengo la mfuko huo ni kusaidia jamii katika kuboresha maisha, huduma za jamii na kusaidia makundi maalumu wakiwemo watoto yatima, wajane, wazee, watu wenye ulemavu na wale wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo hayo Serikali itafanya yafuatayo:-

- Kuendelea kuhamasisha jamii kuhusu taratibu za utekelezaji wa TASAF II;

- Kwa kushirikiana na jamii, kuainisha vipaumbele vyao, kupanga na kutekeleza miradi, ikiwemo miradi ambayo haikukamilika katika Awamu ya Kwanza ya TASAF;

- Kutoa mafunzo ya kujenga uwezo wa usimamizi na kuboresha uwajibikaji kwa watendaji katika Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa, Majiji na Vijiji/shehia ili kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa ufanisi;

- Kusaidia utekelezaji wa miradi iliyoibuliwa na wananchi katika Halmashauri zote za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji kwa upande wa Tanzania Bara, na visiwa vya Pemba na Unguja kwa upande wa Tanzania Zanzibar; na

- Kuhamasisha uanzishwaji wa vikundi vya kuweka akiba na kuwekeza kupitia mpango wa *Community Savings and Investment Promotion* (COMSIP).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/08 TASAF II imepanga kutekeleza yafuatayo:-

- Kuendelea kutoa mafunzo kwa walengwa ili waweze kusimamia miradi yote wanayotekeleza kwa ufanisi mkubwa;

- Kushirikiana na wananchi kuibua na kutekeleza miradi mipya katika Halmashauri zote Tanzania Bara na Visiwa vya Unguja na Pemba kwa Tanzania Zanzibar; na

- Kufanya tathmini ya miradi inayotekelezwa ili kubaini kama malengo ya utekelezaji wa miradi yanafikiwa na walengwa wanapata huduma kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika**,** kuhusu Ukuzaji wa Sekta Binafsi na Uwekezaji, utekelezaji wa Mipango na Programu Mbalimbali, Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), limefanya mikutano mikubwa mitatu mwaka 2006/07 chini ya Mwenyekiti wake Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Madhumuni ya mikutano hii ni kuishauri Serikali jinsi ya kuboresha mazingira ya kiabashara na uwekezaji ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje. Mikutano hiyo ni pamoja na "*Investor Round Table*" kwa wawekezaji wa ndani na nje.

Aidha, kwa kupitia Baraza, Serikali iliendelea kuanzisha na kuendeleza shughuli za Mabaraza ya Biashara ya Mikoa kwa lengo la kupanua wigo wa mashauriano. Hadi Desemba 2006, Mikoa yote ilikuwa tayari imekwishaanzisha mabaraza hayo. Baadhi ya Mabaraza yaliyoweza kufanya warsha za uwekezaji ambazo ni Kilimanjaro, Mwanza, Mtwara, Mara na Rukwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa Kujenga Uwezo wa Ushindani katika Sekta Binafsi *(Private Sector Competitiveness Project),* Wajasiriamali wadogo na wa kati wamekuwa wakishindwa kuhimili ushindani wa soko. Matatizo yanayowapata ni pamoja na ukosefu wa mazingira bora ya kufanyia biashara. Ili kukabiliana na changamoto hizo, pamoja na mambo mengine, mwaka 2006 Serikali ilianza kutekeleza mradi wa "*Private Sector Competitiveness*" ambao unalenga katika kujenga mazingira yatakayowawezesha wajasiriamali wadogo na wa kati kuhimili ushindani katika soko la ndani na nje.

Aidha, mradi huo utatoa msaada wa kiufundi ili kuimarisha mipango ya biashara na uzalishaji ili waweze kuhimili ushindani wa soko. Matokeo ya utekelezaji wa mradi huo yanatarajiwa kuanza kubainishwa katika mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), unalenga katika kurasimisha biashara na rasilimali za wananchi. Mpango huu unatekelezwa katika hatua nne ambazo ni: (i) tathmini ya sekta isiyo rasmi (ii) utayarishaji wa maboresho katika sekta isiyo rasmi; (iii) utekelezaji wa maboresho katika sekta isiyo rasmi; na (iv) ukuzaji wa mitaji na

uimarishaji wa utawala bora. Hivi sasa, utekelezaji wa MKURABITA upo kwenye hatua ya pili, iliyokuwa imepangwa kukamilika ilipofika mwisho wa Juni 2006.

Hata hivyo, utekelezaji wa hatua ya pili uliweza tu kukamilika kwa Mikoa ya Dar es Salaam na Mbeya, na unaendelea katika sehemu zilizobaki**.**

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007 shughuli za MKURABITA ziligawanyika katika makundi makuu mawili ambayo ni shughuli za maandalizi ya maboresho kama zilivyoainishwa katika mkataba kati ya Serikali ya Tanzania na mshauri, ILD wa Peru na shughuli ambazo zimekwenda sambamba na maandalizi ya maboresho. Kama sehemu ya shughuli hizo, utafiti ulifanyika katika Wilaya 34 za Tanzania Bara na Wilaya 9 za Tanzania Zanzibar ili kutoa mapendekezo yatakayoboresha muundo wa sheria zinazosimamia umiliki wa mali na biashara Tanzania. Mapendekezo hayo yamejumuisha mabadiliko ya sera, sheria na taasisi husika ili iwe rahisi zaidi kwa Watanzania walio wengi kunufaika na sheria za umiliki wa mali na biashara. Mshauri, ILD, ameshatoa ripoti ya kwanza ya matokeo ya utafiti huu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania ikishirikiana na Serikali ya Norway ilifanya uchambuzi yakinifu wa tathmini ya taarifa ya kwanza ya mshauri kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba mapendekezo yaliyotolewa yanawiana vyema na programu zingine za kitaifa, na kwamba umiliki wa Kitanzania unadhihirika wazi katika matayarisho hayo.

Hivyo basi mfumo mpya umeshakubalika kati ya Serikali ya Tanzania na Mshauri ili shughuli zote za maandalizi ya maboresho ziongozwe kutoka Dar es Salaam na siyo Peru, kama ilivyokuwa hapo awali. Mpango-kazi unaoendana na makubaliano haya umeshaidhinishwa kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Norway, na utekelezaji wake ulianza mapema mwezi Machi 2007.

Mheshimiwa Spika, shughuli ambazo zimekwenda sambamba na maandalizi ya maboresho ni muhimu kufanyika ili kuweza kupata mafunzo yatakayoimarisha maboresho yanayokusudiwa. Shughuli hizi zimeendeshwa kwa kutumia bajeti ya Serikali. Baadhi ya shughuli zilizofanywa ni pamoja na zifuatazo:-

- Kufanya utafiti wa msingi wa sekta isiyo rasmi unaolenga kusaidia katika kuratibu ukuaji wa sekta hiyo. Kazi hii imefanywa na Ofisi ya Takwimu ya Taifa ikishirikiana na Kitengo cha Utafiti wa Uchumi cha Chuo Kikuu cha Dar es salaam *(ERB)* na iko mbioni kukamilika;

- Kutengeneza miongozo na taratibu ambazo zitawapa uwezo walengwa na watekelezaji kwa kushiriki kikamilifu katika suala zima la urasimishaji. Taratibu za kutengeneza kitabu cha rejea cha watoa huduma zimeshaanza ili kuwawezesha walengwa kupata huduma kwa wakati unaofaa na kwa bei inayofaa. Aidha, miradi ya majaribio na tafiti mbalimbali zitawezesha kuandaa miongozo mahsusi kwa ajili ya kusajili ardhi na biashara, na upatikanaji wa mikopo na huduma nyingine za kifedha;

· Kuwawezesha walengwa ambao kwa sasa wameshaanza mchakato wa kurasimisha rasilimali na biashara zao kukamilisha urasimishaji na kuanza kutumia rasilimali na biashara zao kupata mikopo na fursa nyingine katika soko rasmi. Mawasiliano na mabenki yanaendelea ili kuona uwezekano wa mabenki kurekebisha masharti hasa kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati. Mazungumzo yanaendelea na taasisi za fedha zifuatazo; Benki ya Akiba, *CRDB Bank Ltd, NBC, Eurafrican Bank;* na

. Kuanzisha mchakato wa kutengeneza taratibu za usajili ambapo rasilimali za majengo, ardhi na biashara, utambuzi wa watu na taarifa nyinginemuhimu zinaweza kupatikana kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Awamu ya Pili ya Maboresho na Mageuzi ya Sekta ya Fedha, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia, ilifanya mapitio ya maendeleo katika Sekta ya Fedha nchini na kubaini kwamba, pamoja na sekta ya fedha nchini Tanzania kuwa na mchango mkubwa katika kukuza uchumi, bado haijafikia upeo wa matarajio ya mchango wake katika uchumi wa Taifa letu.

Aidha, ilibainishwa kuwepo kwa haja ya kufanya maboresho kadhaa muhimu ili sekta hiyo iweze kuongeza mchango wake katika uchumi wa nchi. Pamoja na sekta hiyo kuwa na fedha nyingi zinazoweza kukidhi mahitaji ya wananchi kwa kiasi kikubwa, bado kuna matatizo makubwa katika utoaji wa mikopo, hususan ya muda mrefu.

Uchambuzi umeonyesha kuwepo kwa umuhimu wa kufanya maboresho katika sheria na taratibu mbalimbali pamoja na kuanzishwa kwa taasisi za kifedha zenye uwezo endelevu wa kutoa mikopo ya muda mrefu. Utekelezaji wa maboresho hayo ulianza mwaka wa fedha 2006/07 ambapo Bunge lilipitisha sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubinafsihaji hadi kufikia Juni 2006, Mashirika ya Umma 329 yalikuwa yamebinafsishwa na mali za mashirika zipatazo 638 zilikuwa zimeuzwa tangu Tume ya Rais ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma ilipoanzishwa mwaka 1993. Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2006, ubinafsishaji mkubwa uliofanyika ni pamoja na Serikali kuuza asilimia 25.0 ya hisa zake katika *Celtel Tanzania Limited* kwa kampuni ya *Mobile Systems International Cellular Investment* (T) BV, na asilimia 49.0 ya hisa zake za NMB kwa wawekezaji wanaoongozwa na *Rabobank* ya Uholanzi. Vilevile, Serikali iliuza kinu cha kusaga cha Kurasini kwa M/*S Century Food and Packing Ltd*.

Aidha, mashirika yafuatayo yako katika hatua mbalimbali za ubinafsishaji/ukodishaji:- TAZARA, Shirika la Bima la Taifa na vitengo vya kibiashara vya Mamlaka ya Bandari Tanzania (ukiondoa kitengo cha mizigo-*General Cargo* na kitengo cha makontena ambacho kilishakodishwa). Shirika la Reli la Tanzania limeshakodishwa kwa kampuni ya RITES ya India na mkataba kati ya kampuni hiyo na Serikali umeshatiwa saini. *RITES* itaanza rasmi kuliendesha Shirika la Reli ifikapo Septemba 2007.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Uwekezaji, katika mwaka 2006, Sekta ya Utalii ndiyo ilikuwa inaongoza kwa kuvutia wawekezaji wengi zaidi, ambapo miradi 205 ilikuwa imeidhinishwa. Sekta nyingine zilizovutia wawekezaji wengi ni pamoja (*idadi ya miradi iliyoidhinishwa katika mabano*) na bidhaa za viwandani (179); majengo ya biashara (114); usafirishaji (85); kilimo na mifugo (34); maendeleo ya rasilimali watu (21) na huduma (11). Mchanganuo wa umiliki wa miradi hiyo unaonyesha kuwa kulikuwa na wawekezaji wa ndani 345; wawekezaji wa nje 16; na wawekezaji kwa ubia 173.

Katika mwaka 2006, Kituo cha Uwekezaji (TIC) kiliidhinisha miradi 679 yenye thamani ya shilingi milioni 7,052,749.2 ambayo ilikuwa na fursa za ajira kwa watu 74,946 ikilinganishwa na miradi 550 yenye thamani ya shilingi milioni 1,876,063 mwaka 2005 ambayo ilitarajiwa kutoa fursa za ajira kwa watu 55,663.

Changamoto iliyopo ni kuhakiki matokeo ya uwekezaji huu, ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa nafsi za ajira. Lengo ni kujenga mfumo mahsusi wa ufuatiliaji. Lazima kuanza kujivunia zaidi miradi inayotekelezwa na kukamilika badala ya kupima mafanikio yetu katika miradi iliyosajiliwa tu na *TIC*.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipitisha Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi mwaka 2004 na kisha kuanzisha Baraza la Taifa la Uwezeshaji kwa Sheria ya Bunge Namba 16 ya mwaka huo huo. Baraza la Taifa la Uwezeshaji ni chombo cha kusimamia utekelezaji wa Sera hiyo. Uwezeshaji kiuchumi unachukua sura mbalimbali ili hatimaye kumwezesha mwananchi kutumia kikamilifu na kwa tija fursa zilizopo za kiuchumi ili aweze kumiliki uchumi, kuinua kipato na kuboresha maisha yao. Hivyo, uwezeshaji ni pamoja na kuwapatia wananchi fursa ya kupata mitaji na mikopo kwa ajili ya kuwekeza katika miradi ya kiuchumi, kurahisisha mazingira ya kufanya biashara, kupata elimu na maarifa ya ujasiriamali na kupata taarifa muhimu kuhusu masoko ya bidhaa wanazozalisha.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba kazi ya uwezeshaji ni jukumu la sekta zote na watendaji wa Serikali, Mashirika yasiyokuwa ya Serikali na sekta binafsi. Baadhi ya asasi na programu za uwezeshaji zimekuwepo kabla hata ya kuanzishwa kwa Sera ya sasa ya Uwezeshaji wananchi kiuchumi, pamoja na Sheria yake na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, na nyingine zimeanzishwa baada ya Sera kutolewa.

Katika mwaka 2006, Serikali ilikamilisha uundaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji kwa kuajiri watumishi wanaohitajika na kulipatia Baraza hilo ofisi na vitendea kazi. Taarifa za kina za utekelezaji wa shughuli mbalimbali za uwezeshaji zitatolewa na Wizara mbalimbali wakati zitakapowasilisha taarifa za utekelezaji wa mwaka uliopita na mpango wa mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha, utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji utaweka mkazo katika kuongeza na kurahisisha upatikanaji wa mitaji na

mikopo; kuhakikisha na kurahisisha upatikanaji wa elimu ya ujasiriamali; kuboresha mazingira ya biashara na upatikanaji wa taarifa muhimu za masoko ya bidhaa.

Aidha, Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi *(National Economic Empowerment Fund)* utaanzishwa rasmi kama Sheria Na. 16 ya 2004 inavyoelekeza. Wito wangu ni kuwaomba Sekta Binafsi, hasa Mabenki ya biashara na taasisi za kifedha kuchangia kutunisha mfuko huu. Pia nawaomba washiriki wetu wa maendeleo kuchangia mfuko huu ili tuwawezeshe wananchi wengi zaidi kunufaika na mikopo hii yenye masharti nafuu.

Kuhusu Kupeleka Madaraka kwa Wananchi *(D by D)*, kusudio la kupeleka madaraka kwa wananchi lilianza rasmi mwaka 1998 pale ilipoanzishwa Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa *(Local Government Reform Programme*). Maboresho haya yanafuata mtindo wa "*Decentralisation by Devolution*" *(D by D)* yaani kuhakikisha kuwa shughuli na miradi itakayohamishiwa kwenye Mikoa na Halmashauri inaendelea kuhamishwa pamoja na rasilimali zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006, Serikali iliamua kufanya tathmini ya Wizara sita kuhusu uzingatiaji wa zoezi hilo. Wizara hizo ni pamoja na Kilimo, Chakula na Ushirika; Elimu na Mafunzo ya Ufundi; Afya na Ustawi wa Jamii; Maendeleo ya Miundombinu; Maji na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambazo ndizo zinazoonekana kuwa na shughuli nyingi zinazoweza kuchangia kwa kiasi kikubwa kwenye suala zima la upelekaji madaraka kwa wananchi. Tathmini ya aina hiyo itafanyika kwenye Wizara zilizosalia katika mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008 Serikali itaendelea na utekelezaji wa sera hii ya kupeleka madaraka kwa wananchi kwa kuhakikisha kwamba fedha za miradi yote inayotekelezwa chini ya Serikali za Mitaa zinapelekwa moja kwa moja bila kupitia Wizara husika. Kwa mantiki hiyo, Serikali itazingatia yafuatayo:-

- Kutumia vizuri ripoti ya tathmini za *D by D* kuhusu dhana ya ugatuaji wa shughuli pamoja na rasilimali-fedha, watu na vifaa kwa ujumla;

- Katika utayarishaji wa mipango-mkakati *(strategic plans)* na *MTEF*, Wizara zitashirikiana na TAMISEMI katika nafasi yake kama mratibu mkuu wa *D by D* zinapofanya mabadiliko ya taratibu husika katika uendeshaji wa miradi; na

- Maandalizi ya programu mpya za kisekta yatazingatia sehemu za programu zitakazotekelezwa katika maeneo ya vijiji kwa usimamizi wa Halmashauri na mgawanyo wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza mageuzi ya kiuchumi katika kipindi cha muda wa kati, hususan katika kuendelea kutengamaza vigezo muhimu vya uchumi jumla, malengo *(targets)* katika mwaka 2007/2008 -2009/2010 yatakuwa kama ifuatavyo:-

(i) Pato la Taifa halisi litakua kwa asilimia 7.3 mwaka 2007, asilimia 7.7 mwaka 2008, asilimia 7.9 mwaka 2009 na asilimia 8.1 mwaka 2010;

(ii) Kudhibiti kasi ya upandaji mfumuko wa bei na kufikia chini ya asilimia 4.5 ifikapo mwishoni mwa Juni, 2008, kuendana na kasi ya upandaji wa mfumuko wa bei ya washirika wetu wakuu wa biashara;

(iii) Kuongeza mapato ya ndani kufikia uwiano na Pato la Taifa, kwa asilimia 18.0 mwaka 2007/2008, asilimia 18.1 mwaka 2008/2009 na asilimia 18.2 mwaka 2009/2010;

(iv) Kudhibiti ongezeko la ujazi wa fedha (kwa tafsiri pana, M2) lifikie kiwango kisichozidi asilimia 23.1 mwaka 2007/2008, asilimia 23.0 mwaka 2008/2009 na asilimia 22.6 mwaka 2009/2010 litakalowiana na malengo ya ukuaji wa uchumi na kasi ya upandaji mfumuko wa bei;

(v) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni itakayoweza kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma toka nje kwa kipindi kisichopungua miezi mitano;

(vi) Kuwa na kiwango cha ubadilishaji wa fedha kinachoendana na mwenendo wa soko la fedha (IFEM); na

(vii) Kupunguza tofauti kubwa iliyopo kati ya viwango vya riba za kukopeshwa na riba za amana katika mabenki ya biashara.

Mheshimiwa Spika, ili malengo hayo (targets) ya uchumi jumla yaweze kufikiwa, misingi ya malengo *(basis and assumptions)* hayo ya uchumi jumla na maendeleo ya jamii kwa kipindi cha muda wa kati (2007/2008– 2009/2010), ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa MKUKUTA na kuelekeza rasilimali zaidi katika maeneo yatakayokuza uchumi kwa haraka zaidi katika kipindi cha muda wa kati, ikijumuisha kilimo na miundombinu kama barabara, reli, nishati na kadhalika.

(ii) Kuendeleza mageuzi ya kiuchumi katika kipindi cha muda wa kati na kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika miaka ya nyuma;

(iii) Misaada na mikopo yenye masharti nafuu itaendelea kupatikana, japo kwa kiwango pungufu ikilinganishwa na kiwango cha mwaka 2006/2007, na kwamba unafuu wa madeni chini ya mpango wa *HIPC* utaendelea kutolewa na nchi wahisani na Mashirika ya Kimataifa;

(iv) Kuendelea kuongezeka kwa mitaji ya moja kwa moja kutoka nje, kutokana na kuboreshwa kwa mazingira ya biashara na uwekezaji;

(v) Benki Kuu ya Tanzania kuendelea kuimarisha sera za udhibiti wa mwenendo wa fedha nchini *(supportive monetary policy);*

(vi) Kuondolewa kwa vikwazo vya kimfumo na kimuundo katika sekta ya fedha, vinavyokwaza upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi; na

(vii) Kuimarishwa ushirikishwaji wa wananchi katika harakati za kukuza uchumi na maendeleo ya jamii kupitia Serikali zao za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea hali ya uchumi wa Taifa, matarajio, misingi na malengo hapo juu, mwenendo wa ukuaji wa uchumi jumla kwa mwaka 2006 unaonyesha wazi hatua zilizochukuliwa na Serikali kwa njia ya kutayarisha na kutekeleza sera, mikakati na programu mbalimbali za mageuzi. Kwa kiasi kikubwa zimeweza kuzaa matunda yaliyotarajiwa. Changamoto kubwa iliyopo ni ukuaji huo kuwiana na maendeleo ya kila Mtanzania (kumnufaisha mwananchi wa kawaida kuondokana na umasikini).

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kusisitiza kuwa masuala yatakayopewa kipaumbele katika kipindi cha muda wa kati, kama sehemu ya utekelezaji wa MKUKUTA na Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya Mwaka 2005, ni pamoja na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi; uwekezaji katika miundombinu; uendelezaji kilimo; maendeleo ya rasilimali watu; kuboresha utoaji wa huduma za jamii; kukuza soko la nje kwa kuongeza kiwango cha uuzaji wa bidhaa za asili na zisizo za asili; utekelezaji wa awamu ya pili ya maboresho na mageuzi ya Sekta ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, kasi ya ukuaji wa uchumi katika viwango vya juu na endelevu inahitajika ili kuweza kupunguza umaskini wa kipato na kuongeza ubora wa maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo hayo, juhudi zaidi na endelevu zitaelekezwa katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuendelea kutengamaza vigezo muhimu vya uchumi jumla, kwa mfano ukuaji wa Pato la Taifa, kasi ya upandaji bei, mapato ya ndani, na kadhalika;

(ii) Kuendeleza uwekezaji katika maeneo machache ambayo yatakuza na kuibua shughuli nyingine za kiuchumi kwa haraka, kama kilimo, miundombinu, viwanda na nishati;

(iii) Kuendelea kutekeleza mikakati na mipango maalumu, ikiwemo MKURABITA, TMTP2020, MKUMBITA na kadhalika;

(iv) Kuendelea kutekeleza sera na programu zitakazoibua fursa za kiuchumi na kujenga uwezo wa kujikwamua kiuchumi;

(v) Kuendelea kujenga mazingira yatakayovutia wawekezaji kutoka nje na ndani kuwekeza katika Kanda Maalumu za Kiuchumi *(SEZsI* na *EPZs II)*

zitakazozalisha bidhaa na huduma kwa wingi na ubora unaotakiwa katika masoko ya ndani na nje;

(vi) Kuendelea kuimarisha usimamizi wa kukusanya kodi na mapato mengine ya Serikali na kupanua wigo wa kodi. Aidha, hatua mahsusi zitachukuliwa kuimarisha ukusanyaji wa kodi na mapato mengine ya Serikali yatokanayo na mazao ya maliasili, hususan biashara ya mazao ya misitu, kwa mfano magogo, mbao, na kadhalika;

(vii) Kuongeza ufanisi katika Sekta ya Kilimo na hasa skimu za umwagiliaji ili kuongeza tija na kuboresha huduma za ughani;

(viii) Kuendelea kuhimiza uzalishaji wa bidhaa asilia na zisizo asilia kwa ajili ya kuuza nje, pamoja na kizingatia viwango vya ubora wa bidhaa hizo;

(ix) Kuziwezesha Serikali za Mitaa ki-madaraka na ki-rasilimali *(D by D3)* ili kuziongezea uwezo na ufanisi katika utekelezaji wa MKUKUTA;

(x) Kuongeza juhudi zaidi katika kutafuta nishati jadilifu ili kukidhi mahitaji ya nishati kama umeme wa nguvu za jua, upepo na "*geothermal*";

(xi) Kuelekeza rasilimali za kutosha, pamoja na kuwashirikisha wananchi katika utunzaji na usimamizi endelevu wa mazingira, hususan mabonde na maeneo yenye vyanzo vya maji, kupanda na kuitunza miti, kudhibiti uchafuzi wa mazingira ya ardhi utokanao na taka za plastiki na mpango wa matumizi bora ya ardhi *(land-use planning);*

(xii) Serikali itaendeleza kuwianisha masuala ya jinsia katika sera na mipango yake yote ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii;

(xiii) Kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI; na

(xiv) Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii ili kuwashukuru wote waliotusaidia. Ninapenda nizitaje baadhi ya nchi na Mashirika ya Kimataifa yafuatayo: Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF);* Mashirika mbali mbali ya Umoja wa Mataifa kama vile *UNDP, UNESCO, UNFPA, UNHCR, UNICEF, UNIFEM, FAO, IFAD, WFP, ILO* na *WHO*, Jumuiya ya Nchi za Ulaya, Mfuko wa Fedha wa Nchi Wanachama wa Uzalishaji Mafuta *(OPEC Fund),* Shirika la Maendeleo la Norway *(NORAD),* Shirika la Maendeleo la Marekani *(USAID),* Shirika la Maendeleo la Sweden *(SIDA)*, Shirika la Maendeleo la Finland *(FINNIDA),* Shirika la Maendeleo la Kanada *(CIDA)*, Shirika la Maendeleo la Denmark *(DANIDA)*, Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)*, Shirika la Maendeleo la Japan *(JICA),* Serikali ya Uswisi, Uholanzi, Ujerumani, Ufaransa, Uingereza, Hispania, China, Afrika Kusini, Kuwait, Italia, Ireland na nchi

nyingine zote marafiki na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa yasiyo ya Kiserikali *(NGOs).* Wote hawa wametoa mchango mkubwa sana katika maendeleo yetu. *(Makofi)*

Aidha, napenda nitumie nafasi hii kuwaomba washirika wetu wa maendeleo kutusaidia katika kipindi kijacho ili tuweze kufanikiwa zaidi katika vita dhidi ya umaskini na juhudi zetu za kuboresha maisha ya kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Ninatumaini kwamba hotuba zitakazofuata hasa zile za kuwasilisha Makadirio hazitakuwa na urefu huu tulioushuhudia.

Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa utamaduni wetu na taratibu zetu, hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji hujadiliwa baada ya kusikia pia hotuba ya Waziri wa Fedha ambayo leo atawasilisha saa 10.00. Kwa hiyo, mjadala utaanza Jumatatu ijayo.

Kabla sijasitisha shughuli za Bunge, nina matangazo mafupi tu kwamba Wabunge wote ambao ni wanachama wa Chama cha Mapinduzi wanaarifiwa kuwa kutakuwa na Mkutano kesho Ijumaa saa 3.00 asubuhi tarehe 15 katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Wale Wabunge wa CCM ambao hawana nyaraka za Mkutano wa kesho wanakumbushwa wapite pale ofisini kwa Katibu Mheshimiwa Ameir ili waweze kupata karatasi zao. Kuja hivi hivi kesho bila nyaraka itakuwa kidogo ni shida. Kwa hiyo, wote ambao hawana wapitie hapo.

Nimepokea lalamiko la Mheshimiwa Mbunge mmoja mwanamke kwamba kuna baridi sana humu ndani. Nimeamua kulipuuza kwa sababu tatu zifuatazo: Kwanza saa 10.00 tutasikiliza bajeti. Ni vizuri tuwe na baridi kuliko tuwe na joto. Pili, tutakuwa wengi zaidi humu, ukumbi utajaa na nimemwomba *Serjeant at Arms* baadhi ya wananchi ambao watakuwa wamefurika kuja kusikiliza bajeti tumeweka vyombo kuweza kuona na kusikia kila kinachoendelea kwenye *basement.* Kwa hiyo, usalama wawasaidie wananchi waweze kusikiliza hotuba kutoka kwenye *basement* kwa sababu hatutaenea humu.

Lakini tatu, Waheshimiwa Wabunge nimeona niipuuze tu taarifa hii ya baridi kwa sababu aliyeniandikia ni Mbunge mwanamke ambaye ameolewa hivi majuzi. Nalazimika kuipuuza kwa sababu kwa Mbunge ambaye anatoka kwenye fungate, ushauri wake kuhusu hali ya hewa siwezi kuukubali. *(Kicheko)*

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 10.00 kamili leo jioni.

*(Saa 06.22 Bunge lilifungwa Mpaka Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyotangaza wakati nasitisha shughuli za Bunge kwa Kikao cha leo pale asubuhi, nilieleza kwamba Kikao chetu kitaendelea saa 10.00 kwa shughuli ambazo zimepangwa. Kwa hiyo, namwita Katibu atusomee shughuli hizo ni zipi.

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2007/2008**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2007/2008. Pamoja na hotuba hii, vipo vitabu vinne vinavyoelezea kwa kina takwimu za Bajeti. Kitabu cha Kwanza kinahusu makisio ya mapato.

Kitabu cha Pili na cha Tatu ni vya makisio ya matumizi ya kawaida kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Halmashauri za Miji na Wilaya. Kitabu cha Nne kinaelezea makadirio ya matumizi ya maendeleo kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa pamoja na Halmashauri. Aidha, upo Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2007 ambao ni sehemu ya Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine kufanikisha matayarisho ya Bajeti hii. Napenda kuishukuru Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa kazi nzuri iliyofanywa na Kamati ya kuchambua mapendekezo ya Bajeti kwa makini na kutoa ushauri katika maeneo mbalimbali ya Bajeti inayopendekezwa. Ushauri wa Kamati hii umesaidia sana katika kukamilisha Bajeti ninayowasilisha hii leo.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu, kwa mara ya kwanza katika historia ya Bunge letu, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipata fursa ya kujadili Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2007/2008 hadi 2009/2010 mwezi Aprili, 2007. Mwongozo wa Serikali wa Mpango na Bajeti ni hatua muhimu katika maandalizi ya Bajeti inayowasilishwa na kujadiliwa na Bunge baadaye.

Nachukua nafasi hii kwa niaba ya Serikali kutoa shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wabunge kwa maoni yao mazuri ambayo kwa sehemu kubwa yamezingatiwa katika Bajeti hii. Utaratibu huu utaendelea katika miaka ijayo na kwa pamoja tutatumia fursa hii kuweka mikakati itakayoharakisha utekelezaji wa ahadi yetu ya kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani zangu kwa Wizara zote, Idara zinazojitegemea, Mikoa, Halmashauri za Miji na Wilaya, Taasisi za Kitaifa na Kimataifa

na Wawakilishi wa sekta binafsi, kwa michango yao iliyosaidia kufanikisha maandalizi ya Bajeti hii.

Naomba niishukuru kwa namna ya pekee Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutayarisha kwa wakati Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2007 na nyaraka mbalimbali za sheria ambazo ni sehemu ya Bajeti hii.

Aidha, napenda kuwashukuru wafanyakazi wenzangu wa Wizara ya Fedha, nikianza na Naibu Mawaziri wa Fedha, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib na Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Katibu Mkuu - Gray Mgonja, Naibu Makatibu Wakuu; Ramadhani Khijjah na Andrew Nyumayo, Wakuu wa Idara, Taasisi na Wafanyakazi wote wa Hazina.

Aidha, namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha hotuba hii, vitabu vya Bajeti, pamoja na nyaraka nyingine zinazohusu Bajeti hii kwa wakati. Mwisho, nawashukuru kipekee wataalam na wale wote waliotoa mapendekezo kuhusu maboresho ya ukusanyaji wa kodi mbalimbali na mapato mengine ya Serikali. Mapendekezo na ushauri wao umezingatiwa katika Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, tunakaribia mwisho wa mwaka wa kwanza wa fedha wa Serikali ya Awamu ya Nne. Katika mwaka huu wa kwanza tumeshuhudia mambo mengi mazuri na pia changamoto nyingi. Tangu mwezi Juni, 2006, tumepata Wabunge wapya watatu. Nachukua fursa hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba - Mbunge wa Kuteuliwa, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura - Mbunge wa Tunduru na Mheshimiwa Florance Essa Kyendesya - Mbunge wa Viti Maalum. Tunawakaribisha katika kikosi kazi cha Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya. *(Makofi)*

Aidha, nawapongeza waliochaguliwa kuiwakilisha Nchi yetu ya Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki ambao ni Mheshimiwa Dr. Didas John Massaburi, Mheshimiwa Dr. Aman Walid Kabourou, Mheshimiwa Dr. George Francis Nangale, Mheshimiwa Sylvia Kate Kamba na Mheshimiwa Septuu Nasoro. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Abdallah Ally Hassan Mwinyi, Mheshimiwa Dr. Said Gharib Bilal, Mheshimiwa Janeth Deo Mmari na Mheshimiwa Dr. Fortunatus Lwanyatika Masha. *(Makofi)*

Kuchaguliwa kwao kunathibitisha imani kubwa ambayo Watanzania kupitia Wabunge wao wanayo kwao. Ninawatakia mafanikio katika jukumu la kutetea maslahi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika mwaka huu, Taifa letu limepata heshima kubwa kwa kupewa nafasi za uongozi katika asasi za kimataifa. Nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Watanzania wana imani kubwa katika uwezo wake wa kumudu dhamana aliyokabidhiwa katika nyanja ya kimatafaifa. Akiwa mwanamke

wa kwanza kushika nafasi ya juu namna hiyo katika Umoja wa Mataifa, sina shaka kuwa ataitumikia kwa manufaa ya jamii yote ya wapenda maendeleo kote duniani.

Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dr. William Shija ambaye ameteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Vile vile, nampongeza Balozi Liberatta Mulamula kwa kuteuliwa kwake kuwa Katibu Mtendaji wa kwanza wa Sekretarieti ya Ukanda wa Maziwa Makuu. Uteuzi wa wenzetu hawa ni heshima kubwa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kufurahia matukio haya mazuri katika mwaka huu wa fedha, kumekuwa pia na matukio ya huzuni. Tumempoteza mwenzetu, Marehemu Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti, aliyekuwa Mbunge wa Tunduru na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge), aliyefariki dunia tarehe 4 Januari, 2007 kufuatia ajali ya ndege. Daima tutamkumbuka Marehemu Akukweti kwa bidii yake ya kazi na moyo wake wa upendo. Tunawakumbuka pia watumishi wa Serikali (John Bendera, Nathaniel Katinila, na Theresia Nyantori) ambao nao walifariki dunia kutokana na ajali hiyo ya ndege iliyotokea katika uwanja wa ndege wa Mbeya. Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahala pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa Bajeti 2006/2007. Malengo makuu ya uchumi mpana katika mwaka wa 2006/07 yalikuwa yafuatayo:-

(i) Pato halisi la Taifa lililengwa kukua kwa asilimia 5.9 mwaka 2006 na asilimia 7.3 mwaka 2007;

(ii) Kasi ya upandaji wa bei ilitakiwa isizidi asilimia 4.0 (kwa bei za mwaka 2001) ifikapo Juni 30, 2007;

(iii) Ukusanyaji wa mapato ya ndani ulikadiriwa kufikia asilimia 14.5 ya Pato la Taifa mwaka 2006/07;

(iv) Ongezeko la ujazi wa fedha (kwa tafsiri pana) lilitakiwa liwiane na malengo ya ukuaji wa uchumi na mfumuko wa bei;

(v) Akiba ya fedha za kigeni ilitakiwa itosheleze mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi mitano;

(vi) Mabadiliko muhimu katika sekta ya fedha yalitegemewa kuongeza upatikanaji wa mikopo ya uzalishaji na biashara; na

(vii) Serikali kuendelea kudhibiti deni la Taifa kwa mujibu wa Mkakati wa Taifa wa Madeni pamoja na Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya 1974 iliyorekebishwa mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, Mwenendo wa viashiria hivyo muhimu vya uchumi mpana katika kipindi cha miezi tisa ya mwanzo ya mwaka wa fedha (Julai 2006 - Machi 2007)

kwa ujumla unaridhisha, hasa ikizingatiwa kwamba miezi sita ya kwanza ya mwaka wa fedha wa 2006/07, nchi ilikumbwa na janga la ukame lililosababisha uhaba mkubwa wa chakula na ukosefu wa umeme. Uhaba wa chakula ulichangia kwa kiasi kikubwa kupanda kwa bei za ndani na kuongeza mfumuko wa bei ambao ulifikia asilimia 7.3 mwisho wa Februari, 2007 ikilinganishwa na asilimia 6.8 mwezi Juni, 2006.

Hata hivyo, takwimu za mwezi Aprili 2007, zinaonyesha kwamba mfumuko wa bei umeshuka hadi asilimia 6.1, hasa kutokana na kushuka kwa bei ya chakula. Takwimu za awali za uchumi zinaonyesha pia kwamba Pato la Taifa mwaka 2006 lilikua kwa asilimia 6.2 kiwango ambacho ni cha chini ikilinganishwa na asilimia 6.8 mwaka 2005. Hata hivyo kiwango hicho cha asilimia 6.2 cha ukuaji wa Pato la Taifa mwaka 2006 ni cha juu kuliko lengo la asilimia 5.9.

Aidha mwishoni mwa mwezi Machi 2007, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa inatosheleza mahitaji ya uagizaji ya miezi 5.3 kama ilivyolengwa. Matokeo haya ya viashiria vya uchumi mpana yanaonyesha kwamba kama lisingekuweko janga la ukame, uchumi ungekua kwa kasi kubwa zaidi ya asilimia 6.2.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2006/07, Serikali ililenga kupata mapato ya jumla ya Shilingi bilioni 4,850.588 (trilioni 4.85) kutoka kwenye vianzio vya ndani na misaada ya nje. Aidha, Serikali ilipanga kutumia kiasi hicho hicho kwa matumizi yake ya kawaida na ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2006/07, Serikali ililenga kukusanya mapato ya ndani yasiyopungua shilingi bilioni 2,460.995 (trilioni 2.460).

Ili kufikia lengo hilo la mapato ya ndani, Serikali ilitekeleza mambo mbalimbali ambayo ni pamoja na kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara, kupanua wigo wa kodi kwa kusajili walipa kodi wapya, kuendelea kurekebisha mfumo wa kodi; kusimamia kwa karibu utekelezaji wa mageuzi makubwa ndani ya Mamlaka ya Mapato *(TRA)* chini ya Mpango wake wa mageuzi ambao umekuwa msingi wa kukua kwa mapato mwaka hadi mwaka; na kuimarisha Idara ya Walipakodi Wakubwa kwa kuboresha utendaji; kuweka nguvu zaidi katika usimamizi na utendaji wa Forodha, matumizi ya tekinolojia na kupunguza kero kwa walipakodi; kuziba mianya ya kukwepa kodi na kuongeza ufanisi wa kukusanya mapato yasiyo ya kodi kutoka Wizara na Idara mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2006 hadi Machi, 2007, mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 2,002.4 (trilioni 2.0) au asilimia 81.4 ya Bajeti ya mwaka na asilimia 109.7 ya matarajio kwa kipindi hicho. Vile vile katika kipindi hicho, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilivunja rekodi ya ukusanyaji wa mapato kwa kukusanya shilingi bilioni 259 kwa mwezi wa Machi 2007.

Tatizo la umeme lililoendelea hadi Desemba 2006, halikuwa na athari kubwa katika ukusanyaji wa mapato ya ndani, kwa kuwa *TANESCO* iliagizwa na Serikali isikate umeme kwa viwanda ili kulinda mapato ya Serikali. Matokeo mazuri ya ukusanyaji wa

mapato yanatokana pia na utekelezaji wa hatua za mapato zilizoidhinishwa katika Bajeti ya 2006/2007. Kwa ujumla, vianzio vyote vya mapato ya ndani vinafanya vizuri, isipokuwa ushuru wa bidhaa kwa mafuta ya Petroli na *VAT* kwa bidhaa zinazotoka nje.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu wa 2006/2007, Serikali ilitekeleza hatua mbalimbali za sera na mfumo wa kodi kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ilipunguza kodi ya mapato kutoka asilimia 30 hadi asilimia 25 kwa makampuni mapya yanayojisajili katika Soko la Mitaji la Dar es Salaam na kuuza angalau asilimia 35 ya hisa zao kwa wananchi. Punguzo hili ambalo ni kwa muda wa miaka mitatu limelenga kushawishi makampuni mengi ya binafsi kujiandikisha katika Soko la Hisa na kuongeza umiliki wa wananchi katika makampuni ya Tanzania. Serikali pia ilipunguza kiwango cha kodi ya zuio kwa mapato ya riba ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja *(Collective Investment Schemes)* kutoka asilimia 30 hadi asilimia 10 ili kuhamasisha uwekezaji wa pamoja nchini. Matokeo ya hatua hizi yanategemewa kuonekana katika kipindi cha muda wa kati na mrefu ujao.

Naomba nitumie nafasi hii kutoa wito kwa kampuni za binafsi zijitokeze kutumia fursa hii na kujiandikisha katika Soko la Hisa ili zichangie katika kukuza soko hilo hapa nchini.

(ii) Viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji baridi, bia, mvinyo kutoka nje ya nchi, vinywaji vikali na sigara viliongezwa kwa asilimia saba (7). Hatua hii iliipatia Serikali mapato ya shilingi bilioni 2.390 ambayo ni asilimia 18 zaidi ya kiwango kilichokadiriwa katika kipindi cha Julai – Desemba, 2006.

(iii) Serikali iliongeza kiwango cha Ushuru wa Bidhaa kwenye huduma za mawasiliano ya simu za mkononi kutoka asilimia 5 hadi asilimia saba (7) ya mauzo ili kuongeza mapato na kupunguza tofauti ya viwango vinavyotozwa katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Hatua hii iliipatia Serikali mapato ya ziada ya shilingi bilioni 15.661 katika kipindi cha Julai, 2006 hadi Januari, 2007.

(iv) Marekebisho mbalimbali yalifanywa pia katika viwango vya Ushuru wa Forodha chini ya Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuya ya Afrika Mashariki. Marekebisho hayo yalihusu zaidi malighafi za sabuni, na za karatasi. Aidha, ushuru kwa mitungi ya gesi *(LPG Cylinders)* ilifutwa ili kuhamasisha matumizi ya gesi na kulinda mazingira. Utekelezaji wa hatua hizo kwa pamoja umeipatia Serikali mapato kiasi cha shilingi bilioni 2.998 katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2006.

(v) Ushuru wa mafuta ya petroli uliongezwa kutoka shilingi 90/= kwa lita ya petroli na dizeli, hadi Sh. 100/= kwa lita, ili kuongeza mapato kwa ajili ya matengenezo ya barabara. Hatua hii imeiingizia Serikali mapato mapya kiasi cha shilingi bilioni 5.98 katika kipindi cha Julai, 2006 hadi Januari, 2007 na inategemewa kuingiza mapato mapya zaidi ya shilingi bilioni 10.0 ifikapo mwisho wa mwaka huu wa fedha.

(vi) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha ilifanyiwa marekebisho yaliyolenga kuipa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha *(The Gaming Board)* mamlaka ya kukusanya kodi kutoka kwenye michezo hiyo kwa niaba ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA).*

Marekebisho mengine yalikuwa ni kubadilisha utaratibu wa kutoza kodi kutoka katika *Casino* ili badala ya kutoza viwango maalum kwa vifaa vya kuchezea michezo hiyo, kodi hiyo itozwe kwa kiwango cha asilimia 13 ya mapato yote yatokanayo na michezo ya kubahatisha.

Hatua hii imeipatia Serikali mapato ya shilingi bilioni 2.2 katika nusu mwaka ya kwanza ya mwaka huu wa fedha ikilinganishwa na mapato ya shilingi bilioni 1.1 yaliyokuwa yanatarajiwa kukusanywa hapo awali katika kipindi hicho.

(vii) Ushuru wa Forodha kwenye mafuta ghafi ya kula *(Crude Palm Oil)* kutoka nje ya nchi uliongezwa kutoka asilimia sifuri hadi asilimia 10. Lengo la hatua hii lilikuwa ni kuhamasisha kilimo cha mbegu za mafuta hapa nchini na hivyo kuongeza pato la Wakulima wa Tanzania. Taarifa zinaonyesha kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la bei za mbegu za mafuta, hasa alizeti na mbegu za pamba, katika msimu uliopita. Serikali itaendelea kutoza ushuru huo kwa mafuta yanayoagizwa kutoka nje ili kuwalinda wakulima wetu.

(viii) Ushuru wa Bidhaa kwa mifuko ya *plastic* inayoruhusiwa uliongezwa kutoka asilimia 15 hadi asilimia 120, ili kupunguza matumizi ya mifuko hiyo na hivyo kuzuia uchafuzi wa mazingira. Tathmini inaonyesha kwamba hatua hii ina dalili za mafanikio kwa kuwa matumizi ya mifuko ya *plastic* yameanza kupungua.

(ix) Serikali iliweka kodi ya Ushuru wa Bidhaa wa asilimia 20 kwa magari madogo yenye umri wa miaka 10 na zaidi. Hatua hii ililenga kupunguza uingizaji nchini wa magari chakavu ambayo yana madhara makubwa kwa mazingira na yana gharama kubwa za matengenezo.

(x) Serikali pia ilifanya marekebisho kadhaa katika Sheria ya *VAT* kwa nia ya kulinda mazingira nchini. Marekebisho yaliyofanyika ni pamoja na kutoa msamaha wa *VAT* kwa gesi ya kupikia ya *LPG* na mitungi ya kuhifadhia gesi hiyo kwa lengo la kuhamasisha wananchi kutumia nishati ya gesi na kupunguza matumizi ya mkaa na kuni ili kulinda mazingira. Matokeo ya hatua hii yanategemewa kuonekana katika kipindi cha muda wa kati na mrefu ujao.

(xi) Kifungu cha 19 (2) cha Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 kilichokuwa kinaikataza Serikali kubadili mfumo wa kodi kwa wawekezaji, kilifanyiwa marekebisho ili kiwe kinahusu wawekezaji mahiri pekee. Aidha, msamaha wa kodi ya magari madogo ya binafsi *(non utility vehicles)* kwa wawekezaji uliondolewa na kubakiza msamaha huo kwa magari ya kazi *(utility vehicles)* tu. Lengo la hatua hii ni kupunguza misamaha ya kodi isiyo na tija na ambayo inafuja mapato ya Serikali.

(xii) Kodi ya Ongezeko la Thamani iliondolewa kwenye bidhaa za petroli ili kupunguza athari za ongezeko la bei ya mafuta hayo kwa watumiaji wa mwisho. Aidha, viwango vya ushuru wa bidhaa kwa mafuta ya petroli vilirekebishwa ili kulinda mapato ya Serikali. Vile vile, Serikali iliongeza muda wa usafirishaji wa mafuta ya petroli kwenda nchi za jirani kutoka siku 15 hadi siku 30 ili kurahisisha na kuongeza ufanisi katika biashara ya mafuta ya petroli kati ya Tanzania na nchi jirani bila kuathiri mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji mzuri wa mapato ya ndani ni matokeo ya sera sahihi za uchumi na usimamizi imara wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali, hasa mapato ya kodi. Hatua nilizozitaja hapo awali zilizotekelezwa na ambazo zinaendelea kutekelezwa, zimechangia katika ongezeko la ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, misaada na mikopo ya Bajeti ya 2006/07 hadi mwezi Machi 2007 ilifikia shilingi bilioni 745.685 ambayo ni asilimia 93 ya makadirio ya mwaka mzima. Wahisani wengi walitoa sehemu kubwa ya misaada ya Bajeti katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha kulingana na makubaliano baina yao na Serikali chini ya utaratibu wa *'General Budget Support'*.

Aidha, misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo haipitii katika Bajeti moja kwa moja, ilifikia shilingi bilioni 726.332 katika kipindi cha Julai, 2006 hadi Machi, 2007, sawa na asilimia 92 ya makisio ya mwaka mzima. Kutolewa mapema misaada ya Bajeti *(GBS)* kuliiwezesha Serikali kukabiliana na dharura zilizojitokeza katika nusu ya kwanza ya mwaka 2006/07.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2006 – Machi, 2007 matumizi ya Serikali kwa ujumla yalikuwa shilingi bilioni 3,415.412 (trilioni 3.41) sawa na asilimia 70.4 ya Bajeti ya mwaka mzima wa 2006/2007 ya shilingi bilioni 4,850.6 au asilimia 94 ya makisio ya shilingi bilioni 3,638.314 (trilioni 3.6), katika kipindi hicho. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 2,134.621 (trilioni 2.1) zilikuwa za matumizi ya kawaida, na shilingi bilioni 1,280.791 (trilioni 1.281) matumizi ya maendeleo.

Matumizi ya kawaida ni pamoja na mishahara ya wafanyakazi wa Serikali na Taasisi zake, malipo ya madeni, pensheni, madawa, vifaa vya tiba na vya kufundishia, nyenzo za kufanyia kazi na gharama nyingine za utawala na uendeshaji wa Serikali. Matumizi hayo ni pamoja na yale ya dharura ambayo yalipatiwa fedha kutokana na uhamisho wa ndani kwa ndani na kutokana na akaunti ya msamaha wa madeni ya *IMF*.

Kiasi cha shilingi bilioni 18.7 kilitumika kununulia chakula cha njaa kutoka nje na inategemewa kwamba shilingi bilioni 204.5 zitatumika hadi kufikia mwisho wa Juni, 2007 kulipia mitambo ya kununua na ya kukodi ya kuzalisha umeme. Aidha, Serikali ilitoa ruzuku ya shilingi bilioni 20 kwa *TANESCO* mwezi Desemba, 2006 na iliidhamini *TANESCO* kukopa kutoka benki kiasi cha shilingi bilioni 126.5.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ya dharura ambayo yalipatiwa fedha kwa njia ya uhamisho wa ndani kwa ndani ni pamoja na malipo ya madeni ya ndani

yaliyoongezeka kutokana na kupanda ghafla kwa riba ya dhamana za Serikali, mahitaji ya walimu wa shule za sekondari kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi waliofaulu mitihani ya Darasa la Saba na wananchi kujitolea kujenga shule kwa wingi ili watoto wasome, gharama za kusambaza chakula kutoka kwenye Hifadhi ya Taifa ya Chakula *(SGR)*, kupeleka kwenye maeneo yaliyokumbwa na njaa, gharama za kununua na kusambaza chanjo kukabili mlipuko wa Homa ya Bonde la Ufa na dharura nyingine.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha usimamizi wa fedha za umma kwa kuongeza uwezo na uwajibikaji Serikalini. Hatua zilizochukuliwa katika mwaka huu ni pamoja na kuongeza idadi ya Halmashauri *(LGAs)* zilizounganishwa katika mtandao wa kudhibiti malipo Serikalini *(Integrated Financial Management System (IFMS)* hadi 85 kati ya Halmashauri 122. Halmashauri 37 zilizosalia zitaunganishwa katika mtandao ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha 2007/08. Katika Bajeti ya 2006/07 Serikali Kuu iliahidi kuziwezesha Halmashauri za Wilaya na Miji kujenga uwezo wa utendaji na utaalam, hasa katika fani ya Uhasibu na Ukaguzi wa Ndani. Katika kutekeleza ahadi hii, Serikali imeajiri Wahasibu 207 na Wakaguzi wa Ndani 64 ambao wamesambazwa kwenye Halmashauri mbalimbali nchini. Serikali imeendelea pia kuimarisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuipatia vitendea kazi vya kisasa hadi katika ngazi ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha kufuatilia matumizi ya Serikali kilichopo Wizara ya Fedha kiliimarishwa mwaka huu. Aidha, Kitengo cha kukagua miradi ya maendeleo pia kimeendelea kuimarishwa. Jumla ya miradi 197 kote nchini imefanyiwa tathmini mwaka huu wa 2006/2007.

Jitihada hizi za kusimamia matumizi ya fedha za umma zilifikia katika hatua ya kipekee tarehe 15 Aprili, 2007 wakati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alipoitisha kikao maalum cha wahusika wote Serikalini, kujadili taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Hesabu za mwaka wa fedha wa 2005/2006.

Katika kikao hicho, Mheshimiwa Rais alielekeza mambo ya msingi yanayopaswa kutekelezwa na Viongozi katika kila Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi, Mikoa na Halmashauri. Maelekezo hayo ni pamoja na kuwataka Viongozi Wakuu wa Vyombo vyote vya Umma kusimamia na kuwajibika kikamilifu katika kudhibiti mapato na matumizi ya umma.

Aidha, Viongozi walitakiwa kuratibu kwa karibu zaidi mwenendo wa mapato na matumizi ili kuhakikisha kuwa sheria na kanuni zote kuhusu ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa matumizi zinafuatwa kikamilifu. Vile vile, Mheshimiwa Rais aliwaelekeza viongozi hao kuchukua hatua juu ya hoja mbalimbali zilizobainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika taasisi zao.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwaelimisha wadau na watendaji wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004. Sasa hivi limeanza zoezi la kuchambua kwa undani matatizo yaliyomo

kwenye Halmashauri ili kuandaa mpango mathubuti wa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu, ambao utahakikisha kuwa Halmashauri zina wataalamu wenye ujuzi wa kutosha kuhusu Kanuni za Ununuzi wa Umma. Aidha, Kanuni za Ununuzi za Serikali za Mitaa zimeshasainiwa na mamlaka yenye dhamana hiyo na sasa ziko katika hatua ya mwisho ya kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali ili zianze kutumika mara moja. Ni matumaini yangu kuwa Kanuni hizo zitasaidia kupunguza matatizo na migogoro ya Ununuzi kwenye Serikali za Mitaa. Hili ni eneo muhimu sana katika kudhibiti matumizi ya fedha za Serikali kwa kuwa sehemu kubwa ya Bajeti ya Serikali inatekelezwa kupitia ununuzi wa vifaa, mitambo, madawa, na mahitaji mengine.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2006/07, Serikali imeendelea kutekeleza Mpango wa Awamu ya Pili wa mageuzi katika Sekta ya Fedha kwa lengo la kuwawezesha wananchi kutumia Sekta ya Fedha katika kujiletea maendeleo na kufanya sekta hii itoe mchango wake kamili katika kukuza uchumi wa nchi. Hatua zilizochukuliwa katika eneo hili ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Serikali karibu itakamilisha Muswada wa sheria utakaoweka mazingira ya kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa njia ya ukodishaji vifaa, mitambo na rasilimali nyingine.

(ii) Ili kuboresha mazingira ya upatikanaji wa mikopo ya nyumba *(mortagage finance)* nchini, Serikali inaandaa muswada wa marekebisho ya vipengele kadhaa vya Sheria ya Ardhi na sheria nyingine, pamoja na kutunga sheria ya *Condominium* kama wadau walivyoshauri.

(iii) Serikali inaendelea kudhamini mikopo ya benki kwa wananchi kupitia mifuko yake inayosimamiwa na Benki Kuu ambayo ni Mfuko wa Dhamana kwa Miradi ya Maendeleo ya muda wa kati na mrefu, Mfuko wa Dhamana ya Mikopo kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi na Mfuko wa Dhamana ya Biashara Ndogo Ndogo.

(iv) Hadi mwisho wa mwezi Machi, 2007, Mfuko wa Dhamana kwa Miradi ya Maendeleo ulitoa udhamini kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 19.61, Mfuko wa Dhamana wa Biashara Ndogo Ndogo ulitoa udhamini wa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.204, na Mfuko wa Dhamana wa Uuzaji Bidhaa Nje ulikuwa umetoa udhamini kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 149.17.

Aidha, Serikali inaendelea kuimarisha mifuko hiyo ili wananchi wengi zaidi wafaidike na dhamana inayotolewa na mifuko hiyo.

(v) Katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 Serikali ilianzisha mpango maalum wa kuwawezesha wananchi kupata mikopo ya masharti nafuu ya fedha kupitia benki za *CRDB* na *NMB* kwa kudhaminiwa na Serikali. Chini ya utaratibu huu, kila mkoa ulitengewa takriban shilingi bilioni moja. Benki Kuu kwa kushirikiana na benki za *CRDB* na *NMB* imeweka utaratibu wa kuwasaidia wananchi kupata mafunzo mbalimbali kuwawezesha kupata mikopo kupitia utaratibu huu. Aidha, taratibu zinakamilishwa ili kuijumuisha Zanzibar katika mpango huu. Ni matumaini ya Serikali kwamba waombaji

sasa wanaelewa kanuni husika na kwamba itakuwa rahisi zaidi kushiriki katika awamu ya pili ya mpango huu pale itakapotangazwa kuanza.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyoundwa kwa mujibu wa Ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha Sura ya 140; imewasilisha Serikalini mapendekezo yake kuhusu vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano. Mawaziri wa Fedha wa Serikali ya Muungano Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wemekutana na kukubaliana kwamba kila upande ukamilishe uchambuzi wa mapendekezo ya Tume na kuwasilisha maoni yao kwa Kamati ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri Kiongozi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha, uhusiano wa Tanzania na nchi marafiki na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa, umeendelea kuimarika. Tumeendelea kupata misaada na mikopo yenye masharti nafuu na kufutiwa madeni ya zamani ili kusukuma maendeleo ya nchi yetu. Mwezi Desemba, 2006, Serikali ya Tanzania na Wahisani 19 wakiwemo Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Jumuiya ya Ulaya na Umoja wa Mataifa, tulitia saini Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania *(MPAMITA)* au *Joint Assistance Strategy for Tanzania (JAST)* kwa Kiingereza.

Pamoja na mambo mengine, mkakati huu unawataka Wahisani waongeze misaada na mikopo ya masharti nafuu kupitia kwenye bajeti ya Serikali na kuweka mgawanyo mzuri wa majukumu baina ya Wahisani na kati ya Wahisani na Serikali unaozingatia uzoefu na uwezo linganishi *(comparative advantage)* miongoni mwa Wahisani. Katika mkakati huu, Serikali ya Tanzania inaachiwa jukumu la kupanga vipaumbele vyake na kuamua kuhusu mahitaji na aina ya ushauri wa kitaalam *(technical assistance)* inaotaka, bila kusukumwa na Wahisani. Serikali pia inawajibika katika matumizi ya misaada inayopata pamoja na rasilimali zote za umma.

Mheshimiwa Spika, kufuatia makubaliano na ahadi za Nchi tajiri, Shirika la Fedha la Kimataifa *(International Monetary Fund (IMF)*, Benki ya Dunia, na Benki ya Maendeleo ya Afrika, Tanzania imefutiwa madeni yote ya zamani. Hata hivyo, taratibu za kuhuisha misamaha hiyo ya madeni zinatofautiana kati ya shirika na shirika. Msamaha wa deni la Benki ya Dunia wa Dola za Kimarekani bilioni 2.8 ulitangazwa rasmi tarehe 1 Julai, 2006 na utakamilika katika muda wa miaka arobaini sawa na muda ambao mikopo inayosamehewa ingelipwa.

Benki ya Maendeleo ya Afrika imeifutia Tanzania deni lenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 750. Unafuu kutokana na msamaha huo utakamilika katika kipindi cha miaka 20 sawa na muda ambao mikopo hiyo ya benki ingelipwa. Kwa upande mwingine, msamaha wa deni la *IMF* la Dola za Kimarekani milioni 336, umetolewa mara moja kwa utaratibu tofauti na ule wa Benki ya Dunia na wa Benki ya Maendeleo ya Afrika. Manufaa ya msamaha wa deni la *IMF* yanaonekana mara moja. Serikali inaendelea na juhudi za kupata misamaha ya madeni kutoka kwa wadai waliobaki, hasa

nchi za Algeria, Brazil, Iraq na Iran, kwa mujibu wa makubaliano yaliyofikiwa katika ngazi ya kimataifa kwamba nchi zinazodai nchi masikini za *HIPC* zifute madeni hayo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti mwaka jana, Serikali ya Marekani kupitia shirika lake la *Millennium Challenge Corporation* iliingiza Tanzania katika kundi la nchi zitakazofaidika na msaada wa *Millennium Challenge Account*. Tangu mwaka 2006 tumepata msaada wa Dola za Kimarekani milioni 11.5 chini ya awamu ya kwanza *(Threshold Programme)* kusaidia kuimarisha taasisi za utawala bora zikiwemo Mahakama, TAKURU, Mamlaka ya Ununuzi wa Umma, vita dhidi ya biashara ya fedha haramu na kadhalika.

Aidha, maandalizi ya awamu ya pili ambayo itakuwa na fedha nyingi zaidi ya mpango wa *MCA (Compact Programme)* yanaendelea vizuri na yanategemewa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka huu wa 2007.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mafanikio yetu katika kutekeleza sera za uchumi mpana, chini ya Mpango wa *PRGF*, uhusiano wetu na Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)* sasa unaratibiwa chini ya mpango mpya ujulikanao kama *Policy Support Instrument (PSI)*.

Mpango huu ulibuniwa na *IMF* mwezi Oktoba 2005 kwa ajili ya nchi zinazoendelea, ambazo zimejenga uwezo wa kubuni na kusimamia sera za uchumi kikamilifu ambazo zina uchumi tulivu *(macroeconomic stability)* na ambazo zina mipango na mikakati ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Nchi zinazojiunga katika *PSI* hazipati tena mikopo toka *IMF*, bali zitaendelea kupata ushauri wa kitaalam kuhusu utekelezaji wa sera sahihi za uchumi mpana. Kupitia mpango huu, tumeendelea kuwa na uhusiano mzuri na *IMF* ambayo kwa upande wake imeendelea kutoa taswira nzuri ya nchi yetu kwa wahisani na wawekezaji wa kimataifa.

Mheshimiwa Spika,kwa kuzingatia kwamba hali ya hewa imekuwa nzuri na uzalishaji wa mazao ya kilimo unatarajiwa kuongezeka, na kwa kuzingatia kwamba umeme sasa unapatikana bila mgao, na viwanda havina tatizo la maji wala umeme, Serikali inaamini kwamba Bajeti yake ya 2006/2007 itakuwa katika kiwango kilichopangwa kwa mwaka mzima. Mapato ya ndani yanategemewa kuvuka lengo la asilimia 14.5 ya Pato la Taifa na kufikia asilimia 15.7 ya Pato la Taifa ifikapo mwisho wa Juni, 2007 na misaada na mikopo ya masharti nafuu kutoka nje inategemewa kufikia lengo.

Mheshimiwa Spika, ingawa kumekuwa na matumizi ya dharura ambayo yametumia fedha kwa njia ya uhamisho wa ndani kama nilivyokwishaeleza, mwelekeo unaonyesha kwamba matumizi ya jumla yatakuwa katika kiwango kilichoidhinishwa kwenye bajeti ya 2006/2007 cha shilingi trilioni 4.850 ifikapo tarehe 30 Juni, 2007.

Mheshimiwa Spika, taarifa kamili kuhusu uhamisho wa ndani uliofanywa mwaka huu wa fedha kukidhi mahitaji ya dharura itawasilishwa katika mkutano huu wa Bunge kwa mujibu wa Sheria *(Re-allocation Warrant)*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio ya uchumi, ukusanyaji wa mapato na katika huduma za jamii, hasa elimu na afya, nchi yetu bado inakabiliwa na changamoto nyingi. Changamoto hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Uchumi wetu unakua kwa kasi ndogo ikilinganishwa na mahitaji na hasa ikizingatiwa kwamba Watanzania tunaongezeka kwa asilimia takriban tatu kwa mwaka. Uchumi ukikua kwa kasi kubwa ndipo mapato ya ndani yanaongezeka na uwezo wa Serikali wa kuwekeza na kutoa huduma muhimu unaongezeka. Uwezo huo hatujaufikia.

(ii) Miundombinu hasa barabara, reli, bandari na umeme ni muhimu katika kukuza uchumi. Lakini fedha zinazohitajika kuibua miundombinu ni nyingi kuliko uwezo wa Serikali. Nitalielezea hili zaidi baadaye, lakini ni changamoto kubwa.

(iii) Ingawa nchi tajiri na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa zinaahidi kuendelea kutusaidia, misaada hiyo itakuwa na faida ya kudumu kama itaelekezwa katika maeneo yanayotuongezea uwezo wa kujitegemea hapo baadaye. Changamoto hapa ni kukubaliana jinsi ya kuwekeza misaada ya Wahisani.

(iv) Mahitaji ya rasilimali kwa ajili ya kutekeleza MKUKUTA, hasa ujenzi wa miundombinu ikijumuisha umeme, barabara, reli, viwanja vya ndege, maji, mawasiliano na kilimo na pia kupanua huduma za jamii hasa elimu na afya na vilevile kustawisha utawala bora, ni makubwa sana ikilinganishwa na rasilimali fedha na rasilimali watu zilizopo.

(v) Kwa kuzingatia ukweli huu, changamoto nyingine kubwa ni kukubaliana kuhusu vipaumbele vitakavyotengewa fedha za Bajeti kwanza na kukubaliana ni maeneo yapi yasubiri. Kupanga ni Kuchagua.

(vi) Wakati umefika sasa kuainisha rasmi maeneo ya uchumi na huduma ya jamii ambayo yataachiwa sekta binafsi ili Serikali ijikite kwenye maeneo machache ya kipaumbele.

(vii) Mahitaji ya fedha za kigeni katika uchumi wetu ni makubwa kuliko uwezo wetu wa kuuza bidhaa na huduma nje. Ni muhimu sana kuweka kipaumbele katika kukuza mauzo nje kama njia muhimu ya kujenga uwezo wetu wa kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya mwaka 2007/08 ni ya pili baada ya uchaguzi Mkuu wa mwezi Desemba, 2005. Bajeti hii inazingatia changamoto nilizozieleza, zikisomwa pamoja na Ilani ya CCM ya Uchaguzi wa mwaka 2005, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) na Malengo ya Milenia ambayo pia yanazingatiwa ndani ya MKUKUTA.

Miongozo hii kwa pamoja imejumuishwa katika Misingi ya Sera za uchumi za mwaka 2007/2008 kama zilivyoelezwa na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, wakati akiwasilisha hotuba yake leo asubuhi. Malengo hayo ya uchumi mpana ni pamoja na:-

(i) Pato halisi la Taifa hukua kwa asilimia 7.3 mwaka 2007, asilimia 7.7 mwaka 2008 na asilimia 7.9 mwaka 2009;

(ii) Mfumuko wa bei usizidi asilimia 4.5 ifikapo Juni 30, 2008;

(iii) Kuongeza mapato ya ndani kutoka shilingi trilioni 2.6 zinazotegemewa mwaka 2006/2007 (asilimia 15.7 ya Pato la Taifa), hadi shilingi trilioni 3.5 mwaka 2007/2008 au asilimia 18.1 ya Pato la Taifa (kwa takwimu zilizopo wakati wa kutayarisha bajeti hii) na shilingi trilioni 4.4 au asilimia 22.6 ya Pato la Taifa mwaka 2009/2010 kwa takwimu za sasa;

(iv) Kudhibiti ongezeko la ujazi wa fedha kwa tafsiri pana ili kuwiana na malengo ya ukuaji wa uchumi na mfumuko wa bei;

(v) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kulipia bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi mitano;

(vi) Bei ya kununua na kuuza fedha za kigeni iendelee kutegemea nguvu ya soko na Benki Kuu ya Tanzania iingilie kati kwa lengo la kuleta utengamano pale inapoonekana soko linayumba. Aidha, usimamizi wa Sheria ya Fedha za Kigeni ya mwaka 1992 *(Foreign Exchange Act, 1992)* uimarishwe hasa katika shughuli za maduka ya fedha za kigeni na taasisi na kampuni zinazodai malipo ya huduma zinazotoa kwa fedha za kigeni; na

(vii) Kuchochea mabadiliko muhimu katika sheria na taratibu za Sekta ya Fedha hasa sekta ndogo ya benki ili kupanua upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi, hasa wajasiriamali wadogo na wa kati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2007/2008 Serikali itaendelea kuweka kipaumbele katika ukusanyaji wa mapato ya ndani. Mambo muhimu yatakayozingatiwa ni pamoja na kupanua wigo wa kodi na kuimarisha zaidi usimamizi wa ukusanyaji wa mapato. Haya yatafanikiwa kutokana na hatua zifuatazo:-

(i) Kuimarisha uchumi tulivu unaokua kwa kasi na kuendelea kuweka mazingira bora ya uwekezaji na biashara ili kuwezesha sekta binafsi kukua na hivyo kupanua wigo wa kodi;

(ii) Kusajili walipa kodi wapya ambao watatokana na mpango wa MKURABITA na mipango mingine ya kuongeza biashara zilizosajiliwa na ajira;

(iii) Kuendelea kutekeleza Mpango wa Pili wa maboresho *(Second Corporate Plan)* wa Mamlaka ya Mapato Tanzania ambao pamoja na mambo mengine, unalenga kuimarisha usimamizi wa kodi na kupanua wigo wa kodi ili kuongeza mapato ya Serikali;

(iv) Kurekebisha viwango vya kodi mbalimbali na taratibu za ukusanyaji ili kuongeza ari ya wananchi kulipa kodi bila kusukumwa na kupunguza gharama ya ukusanyaji wa mapato; na

(v) Kuweka mkakati thabiti wa kukusanya mapato yasiyo ya kodi hasa kutokana na matumizi ya maliasili zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mafanikio makubwa yanayoonekana katika ukusanyaji wa mapato ya ndani na kutokana na hatua hizi nilizozitaja za kuongeza mapato, Serikali inalenga kukusanya mapato ya ndani ya shilingi trilioni 3.5 katika mwaka 2007/2008. Hili ni ongezeko la asilimia zaidi ya 30 ikilinganishwa na matarajio ya ukusanyaji wa mapato mwaka huu wa 2006/2007.

Aidha, kiasi hicho cha mapato ya ndani kitakuwa asilimia 18.1 ya Pato la Taifa kwa takwimu zilizoko wakati wa kuandaa bajeti hii. Aidha, Serikali inategemea kupata shilingi bilioni 15 kutokana na mauzo ya asilimia 21 ya hisa zake katika *NMB*. Maelezo zaidi kuhusu mapato ya ndani nitayatoa hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ahadi za nchi Wahisani na makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa, Serikali inategemea kupata misaada na mikopo ya masharti nafuu ya jumla ya shilingi bilioni trilioni 2.5 katika mwaka 2007/2008.

Kiasi hicho cha misaada na mikopo ya nje kinajumuisha shilingi bilioni 881.320 ambazo zitatolewa moja kwa moja kupitia Bajeti ya Serikali *(General Budget Support)*, shilingi bilioni 273.194 ambazo zitatolewa kupitia mifuko *(basket funds)* ya programu mbalimbali za kisekta, shilingi trilioni 1.189 ambazo zitatolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 206.037 kutokana na misamaha ya madeni.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mapato ya ndani ya shilingi trilioni 3.5, mauzo ya hisa katika *NMB* shilingi bilioni 15.0 na misaada na mikopo ya nje ikiwemo misamaha ya madeni ya shilingi trilioni 2.549, uwezo wa Serikali katika bajeti ya 2007/2008 ni shilingi trilioni 6.0668. Kiasi hicho ni ongezeko la asilimia 25 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2006/07 inayofikia mwisho tarehe 30 Juni, 2007 na ni asilimia 31 ya Pato la Taifa, kwa takwimu za sasa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2007/2008, Serikali haitakopa kwa ajili ya kuziba pengo la Bajeti kutoka soko la fedha la ndani kupitia Dhamana na Hati Fungani za Serikali.

Hata hivyo, ili kulisaidia soko hilo kukua, Dhamana na Hati Fungani za Serikali zitaendelea kutumika katika soko hili ili kulipia zile zinazoiva *(rollover)* na kusaidia kudhibiti ujazi wa fedha. Kamati maalum imeteuliwa na kitengo maalum kimeanzishwa *(Cash Management Unit)* ambacho kitafuatilia kwa karibu mzunguko wa fedha za Serikali na soko la dhamana za Serikali *(Treasury Management).* Hatua hii itasaidia kupunguza riba za dhamana za Serikali katika soko la fedha.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya 2007/2008 imezingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Ilani ya Chama Tawala ya Uchaguzi wa 2005, MKUKUTA na miongozo mingine ya Kitaifa ya kuleta maendeleo kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele hivi vimezingatia pia maoni ya Waheshimiwa Wabunge waliyoyatoa wakati wa mkutano kuhusu Mwongozo wa Bajeti uliofanyika mwezi Aprili, 2007, pamoja na Changamoto nilizozieleza hapo awali.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya 2007/2008 imezingatia mambo makuu ambayo yameainishwa katika mpango wa mwaka wa pili wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Mambo hayo ni pamoja na haya yafuatayo:-

(i) Kuimarisha miundombinu muhimu ya kitaifa ambayo ni kichocheo cha kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi;

(ii) Kuimarisha Sekta ya kilimo, ikiwemo mipango ya maendeleo ya kilimo ya Wilaya, kama vile miradi ya umwagiliaji, utafiti, ukuzaji wa teknolojia na ruzuku ya mbegu na pembejeo za kilimo;

(iii) Kuwezesha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa nyumba za walimu hasa katika maeneo yenye mazingira magumu na ununuzi wa zana za kufundishia na kujifunzia;

(iv) Kuboresha maslahi ya watumishi wa umma na kuwezesha ajira katika sekta za huduma muhimu zikiwemo Elimu na Afya;

(v) Kutekeleza mradi wa vitambulisho vya Taifa vya Uraia;

(vi) Kukarabati hospitali za mikoa, zahanati na vituo vya afya; na

(vii) Kuhamasisha na kuwasaidia wananchi kuunda *SACCOS* za makundi mbalimbali ya jamii ambazo zitawezesha wajasiriamali ama mmoja mmoja au vikundi kupata mikopo ya benki mikoani kote nchini, kuendeleza miradi yao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, maeneo yote matatu ya MKUKUTA yamezingatiwa kulingana na uwezo wa bajeti. Maeneo hayo ni:-

(i) Kukuza uchumi na kuondoa umaskini wa kipato;

(ii) Kuboresha hali za maisha ya watu na huduma ya jamii; na

(iii) Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, kimsingi bajeti hii inazingatia umuhimu wa kuongeza rasilimali kwa ajili ya kukuza uchumi kama msingi wa mkakati endelevu wa kupiga vita umaskini. Zoezi la kukokotoa mahitaji ya rasilimali (fedha na watu) zinazohitajika kutekeleza MKUKUTA bado linaendelea.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, viko viashiria muhimu vinavyoonyesha kwamba fedha na rasilimali nyingine zinazohitajika ili kutekeleza MKUKUTA ni nyingi na kwa vyovyote vile Serikali haiwezi kupata uwezo wa kutosha kukidhi mahitaji hayo kwa njia ya mapato ya ndani pekee.

Kwa hali hii, utekelezaji wa MKUKUTA unahitaji ushirikiano wa karibu kati ya Sekta ya Umma, Sekta binafsi, Jumuiya za Wananchi, Nchi Wahisani na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, viashiria vinavyoonyesha gharama za kutekeleza MKUKUTA ni pamoja na hivi vifuatavyo:-

(i) Mpango wa Uwekezaji wa Sekta ya Usafirishaji, inayojumuisha barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege na kadhalika unaonyesha mahitaji ya zaidi ya dola za Kimarekani bilioni tano (5bl) sawa na shilingi trilioni 6.4 katika kipindi cha miaka 10 au shilingi bilioni 640 kwa mwaka.

(ii) Mpango wa ukarabati wa njia za kusambaza umeme na kuimarisha hali ya fedha ya *TANESCO*, unahitaji dola za Kimarekani bilioni 1.3 au shilingi trilioni 1.6, katika kipindi cha miaka mitano au shilingi bilioni 320.0 kwa mwaka.

(iii) Mpango wa Afya ya Msingi kwa ajili ya kufikia malengo ya Milenia unahitaji dola za Kimarekani bilioni 15 au shilingi trilioni 19.5 katika muda wa miaka mitano (5) au shilingi trilioni 3.9 kwa mwaka.

(iv) Mpango wa kuimarisha huduma za Ugani unahitaji shilingi bilioni 193 kwa miaka mitatu au shilingi bilioni 64 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, mahitaji yaliyowasilishwa na Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Halmashauri kwa ajili ya bajeti ya 2007/2008 ni zaidi ya shilingi trilioni 12. Hiki pia ni kigezo cha kukadiria mahitaji ya fedha kwa ajili ya kutekeleza MKUKUTA. Kiasi hiki ni mara mbili ya uwezo ulioko wa mapato ya ndani na misaada ya nje kwa pamoja.

Kwa hali hii, hatuwezi kukwepa kupanga vipaumbele kwa makini sana na hatuwezi kujidanganya kwamba mapato ya ndani pekee yanaweza kutosha kutekeleza MKUKUTA bila misaada ya nje na bila ushiriki wa dhati wa sekta binafsi.

Ni vizuri ieleweke pia kwamba Mashirika ya Maendeleo kama Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika yalianzishwa kwa madhumuni ya kutoa mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hivyo kukopa kutoka kwenye mashirika haya sio utegemezi.

Mheshimiwa Spika, hakuna nchi au kampuni kokote duniani iliyoendelea kihalali bila kukopa. Sehemu kubwa ya fedha za nje katika bajeti hii ni mikopo ya masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Kupata misaada kutoka Nchi marafiki pia sio jambo baya mradi misaada hiyo tuielekeze kwenye maeneo yatakayotuongezea uwezo wetu wenyewe wa kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji, Bajeti ya mwaka 2007/2008 itaendeleza juhudi za Serikali za kuwaongezea uwezo wananchi kwa kujiletea maendeleo yao wenyewe. Ili kufanikisha azma hii, mambo yafuatayo yamezingatiwa:-

(i) Kwanza, kuharakisha utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mageuzi ya sekta ya fedha ambayo itawezesha wananchi wengi zaidi kupata mikopo ya uzalishaji, biashara, na pia mikopo ya nyumba, mikopo ya mali za kukodi na kuboresha mifuko ya pensheni na hifadhi ya jamii. *(Makofi)*

(ii) Pili, Serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri ya kujenga tabia ya kujiwekea akiba miongoni mwa wananchi kwa kuwahamasisha na kuwasaidia wananchi kuunda *SACCOS* za makundi mbalimbali ya wajasiriamali ambazo zitawezesha mtu mmoja mmoja au makundi ya watu kupata mikopo kutoka katika mabenki mikoani kote nchini. *(Makofi)*

(iii) Tatu, mifuko ya dhamana za mikopo inayosimamiwa na Benki Kuu itaendelea kuimarishwa ili itoe dhamana kwa wajasiriamali wengi zaidi. *(Makofi)*

(iv) Nne, Benki ya Rasilimali *(TIB)* itaimarishwa kwa kuongezewa mtaji ili iweze kutekeleza majukumu yake ya sasa kama Benki ya Maendeleo hatua kwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupeleka madaraka kwa wananchi *(D by D)*, Serikali imedhamiria kuongeza kasi ya kupeleka madaraka kwa wananchi kupitia Serikali za Mitaa *(D by D).* Uchambuzi uliofanywa umebainisha kuwa baadhi ya kazi zinazofanywa na Serikali Kuu zinaweza zikatekelezwa vizuri na wananchi watafaidika zaidi kama zikihamishiwa katika Halmashauri. Kwa kuanzia, Bajeti ya mwaka 2007/2008 inajumuisha uhamisho wa baadhi ya majukumu pamoja na rasilimali fedha na rasilimali watu na vitendea kazi kutoka Wizara tano za Serikali Kuu kwenda kwenye Halmashauri.

Wizara zitakazohusika ni Wizara za Afya na Ustawi wa Jamii; Elimu na Mafunzo ya Ufundi; Kilimo, Chakula na Ushirika; Maji; na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI. Aidha, Serikali itaendelea kujenga uwezo wa Halmashauri wa kuandaa, kusimamia na

kudhibiti matumizi ya fedha za umma. Katika kuimarisha usimamizi wa Bajeti ya Serikali, hatua mbalimbali za kiutendaji zitachukuliwa kuboresha taratibu za kusimamia utekelezaji wa Bajeti na kudhibiti matumizi. Lengo ni kuongeza ufanisi, uwazi na uwajibikaji kwa walipakodi na wananchi kwa ujumla. Serikali Kuu itaendelea kuajiri Wahasibu na Wakaguzi wa Ndani kwa ajili ya Halmashauri na itaendelea kutoa mafunzo kama zoezi la kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Bajeti inayopendekezwa imezingatia mambo yafuatayo:-

(i) Kipaumbele kimewekwa katika kukamilisha kwanza miradi na programu zinazoendelea, hasa katika sekta ya miundombinu na maji. *(Makofi)*

(ii) Mgao wa fedha za Bajeti ya mwaka 2007/2008 umezingatia mfumo wa MKUKUTA ambao unalenga katika maeneo makuu *(Clusters)* badala ya mfumo wa kisekta. Hata ikitazamwa kwa mfumo wa kisekta, ni muhimu kuangalia maeneo yote ya sekta, badala ya mtazamo wa Kiwizara. Kwa mfano Sekta ya Kilimo kwa tafsiri pana imetengewa shilingi bilioni 379.578 mwaka 2007/2008, na inajumuisha Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; Idara ya Masoko ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko; Barabara za vijijini chini ya TAMISEMI, Maendeleo ya Mifugo, Halmashauri za Wilaya na kadhalika. Kwa tafsiri hii kilimo kimetengewa asilimia 6.2 ya Bajeti ya mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, sekta ya miundombinu kwa tafsiri pana inajumuisha mambo yaliyopo katika Fungu 98 la Wizara ya Miundombinu, ambalo ni pamoja na fedha za matengenezo ya barabara chini ya Bodi ya Mfuko wa Barabara, Fungu 56 (TAMISEMI) na Halmashauri za Wilaya ambazo pia zimetengewa fedha za miundombinu vijijini. Kwa tafsiri hii, miundombinu imetengewa jumla ya shilingi bilioni 777.2, pamoja na marekebisho yaliyofanywa kuzingatia ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kupitia Kamati za Bunge. *(Makofi)*

Kwa tafsiri hii pana, maeneo yaliyopewa kipaumbele katika Bajeti ya mwaka 2007/2008 ni pamoja na:-

(1) Elimu, shilingi bilioni 1,086.1 (trilioni 1.086) sawa na asilimia 18 ya Bajeti. *(Makofi)*

(2) Miundombinu, shilingi bilioni 777.2 sawa na asilimia 12.8 ya Bajeti. *(Makofi)*
(3) Afya, shilingi bilioni 589.9 sawa na asilimia 10.0 ya Bajeti. *(Makofi)*

(4) Kilimo, shilingi bilioni 379 sawa na asilimia 6.2 ya Bajeti. *(Makofi)*

(5) Maji, shilingi bilioni 309.1 sawa na asilimia 5.1 ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo mengine ambayo yamezingatiwa katika Bajeti ya mwaka 2007/2008 ni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu wa huduma ya pensheni, kwa muda mrefu, huduma kwa wastaafu wa Serikali wanaolipwa pensheni na Hazina imekuwa ikilalamikiwa na wananchi, Wabunge na wadau wengine. Utafiti uliofanywa na Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Mifuko ya Pensheni, umebaini kwamba malalamiko ya wastaafu yametokana na sababu nyingi, baadhi zikiwa ndani ya uwezo wa Wizara na nyingine zikiwa nje ya uwezo wa Wizara ya Fedha.

Kwa mujibu wa makubaliano yaliyofikiwa kati ya Serikali na Mifuko ya Pensheni na Hifadhi ya Jamii, wastaafu wote ambao sasa wanalipwa malipo ya uzeeni na Wizara ya Fedha, watahamishiwa katika mifuko ya Pensheni ya *NSSF*, *PSPF*, *PPF* na *GEPF*. Zoezi la kuwahamisha litatekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2007/2008. Hatua hii itaondoa kero wanazopata wastaafu hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Bunge *(National Assembly Fund)*, kuanzia sasa, Fungu la 42 la Bajeti linaitwa Mfuko wa Bunge ambao utasimamiwa moja kwa moja na Katibu wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo *(Constituency Development Fund)*, suala la kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo litawasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati akiwasilisha mapendekezo yake Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mishahara, Serikali imepokea mapendekezo ya Tume ya Rais kuhusu kuboresha maslahi ya Watumishi wa Umma. Uchambuzi wa mapendekezo hayo unaendelea. Serikali itatekeleza mapendekezo ya Tume kwa awamu, kuanzia Bajeti ya mwaka 2007/2008. Aidha, Serikali imezingatia mahitaji ya kuongeza ajira hasa katika sekta za elimu na afya. Maelezo zaidi yatatolewa na Waziri wa Utumishi pamoja na Mawaziri wa Sekta hizo mbili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vitambulisho vya Taifa vya Uraia, zoezi la kutengeneza vitambulisho vya Taifa ili kila mwananchi wa Tanzania awe na kitambulisho linaendelea. Jengo kwa ajili ya ofisi ya Mratibu wa mradi limepatikana na Bajeti ya mwaka 2007/2008 imetenga fedha kwa ajili ya ajira ya watendaji, ununuzi wa vitendea kazi na ukarabati wa jengo hilo. Mradi huu unaratibiwa na Idara ya Uhamiaji. Vitambulisho vya Uraia ni nyenzo muhimu sana katika ukusanyaji wa mapato, upatikanaji wa mikopo ya benki, vita dhidi ya uhalifu, kujenga demokrasia na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mgao wa fedha kwa Serikali ya Mapinduzi, kama nilivyosema awali, Tume ya Fedha ya Pamoja imewasilisha mapendekezo yake Serikalini na mchakato wa kufikia maamuzi kuhusu mapendekezo hayo bado unaendelea. Kwa hivyo, Bajeti ya mwaka 2007/2008 imetenga fedha za mgao kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa utaratibu wa asilimia 4.5 ya misaada ya nje ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo mengine muhimu yaliyozingatiwa katika Bajeti hii ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Ukarabati wa hospitali za mikoa;

(ii) Kuendelea kuimarisha taaluma ya uhasibu na ukaguzi wa ndani katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa;

(iii) Kuimarisha ukaguzi wa ununuzi wa umma na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Bajeti;

(iv) Ukarabati wa Ofisi za Wakuu wa Wilaya;

(v) Mahitaji ya Wilaya na Halmashauri mpya;

(vi) Mradi wa mabasi yaendayo kasi jijini Dar es Salaam;

(vii) Mikoa imeongezewa fedha mara mbili kulinganisha na mwaka 2006/2007; na

(viii) Zoezi la *"D by D"* linahamisha fedha kiasi cha shilingi bilioni 286 kutoka Serikali Kuu kwenda kwenye Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya mfumo wa kodi, ada, tozo na hatua nyingine za mapato, Mamlaka ya Mapato Tanzania inaendelea kuimarisha usimamizi wa kodi na mapato mengine yanayokusanywa na Mamlaka hiyo. Serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya mfumo na viwango vya baadhi ya kodi katika maeneo kadhaa ili kurahisisha ukusanyaji na kuhamasisha wananchi kulipa kodi kwa hiari, na pia kuongeza mapato kwa ajili ya matengenezo ya barabara, na kwa ajili ya mfuko wa umeme vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inapendekeza kurekebisha baadhi ya viwango vya kodi na tozo nyingine zisizo za kodi chini ya Sheria mbali mbali za kodi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, inapendekezwa kufanya marekebisho yafuatayo:-

(i) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mitungi ya kuzimia moto ili kupunguza gharama na kuhamasisha matumizi ya vifaa hivyo katika kupambana na majanga ya moto. *(Makofi)*

(ii) Kuondoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye nyuzi ghafi zinazotengenezwa nchini ili kuwawezesha wazalishaji kurejeshewa *VAT* wanayolipa kwenye malighafi na huduma kama umeme, dawa na kadhalika na hivyo kuwaongezea uwezo wa ushindani. *(Makofi)*

(iii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye *pampers* na mifuko ya usafi kwa matumizi ya tiba.

(iv) Kufanya marekebisho katika aya ya nne ya jedwali la tatu la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili unafuu unaotolewa kwa shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini uhusishe pia shughuli za utafutaji wa gesi na mafuta ya petroli. Hatua hizi katika Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa pamoja zinakadiriwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 400.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato inapendekezwa kupunguza kiwango cha chini cha kukokotoa kodi ya mapato ya ajira kutoka asilimia 18.5 hadi asilimia 15 ili kupunguza mzigo wa kodi kwa wafanyakazi wa kipato cha chini. Hatua hii ambayo itaongeza kipato halisi cha wafanyakazi, itapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shillingi bilioni 1.809.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria ya ushuru wa bidhaa, inapendekezwa kufanya marekebisho yafuatayo:-

(i) Kuondoa sharti la kuweka alama ya *for export only* katika bidhaa zinazouzwa nje ya nchi. Sharti hili limeonekana kukwamisha juhudi za kuongeza mauzo nje badala ya kuhamasisha.

(ii) Kurasimisha ndani ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, utaratibu wa kuirejeshea Serikali ya Mapinduzi Zanzibar makusanyo ya ushuru kwa bidhaa zinazozalishwa Bara na kuuzwa au kutumika Zanzibar.

(iii) Kurekebisha kwa asilimia 7, viwango vya Ushuru wa Bidhaa kwa bidhaa zinazotozwa ushuru huo. Kiwango hiki cha asilimia 7 kinakaribia kiwango cha mfumuko wa bei.

Aidha, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa imetaja kwamba ushuru huo utaongezwa kila mwaka kwa kiwango cha mfumuko wa bei ili kulinda thamani halisi ya mapato ya Serikali kutoka kwenye vyanzo hivi. Viwango vinavyopendekezwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Vinywaji baridi kutoka shilingi 45 kwa lita hadi shilingi 48 kwa lita. *(Makofi)*

(ii) Bia inayotengenezwa kwa nafaka ya hapa nchini na ambayo haijaoteshwa kutoka shilingi 161 kwa lita hadi shilingi 173 kwa lita. *(Makofi)*

(iii) Bia nyingine zote kutoka shilingi 274 kwa lita hadi shilingi 294 kwa lita.*(Makofi)*

(iv) Mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 25 kutoka shilingi 878 kwa lita hadi shilingi 940 kwa lita. *(Makofi)*

(v) Vinywaji vikali kutoka shilingi 1,302 kwa lita hadi shilingi 1,394 kwa lita. *(Makofi)*

(vi) Kurekebisha viwango vya Ushuru wa Bidhaa kwenye bidhaa za mafuta ya petroli kama ifuatavyo:-

(a) Petroli *(MSP* na *MSR)* kutoka shilingi 315 kwa lita hadi shilingi 337 kwa lita.

(b) Diseli *(GO)* kutoka shilingi 292 kwa lita hadi shilingi 312 kwa lita.

(c) Mafuta ya taa *(IK)* kutoka shilingi 52 kwa lita hadi shilingi 56 kwa lita.

(d) Mafuta mazito ya mitambo *(HFO)* kutoka shilingi 109 kwa lita hadi shilingi 117 kwa lita.

(e) Dizeli nzito ya kuendeshea mitambo viwandani *(IDO)* kutoka shilingi 366 kwa lita hadi shilingi 392 kwa lita.

(vii) Kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye sigara kama ifuatavyo:-

(a) Sigara zisizo na kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 4,462 hadi shilingi 4,775 kwa sigara elfu moja. *(Makofi)*

(b) Sigara zenye kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 10,529 hadi shilingi 11,266 kwa sigara elfu moja. *(Makofi)*

(c) Sigara nyingine zenye sifa tofauti na (a) na (b) kutoka shilingi 19,195 hadi shilingi 20,460 kwa sigara elfu moja. *(Makofi)*

(d) Tumbaku ambayo iko tayari kutengeneza sigara *(cut filler)* kutoka shilingi 9,657 hadi shilingi 10,333 kwa kilo; na

(e) Ushuru wa bidhaa kwa *Cigar* unabaki kuwa asilimia 30.

Kwa pamoja, hatua hizi katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa zinakadiriwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shillingi bilioni 34.446.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Barabara kwenye Mafuta ya Petroli, ili kuongeza uwezo wa Mfuko wa Barabara kumudu ongezeko la gharama za matengenezo ya barabara, Serikali inapendekeza kuongeza ushuru wa mafuta ya petroli kutoka shilingi 100/= za sasa kwa lita hadi shilingi 200/= kwa lita. *(Makofi)*

Aidha, Serikali inapendekeza kubadili mfumo wa kutoza ada ya mwaka ya leseni za magari kutoka kiwango kimoja cha shilingi 20,000 kwa gari na kuwa na viwango vitatu kulingana na ujazo wa injini kama ifuatavyo:-

(i) Kwa magari yenye ujazo wa injini usiozidi 1,500cc kiwango cha ada kitakuwa shilingi 80,000 kwa mwaka. *(Makofi)*

(ii) Kwa magari yenye ujazo wa injini unoazidi 1,500cc lakini hauzidi 5,000cc kiwango cha ada kitakuwa shilingi 230,000 kwa mwaka.

(iii) Kwa magari yenye ujazo wa injini unaozidi 5,000cc kiwango cha ada kitakuwa shilingi 100,000 kwa mwaka. Haya ni magari ya mizigo na mabasi ya abiria. Hatua hizi kwa pamoja zinakadariwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 169.737. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Naomba utulivu Bungeni. Tuendelee kusikiliza.

**WAZIRI WA FEDHA:**Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, katika kikao cha maandalizi ya Bajeti cha Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(Pre - Budget)* kilichofanyika tarehe 31 Mei, 2007 mjini Arusha, kilipendekeza marekebisho ya viwango vya Ushuru wa Forodha katika mwaka wa fedha wa 2007/2008. Mapendekezo hayo yalipitishwa na Kamati ya Kisekta ya Mawaziri wa Biashara, Fedha na Uwekezaji wa Jumuiya kama ifuatavyo:-

(i) Tanzania itoze kwa muda ushuru wa forodha katika kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 25 kwa mabasi yatakayoingizwa kwa ajili ya mradi wa mabasi yaendayo kasi jijini Dar es Salaam.

(ii) Tanzania itoze kwa muda kiwango cha asilimia 10 kwenye dawa za binadamu zinazotoka nje ya nchi isipokuwa dawa za kurefusha maisha ya wenye virusi vya UKIMWI, dawa za kutibu Malaria na Kifua Kikuu, pamoja na dawa zinazonunuliwa na Serikali.

(iii) Kupunguza kiwango cha Ushuru wa Forodha kwenye malighafi za kutengenezea uchujio *(filter)* za magari zilizo chini ya *HSCODE* 4805.50.00 kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 ili kupunguza gharama za uzalishaji ndani ya Jumuiya.

(iv) Kupunguza kiwango cha Ushuru wa Forodha kwenye malighafi za kutengenezea makaratasi zilizo chini ya *HSCODE* 5911.32.00, kutoka asilimia 10 hadi asilimia sifuri ili kupunguza gharama za uzalishaji ndani ya Jumuiya.

(v) Kupunguza kiwango cha Ushuru wa Forodha kwenye malighafi za kutengeneza bidhaa za karatasi zilizo chini ya *HSCODE* 6804.10.00 kutoka asilimia 25 hadi asilimia sifuri.

(vi) Kusamehe Ushuru wa Forodha kwenye *bulb* maalumu zinazotumia umeme kidogo.

(vii) Kusamehe Ushuru wa Forodha kwenye malighafi za kutengeneza vifaa vinavyotumia nguvu ya jua. *(Makofi)*

(viii) Kusamehe Ushuru wa Forodha kwenye vifaa vya hospitali zilizosajiliwa. *(Makofi)*

(ix) Tanzania kuongezewa muda wa kutumia kiwango cha asilimia 10 cha ushuru wa forodha kwenye ngano badala ya kiwango cha asilimia 35% kwa miaka miwili zaidi hadi Juni 2009.

(x) Kupunguza kiwango cha Ushuru wa Forodha kwenye bidhaa zilizo chini ya *HSCODE* 7415 kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10.

(xi) Kuondoa Ushuru wa Forodha kwenye malighafi za kutengeneza chaki za shule.

(xii) Kupunguza kiwango cha Ushuru wa Forodha kwenye simu za mezani zisizo na waya na simu za mikononi zilizo chini ya *HSCODE* 8517.11.00 na 8517.12.00 kutoka asilimia 10 hadi asilimia sifuri ili kuhamasisha maendeleo ya teknolojia katika sekta ya mawasiliano ya simu. *(Makofi)*

Hatua hizi katika ushuru wa forodha kwa pamoja zinakadiriwa kuongeza mapato ya Serikali kwa shilingi bilioni 2.772.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi za Ushuru wa Forodha zitatangazwa katika Gazeti la Jumuiya ya Afrika Mashariki kabla ya tarehe 1 Julai, 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapato yasiyo ya Kodi, inapendekezwa kuongeza viwango vya ada na tozo mbalimbali zinazokusanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii ili viendane na wakati, pia ili kulinda maliasili yetu na kuongeza mapato ya Serikali. Hatua hii inakadiriwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 33.616. Muda wa Kodi mpya kutumika, Hatua hizi mpya za kodi zitaanza kutumika Julai Mosi 2007, isipokuwa pale ilipoelezwa vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na marekebisho ya ushuru wa forodha ambayo mengi yanalenga kupunguza gharama za uzalishaji viwandani katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashiriki, yako malalamiko mengi kuhusu ucheleweshaji wa kutoa mizigo katika bandari ya Dar es Salaam. Uchambuzi umebaini kwamba tatizo hili linachangiwa pia na idadi kubwa ya taasisi zinazosimamia uingizaji wa bidhaa nchini. Wadau wa bandari wamekuwa wakishauriana kuhusu namna ya kuhuisha taratibu zao ili kumaliza tatizo hili. Kwa upande wake, Mamlaka ya Mapato Tanzania, imechukua hatua thabiti kuanzia tarehe 1 Juni, 2007 kama sehemu ya ufumbuzi wa tatizo hilo. Hatua hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(ii) Umeanzishwa utaratibu wa kupitisha moja kwa moja *(fast tracking)* bila ukaguzi bidhaa zote zinazoagizwa na wafanyabiashara ambao tayari wameainishwa kama wawajibikaji wazuri katika kulipa kodi *(compliant traders). (Makofi)*

**SPIKA:** *Order, Order, please!* Utulivu.

**WAZIRI WA FEDHA:** (ii) Kiwango cha bidhaa zinazopitishwa kwenye milango mekundu *(red channels)* kimepunguzwa kutoka asilimia 80 kama ifuatavyo:-

(a) Asilimia 40 ya bidhaa zitapitishwa kwenye milango ya kijani na kuondoshwa bandarini moja kwa moja.

(b) Asilimia 40 ya bidhaa zitafanyiwa ukaguzi wa kawaida bila upekuzi *(normal risk assessment).* Zitafuatiwa na ukaguzi wa kina *(post clearance audits)* baada ya kuondolewa bandarini.

(c) Asilimia 20 tu ya bidhaa ndizo zitakazofanyiwa upekuzi kabla ya kuondolewa bandarini. *(Makofi)*

(iii) Asilimia 75 ya bidhaa zote zinazoingizwa na wawekezaji waliosajiliwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)* zitapitishwa moja kwa moja katika milango ya kijani. Asilimia 25 ya bidhaa hizo zitafanyiwa ukaguzi wa kawaida, ukifuatiwa na ukaguzi wa kina *(post clearance audit)* baada ya kuondolewa bandarini.

(iv) Magari mapya na yale yaliyotumika kwa kipindi kisichozidi miaka mitano hayatapitishwa kwenye *red channel* kama ilivyokuwa awali.

(v) Bidhaa maalumu zinazohitaji vibali kutoka Idara mbalimbali za Serikali zitafanyiwa ukaguzi wa nyaraka pekee *(documentary checks)* badala ya upekuzi kamili wa bidhaa zenyewe *(full offload)* ili kuharakisha uondoshaji bandarini wa bidhaa hizo.

(vi) Mamlaka itatoa uamuzi katika muda wa saa 24 ili kuondoa bandarini bidhaa zote zilizoagizwa kwa kutumia thamani zilizobainishwa kwenye kadhia na mwagizaji, ambazo bei zake *(transaction data base)* hazitapatikana muda huo.

Mheshimiwa Spika, mapato yanayokadiriwa kupatikana kutokana na hatua mpya za mapato yanaonyeshwa katika muhtasari hapa chini:-

(i) Kodi ya Ongezeko la Thamani shilingi bilioni 0.400;
(ii) Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 shilingi bilioni 1.809;
(iii) Ushuru wa Bidhaa shilingi bilioni 34.446;
(iv) Ushuru wa Forodha shilingi bilioni 2.772;
(v) Ada ya mwaka ya leseni za magari shilingi bilioni 60.500;
(vi) Ushuru wa Barabara shilingi bilioni 109.237;
(vii) Mapato yasiyo kodi shilingi bilioni 33.616.

Mheshimiwa Spika, jumla ni shilingi bilioni 239.161

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelezo hayo, sura ya Bajeti ya mwaka 2007/2008 inakuwa kama ifuatavyo:-

| **Mapato** | | **Shilingi bilioni** |
|---|---|---|
| A. Mapato ya Ndani | | 3,502.583 |
| (i) Mapato ya Kodi *(TRA)* | 3,237.096 | |
| (ii) Mapato ya siyo ya Kodi | 265.487 | |
| B. Mikopo na Misaada ya Nje Ikijumuisha *HIPC/MDRI* | | 2,549.249 |
| C. Mauzo ya Hisa za Serikali | | 15.000 |
| **Jumla ya Mapato yote** | | **6,066.832** |
| **Matumizi** | | |
| D. Matumizi ya Kawaida | | 3,865.736 |
| (i) Mfuko Mkuu/CFS | 615.039 | |
| (ii) Wizara | 2,357.587 | |
| (iii) Mikoa | 83.059 | |
| (iv) Halmashauri | 810.051 | |
| E. Matumizi ya Maendeleo | | 2,201.096 |
| (a) Fedha za Ndani | 739.204 | |
| (b) Fedha za Nje | 1,461.892 | |
| **Jumla ya Matumizi yote** | | **6,066.832** |

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali, majadiliano kati ya Serikali ya Tanzania na Shirika la *Millenuim Challenge Corporation* la Serikali ya Marekani yanaendelea vizuri na kuna uwezekano mkubwa kwamba mkataba wa kupatiwa fedha chini ya *Compact Programme* ya *MCC* utasainiwa kabla ya mwisho wa mwezi Desemba, 2007. Kwa msingi wa makubaliano yaliyofikiwa hadi sasa, miradi itakayofaidika na programu hii ni pamoja na barabara, umeme na maji. Kwa kuwa majadiliano hayo hayajakamilika na mkataba haujasainiwa, Bajeti hii ninayowasilisha leo haijaingiza programu ya *MCC*. Serikali inakusudia kuomba kibali cha Bunge cha kuingiza fedha za *MCC* katika Bajeti hii kwa njia ya *Supplementary Budget* kwa mujibu wa sheria mara tu mkataba husika utakaposainiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kurejea, Bajeti ya mwaka 2007/2008 imezingatia azma ya Serikali ya kutekeleza:-

(i) Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005;

(ii) Dira ya Maendeleo ya Taifa hadi mwaka 2025;

(iii) Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA);

(iv) Malengo ya Milenia; na

(v) Sera za Kijumla za Uchumi kwa mwaka 2007/2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2007/2008 Serikali imeongeza fedha katika maeneo makuu ya kipaumbele ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa MKUKUTA na Ilani ya Uchaguzi wa mwaka 2005.

Aidha, Bajeti imezingatia umuhimu wa kuongeza uwekezaji katika maeneo ya kukuza uchumi, kama msingi wa mkakati endelevu wa kuongeza pato la kila mwananchi. Ili kuongeza kasi ya kupunguza umaskini wa kipato na kuimarisha huduma endelevu za jamii zikiwemo elimu na afya, kiwango cha ukuaji wa uchumi kinatakiwa kiwe endelevu.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika elimu, miundombinu, kilimo na nishati, katika ngazi zote hauna budi kupewa kipaumbele ili uwe chachu ya kukua kwa uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne, imedhamiria kuweka misingi imara ya kujenga uwezo wa nchi yetu kukusanya nguvu zetu hasa katika kukusanya mapato ya ndani. Uwezo unaotakiwa ni pamoja na kutumia misaada tunayopata kutoka nje, kuwekeza kwenye maeneo ambayo yatatuongezea uwezo wa kujitegemea.

Hivyo basi, hatuna budi kila mmoja wetu na kwa pamoja kuongeza ubunifu katika uzalishaji wenye tija utakaoongeza Pato la Taifa na hatimaye kuondokana na umasikini. Aidha, ni muhimu kwa kila mmoja wetu kuzingatia suala la utawala bora na uwajibikaji katika kuboresha hali za maisha ya wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya fedha kwa ajili ya kutekeleza MKUKUTA ni makubwa kuliko uwezo wa Serikali. Sekta binafsi ina nafasi nzuri sana ya kuchangia katika utekelezaji wa MKUKUTA. Serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri kwa sekta binafsi ili iweze kutoa mchango wake, hasa kwa njia ya ajira, mauzo ya nje na mapato ya Serikali. Sekta ndogo ya benki ambayo inakusanya akiba za wananchi na wafanyabiashara wa hapa nchini ina nafasi nzuri sana ya kutoa mchango wake katika kutekeleza MKUKUTA kwa kuongeza mikopo kwa wajasiriamali ambao ni sehemu ya sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, changamoto mbele yetu ni nyingi na ni kubwa, lakini tunaweza kuzishinda kama sote tutaamua kutimiza wajibu wetu, *It can be done, play your part.* Naamini inawezekana kama kila mtu akitimiza wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika**,** naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.*(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu nina hakika mtapenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa hotuba ambayo imekuwa na mpangilio mzuri sana. Kuhusu maudhui, hayo ninyi ni juu yenu, mtajadili wiki ijayo. Mimi nasema tu ni hotuba nzuri kwa mpangilio wake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mkutano wetu huu baada ya kupokea hizi hotuba mbili siku ya Jumatatu tarehe 18 Juni, 2007 ndiyo utaanza mjadala. Kwa hiyo, hakuna shughuli yoyote ya Bunge, kama mlivyoona mambo yenyewe haya ni mazito sana yanahitaji muda wa kutafakari. Tarakimu hizi mzisome vizuri ili kama kawaida yetu mjadala uwe mzuri na wa kujitahidi kujenga nchi yetu tunayoipenda. Kwa hiyo, yale ambayo yalikuwemo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na haya ambayo tumeyasikia hivi punde ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha yatajadiliwa kwa siku takriban tano, yaani Jumatatu hadi Ijumaa tarehe 22 Juni, 2007 wiki ijayo na ndiyo atahitimisha na baada ya hapo tutakuwa na fursa ya kumsikiliza Mheshimiwa Waziri Mkuu kuanzia Jumatatu tarehe 25 Juni hadi Ijumaa tarehe 29 Juni, 2007. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ni dhahiri wiki mbili hizi ni za hotuba muhimu sana, natarajia Waheshimiwa Wabunge wote tutakuwepo ili tuweze kuchangia. Kwa kiasi kikubwa tutakavyoweza kuchangia katika wiki mbili hizi, itarahisisha kazi tunapoingia katika sekta baada ya hapo. *(Makofi)*

Wale walio na wasiwasi wa mambo ya mishahara yao na kadhalika, niwatoe wasiwasi kwamba hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itakuja mapema tu ili hatma ya mishahara iweze kujulikana na mipangilio ifanywe ili kuweza kupata kuanzia tarehe 1 Julai, 2007 mishahara mipya iliyoahidiwa. *(Makofi)*

Hadi sasa nimekwishapata orodha ya wachangiaji 37, wala tusishtuke mwaka jana kwenye Mkutano wa Nne tulipata wachangiaji 76. Kwa hiyo, mlango bado uko wazi nakaribisha wale ambao watapenda kuchangia katika hotuba hizi mbili. Katibu ataendelea kupokea karatasi hizo. *(Makofi)*

Nawajibika Waheshimiwa kuwatambua wageni mashuhuri walioungana nasi kwa siku ya leo ambao wamekaa pale *Speaker's Gallery* na nitaomba nikiwataja waweze kusimama ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuwatambua.

*Guests at Speaker's Gallery when I mention your name, your Exellencies, please stand up so that Members of Parliament can acknowledge you.* *(Makofi)*

Nitaanza na Mama, Mheshimiwa Regina Lowassa. Ahsante sana, ahsante karibu sana. *(Makofi)*

Katibu Mkuu Kiongozi, Ndugu Philemon Luhanjo, ahsante sana. Mzee wetu, mmoja wa Mawaziri wa kwanza kabisa katika Uhuru wa nchi yetu, Balozi Sir George Kahama. *(Makofi)*

Sasa wanaofuata ni kama ifuatavyo, Mheshimiwa Balozi wa Nigeria, Mheshimiwa Balozi wa Jamhuri ya Rwanda, Mheshimiwa Balozi wa Burundi, Mheshimiwa Balozi wa Zambia, Mheshimiwa Balozi wa Zimbabwe, labda ana udhuru kidogo, Mheshimiwa Balozi wa Indonesia, Mheshimiwa Balozi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Mheshimiwa Mwakilishi Balozi wa Uganda, ahsante sana. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mwakilishi wa Balozi wa Afrika Kusini, Mheshimiwa Mwakilishi wa Balozi wa Canada, Mwakilishi wa Mheshimiwa Balozi wa Uingereza na Mkuu wa Magereza. *(Makofi)*

Kama nilivyosema Waheshimiwa ni wengi sana, lakini nimetambulisha wale walioko kwenye *Speaker's Gallery.* Gavana wa Benki aah, Mwakilishi wa Benki ya Dunia, *World Bank* aah, *hallow Judith nice to see you.* *(Kicheko/Makofi)*

Mwakilishi wa *IMF* karibu sana, karibu. Kumbe kuna Mabalozi wengine upande ule ambao wala bahati mbaya nina orodha hii. Balozi wa Uholanzi, *The Netherlands. All they are spread out, so it is very difficult for me now, so I ask all the Representatives or His Exellency Ambassadors represented here in Tanzania, please to stand up, the ones that I didn't mention.* Ahsante sana. *(Makofi)*

Gavana Daudi Balali yupo sijui? Aah, ahsante sana karibu. Sijui na Naibu Gavana pengine naye yupo. Nadhani wengine wanaohusika na Wizara kama Katibu Mkuu Ndugu Gray Mgonja, *TRA* pale na kadhalika, wapo kama kawaida kazini. Tutapata nafasi ya kuwatambua na kufanya nao kazi wiki ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ameniomba nimtambulishe dada yake anaitwa Rabia Hamdani ametoka Zanzibar mahususi kwa ajili ya kuja, yule pale kweli. Huyu Binti Hamdani kweli kweli, wanafanana kweli kweli yaani na mwanae Mheshimiwa Waziri, Bi. Jamila Meghji, yule pale. Hawa wawili wamekuja kwa lugha ya kisasa kuja kumpa *tough* Waziri. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi Jumatatu ijayo tarehe 18 Juni, 2007 saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.42 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu,*
*Tarehe 18 Juni, 2007 saa tatu asubuhi)*